# Nipashe

Alhamisi Januari 5, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581181

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS. 1,063,605,974

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ PIGA *150*87#




**Mafuta** yashuka Dar, Kaskazini, Kusini yapanda

UKURASA 3




UKURASA 13

# Kicheko Mbowe kurudi kundini

• **Wapinzani** wasema ataongeza nguvu, Rais Samia amiminiwa pongezi... *uk. 2 & 3*



Hamad Rashid Mohamed



Joseph Selasini



Freeman Mbowe



Juma Khatibu



Prof. Ibrahimu Lipumba

## 11 wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji

UKURASA 4

## Udanganyifu, matusi vyatawala matokeo Kidato cha Pili, la Nne

UKURASA 2


**MICHEZO** **MUDATHIR AHOFIA NAMBA YANGA** UK.32 **MAONI** UK.6




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (katikati), akishuhudia utiaji saini makubaliano ya ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, baina ya Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Fatma Khamis Rajab (kulia) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Mecco Tanzania, Nasser Abdulkadir Sheikh, katika hafla iliyofanyika Ikulu Zanzibar. **PICHA: IKULU**

# Kicheko wapinzani Mbowe kurudi kundini

**Na Elizabeth Zaya**

MWENYEKITI wa Baraza la Vyama vya Siasa, Juma Khatib, amesema kukosekana kwa viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) akiwamo Mwenyekiti wake, Freeman Mbowe, katika mikutano mbalimbali kulikuwa kunawaumiza.

Lakini sasa amesema kuungana nao katika baraza hilo ni faraja kubwa na wana tumaini kuwa ataongeza nguvu zaidi.

Khatib alisema hayo jana Dar es Salaam wakati wa mkutano na waandishi wa habari uliolenga kumshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuruhusu mikutano ya hadhara kwa vyama hivyo pamoja na kuahidi kufufua mchakato wa Katiba.

Khatib alimpongeza Mbowe pamoja na viongozi wote wa chama hicho kwa kukubali kushiriki katika mkutano kati ya Rais Samia na viongozi wa kitaifa wa vyama vya siasa uliofanyika juzi, Ikulu jijini Dar es Salaam.

"Tulikuwa hatujisikii vizuri kwa sababu ni wanasiasa wenzetu. Tulikuwa tunataka waje na wao watoe michango yao lakini sasa tumefurahi mno. Mimi kama mwenyekiti wa baraza la vyama vya siasa, nafurahi kuona wajumbe wangu wote walishiriki katika tukio la jana (juzi).

"Kwa ukomavu mkubwa wa kisiasa, Rais Samia ameuonyesha kwa vitendo na sisi kukaa pamoja na wenzetu jana (juzi) kushiriki katika tukio lile kubwa katika nchi yetu. Tuna kila sababu ya kumpongeza. Vikao na matukio mengi ya kitaifa yamefanyika lakini wenzetu walikuwa wanajitenga, hatukuwa tukifurahishwa. Lilikuwa jambo linalotuumiza moyoni kabisa.

"Lakini ni kiongozi, ameonyesha uwezo na uzalendo mkubwa wa kujishusha yeye kama Rais na kama Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi(CCM), kuzungumza na Watanzania wenzetu ikiwamo hawa wa CHADEMA na nampongeza sana Mbowe pamoja na chama chake kwa kushiriki tukio lile. Hili ni jambo la kihistoria na hii ndio Tanzania tunayoitaka. Tukae pamoja, tushindane kwa hoja bila kugombana, bila kupigana," alisema.

Jambo la maridhiano alilolifanya Rais Samia hadi kuwaleta pamoja wanasiasa wote, alisema linapaswa kupongezwa na kuungwa mkono na kila mtu badala ya kuviachia vyama vya siasa pekee.

"Hii imesababisha kwa haraka nikaitisha kikao hiki cha kutoa kauli ya kumuunga mkono Rais. Kuna mambo mengi yalikuwa yanawakera wananchi lakini yote ameyatolea kauli. Kwa hiyo anastahili kupongezwa na tutaendelea kumpongeza. Kwa niaba ya chama changu cha ADA Tadea, naahidi kwamba tutampatia ushirikiano wa kutosha," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahimu Lipumba, alisema Rais Samia alitumia utashi wa demokrasia kuhakikisha vyama vyote vinakutana Ikulu kwa kuhakikisha CHADEMA wanakuwapo.

"Wakati tumekutana Ikulu, vyama vyote 17 vilikuja pale na wote tulisimama kupiga makofi zile hatua ambazo Rais amezieleza kwamba anapaswa kuzifanya. Kwa hiyo ni jambo la heri kutumia diplomasia kuhakikisha vyama vyote vinashiriki katika kikao kile na ninaamini vyama vyote vitaendelea kushiriki katika mchakato wa kuleta mabadiliko chanya katika nchi yetu," alisema.

Juzi Rais Samia alieleza namna ambavyo ilikuwa vuta nikuvute kuwaweka pamoja upande wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na CHADEMA, kwamba walikaa takriban vikao sita hadi kufanikisha kufikia maridhiano.

# Udanganyifu, matusi vyatawala matokeo Kidato cha Pili, la Nne

**Na Christina Mwakangale**

UDANGANYIFU na matusi kwa mara nyingine yamejiri katika matokeo ya mitihani wa kidato cha pili na darasa la nne yaliyotangazwa jana.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), Athumani Amasi, aliyasema hayo mkoani Dar es Salaam, wakati akitangaza matokeo ya mitihani hiyo, iliyofanyikia Oktoba na Novemba, 2022.

Alisema kutokana na hali hiyo, wanafunzi 279 wamefutiwa matokeo na kati yao 82 ni wa darasa la nne na 213 wa kidato cha pili. Alisema wanafunzi hao wamefutiwa matokeo hayo baada ya kubainika walifanya udanganyifu na 14 wa kidato cha pili waliandika matusi.

"Baraza la Mitihani limefuta matokeo yote ya wanafunzi waliobainika kufanya udanganyifu wakiwamo 14 walioandika matusi katika upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili mwaka 2022.

"Natoa wito kwa wazazi, walezi kuacha tabia ya kuwadanganya wanafunzi, watoto wao kwa mbinu tofauti. Ili wafaulu, wawaache wafanye mitihani kwa uwezo wao, wakiandaliwa vizuri watafaulu," alisema Amasi.

Aidha, Amasi alisema kwenye matokeo hayo, upande wa darasa la nne, wanafunzi 1,320,700 kati ya 1,592,235 wamefaulu kwa madaraja tofauti, wasichana wakiwa asilimia 84.76 na wavulana 81.03.

Amasi alisema kati ya wanafunzi hao waliofaulu kwa darasa la nne kwenye somo la Kiswahili 488,722 sawa na asilimia 20.73 walipata daraja C huku 815,875 ambayo ni asilimia 51.28 katika somo la Kiingereza wakipata daraja D.

"Somo la hisabati kwa darasa la nne wanafunzi 800,462 sawa na asilimia 5029 walipata daraja E na somo la sayansi na teknolojia wanafunzi 453,169 walipata daraja C," alisema katibu mtendaj huyo.

Kuhusu ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha pili, Amasi alisema 539,645 kati ya 633,537 wamefaulu kwa madaraja tofauti na kati yao wasichana waliofaulu ni 263,541 sawa na asilimia 83.05 huku wavulana wakiwa 256,104 sawa na asilimia 87.67.

"Masomo ya lugha; Kiingereza na Kiswahili kidato cha pili, takwimu zinaonesha somo la Kiswahili walipata daraja A ni 78,986 sawa na silimia 12.47 na pia somo la Kiingereza wanafunzi 18,920 walipata daraja A," alisema Amasi.

Kadhalika, Amasi alisema kwamba wanafunzi hao wa kidato cha pili, kwenye somo la Fizikia wanafunzi 515,734 sawa na asilimia 91.79 walipata daraja F na katika somo la Kemia 421,138 sawa na asilimia 66.55 wakipata F.

Kwa upande wa somo la hisabati, Amasi alisema wanafunzi hao wa kidato cha pili, walipata daraja F ni 528,344 sawa na asilimia 83.44 na somo la baiolojì wanafunzi 335,847 ikiwa ni asilimia walipata daraja F.

"Baraza la Mitihani Tanzania, limezuia kutoa matokeo ya wanafunzi 442 ambao walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani wa darasa la nne kwa masomo yote au idadi kubwa ya masomo.

"258 walipata matatizo ya kiafya na kushindwa kufanya mtihani ni wanafunzi wa kidato cha pili, nao kwa masomo yote au idadi kubwa ya masomo. Wanafunzi husika wamepewa fursa kufanya mtihani mwaka 2023," alisema katibu mtendaji wa baraza hilo.

# Vyama vyampongeza Samia mikutano, Katiba mpya

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameendelea kumiminiwa pongezi kutokana na uthubutu wake wa kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa na kuanza utaratibu wa kukwamua mchakato wa Katiba mpya.

Jana, vyama vinane vilizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam na kueleza kuwa hivi karibuni vitaanza harakati za kisiasa ikiwamo mikutano ya hadhara ambayo walikuwa 'kifungoni' kwa miaka sita.

Kauli ya vyama hivyo iliungwa mkono na viongozi wa Nyanda za Juu Kusini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na chama cha Alliance for Democratic Change (ADC) kwamba Rais ameonyesha ukomavu, busara na hekima kwenye kuongoza taifa.

Viongozi saba wa vyama vya siasa, jana walikutana Dar es Salaam kupongeza uamuzi wa Rais Samia kwa kuondoa zuio la mikutano ya hadhara kwa vyama hivyo ikiwamo kuahidi kukwamua mchakato wa Katiba.

Wakizungumza na waandishi wa habari, viongozi wa vyama hivyo walisema uamuzi aliofanya Rais Samia ni wa kupongezwa huku wakiahidi kumuunga mkono na kufanya mikutano ya kistaarabu.

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Juma Khatib, alisema baraza hilo litaendelea kumuunga mkono Rais Samia bila kuangalia itikadi za vyama isipokuwa kwa kuzingatia uzalendo, umoja na utaifa.

Alisema kwa muda mrefu vyama vya siasa vilikuwa kifungoni lakini kupitia utashi wa Rais Samia amerejesha furaha hiyo, hivyo hawana budi kumuunga mkono.

Mwenyekiti wa Chama cha Alliance For Democratic Change (ADC), Hamad Rashid Mohamed , alisema kwa uamuzi alioufanya Rais Samia anapaswa kuungwa mkono na vyama vyote bila kujali ni kikubwa au ni kidogo.

"Rais Samia ni kiongozi ambaye anatembea kwenye maneno yake na ni mwenye utashi. Katika hilo tunahitaji kumuunga mkono bila kujali ni chama kikubwa au ni kidogo. ADC tunaahidi kumpa ushirikiano na tunaomba watanzania wote tumuunge mkono," alisema Hamad. Makamu Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, Joseph Selasini, alisema wako tayari kufanya mikutano ya kistaarabu, ili kuuunga mkono uamuzi mzuri alioufanya Rais Samia.

"Kuna watu wanasema kumuunga mkono Rais ambaye ni mwenyekiti wa CCM, ni kuuweka rehani upinzani, haya ni maneno ya kushangaza kwa sababu najiuliza, hivi Rais huyohuyo ambaye ni mwenyekiti wa CCM, angeamua kutoruhusu hiyo mikutano, sisi wapinzani tungejiandaa kufanya nini ili kuipatana hiyo mikutano, au hao wanaosema hivyo, walishajiandaa namna gani kuipata hiyo mikutano.

"Rais alipoingia madarakani, aliingia na neno maridhiano kwa sababu yeye akiwa ndani ya serikali aliona jinsi ambavyo uchangamfu wa Watanzania umepotezwa kwa sababu ya mambo mbalimbali, kwa hiyo uamuzi alioufanya ni mzito sana, tunapaswa kumuunga mkono," alisema.

Vyama vilivyoshiriki katika mkutano huo jana ni ADA Tadea, Democratic Party (DP), ADC, Demokrasia Makini, CUF, NCCR-Mageuzi na UPDP.

Mwenyekiti wa Chama Cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema ni fursa sasa kwa vyama vya siasa kueneza sera, kukosoa mahali ambapo hapaendi vizuri na kupongeza mahali ambapo panaenda vizuri.

Mwenyekiti wa Demokrasia Makini, Ameir Hassan, alisema uamuzi wa Rais Samia umeleta faraja kwa Watanzania.

"Tulikuwa gerezani, tulikuwa tunakonda, vyakula vya vyama vya siasa ni mikutano ya hadhara, tulikuwa hatupati chakula hicho, kwa hiyo Rais ametumia umama wa kuona kwamba watoto wake walikuwa na masikitiko, kauli yake imeleta faraja, hata tukiandika kitabu cha kumzungumzia kitataja, hayo kwa hiyo tuikosoe serikali kistaarabu."

**IRINGA**

Wakizungumza kwa nyakati tofauti mjini Iringa juzi aliyekuwa Mbunge wa Iringa Mjini ambaye pia ni Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, Peter Msigwa, alisema hatua hiyo ya Samia inaonyesha busara na hekima alizonazo katika kuliongoza Taifa.

"Rais Samia ameonesha alama kubwa hapa nchini katika uongozi wake, kitendo hiki alichokifanya siyo kitampa heshima hapa Tanzania bali duniani kote kwa kuwa siasa ni kitu kinachotambulika kila mahali," alisema Msigwa.

Alisema dhamira ya CHADEMA ni kufanya siasa za kistaarabu hivyo watafanya mikutano yao kwa lengo la kutangaza ilani na sera zao kwa wananchi ambazo kwa kipindi kirefu walikosa.

Kamishna wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kupitia Chama cha ADC, Daudi Masasi, alimpongeza Rais Dk. Samia Suluhu Hassan na kikosi kazi kwa kazi nzuri.

Alisema kinachotakiwa ni kutoa elimu ya uraia kwa wananchi na kuikosoa serikali mapungufu ili iweze kuyafanyia kazi ili wananchi wapate huduma stahiki.

"Kufunguliwa kwa milango ya kufanya mikutano ya hadhara ya siasa kumekuwa na faida nyingi kwani kwa muda mrefu tulikuwa hatujaongea na wananchi," alisema Masasi.

**Imeandikwa na Elizabeth Zaya (DAR), Friday Simbaya (IRINGA).**

## Mafuta yashuka Dar, yazidi kupanda Kaskazini na Kusini

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imetangaza kushuka kwa bei ya mafuta ya petroli na dizeli kwa Bandari ya Dar es Salaam huku Tanga na Mtwara, ikipaa.

Mkurugenzi Mkuu wa EWURA, Modestus Lumato, kwenye taarifa yake, alisema bei hizo zitaanza kutumika kuanzia Januari 4, mwaka huu na ya rejareja ya petroli kwa Dar es Salaam imepungua kwa Shilingi nane kwa lita.

Alisema kwa mikoa ya Tanga na Mtwara bei ya petroli imeongezeka kwa Sh. 164 kwa lita hadi Sh. 168 mtawalia, ikilinganishwa na iliyokuwa ikiuzwa Desemba, mwaka jana.

"Bei ya dizeli kwa Dar es Salaam, Tanga na Mtwara imeongezeka kwa Sh. 48.91 na 135 kwa lita, mtawalia. Bei ya mafuta ya taa kwa Bandari ya Dar es Salaam imepungua kwa Sh. 49 kwa lita ikilinganishwa na bei zilizopita," alisema.

Alisema kuongezeka kwa bei hizo, kunasababishwa na mabadiliko ya bei za mafuta yaliyosafishwa katika Soko la Dunia (FOB), gharama za uagizaji mafuta na kuongezeka kwa thamani ya Dola ya Marekani ikilinganishwa na shilingi.

Bei za miji, wilaya na mikoani ni tofauti kutoka sehemu moja kwenda nyingine, kutokana na mafuta yanapochukuliwa na gharama ya usafirishaji.

"Katika kutekeleza bei hizi, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii wanatakiwa kuzingatia bei ya kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika," alisema Lumato na kuongeza:

"Kwa mujibu wa kifungu namba 166 cha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta." Lumato alisema kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa ya petroli kwa bei ya ushindani, bila kuvuka iliyoko kwenye kikomo au kushuka chini ya bei iliyoruhusiwa.

"Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika," alisema Lumato. "Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi, ili kushamirisha ushindani. Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja."

Alisema vituo ambavyo havitaweka bei kwenye mabango, vitapewa adhabu kali kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.

"Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei iliyoelekezwa. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka," alisema mkurugenzi huyo.



HABARI KITAIFA



Kamishna wa Sera wa Wizara ya Fedha na Mipango, Elijah Mwandumbya, akizungumza jijini Dodoma na wanahabari kuhusu kongamano la kwanza la kodi kitaifa lenye lengo la kuongeza ushiriki wa wadau kwenye maboresho ya sera za kodi, linalotarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watu 11 wahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa mauaji mbalimbali

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Sumbawanga iliyoketi Mpanda mkoani Katavi, imewahukumu kunyongwa hadi kufa watu 11 kati ya 16 waliokuwa wakishtakiwa kwa mauaji, yaliyotokea kwa nyakati tofauti maeneo mbalimbali.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Abubakar Mrisha huku waliokumbwa na adhabu hiyo wakiwa ni Masanja Kitalya (32) ambaye alitenda kosa hilo Aprili 22, 2018 katika kijiji cha Ilunde, wilaya ya Mlele mkoani Katavi.

Jaji Mrisha alisema Kitalya alishtakiwa kwa kumuua mtoto Kundi Masanja mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi minane kwa kumkata na kitu chenye ncha kali shingoni huku chanzo kikitajwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Ilidaiwa kuwa Kitalya alimtuhumu baba wa mtoto huyo kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mke wake na kabla ya kutekeleza mauaji hayo, alifika katika familia hiyo kumtafuta baba wa mtoto huyo na mara ya mwisho aliambiwa amekwenda kanisani.

Baada ya kuona amemtafuta kwa muda mrefu bila mafanikio, alikwenda tena katika nyumba hiyo na kuwakuta watoto peke yao waliokuwa na uwezo wa kukimbia walikimbia, akabaki mtoto huyo mdogo, hivyo kuamua kumkata shingo.

Baada ya kutekeleza mauaji hayo, alijaribu kujiua kwa kutumia shati lake lakini ilishindikana baada ya shati hilo kuchanika na hatimaye kuchukua uamuzi wa kujisalimisha polisi.

Katika kesi nyingine, Chiba Kulwa (30), Thomas Malongo (54), Masesa Lwenganija (33) na Mganga Luchagula (38) wote kwa pamoja walishtakiwa Mei 10, 2020 kwa madai ya kumuua baba yao, Lumba Daudi (57), katika kijiji cha Kasekese, wilaya ya Tanganyika mkoani Katavi kwa kumkata na kitu chenye ncha kali kisha kumchuna ngozi sehemu zake za siri na kuondoka nayo.

Chanzo cha tukio hilo ilidaiwa ni tamaa za mali na imani za kishirikiana. Ilidaiwa kuwa kabla ya kutekeleza mauaji hayo, walimnywesha pombe nyingi baba yao kiasi cha kushindwa kujitambua, hivyo wakati wakirudi nyumbani, walitekeleza mauaji hayo.

Wengine waliohukumiwa ni Shimba Igishaminaza, Mahangila Timba, Lyande Salu na Mbeje Salu, ambao wote kwa pamoja walishtakiwa kwa madai ya kumuua Mwasi Mahangila kwa kumtuhumu kuwa ni mchawi.

Washtakiwa hao kwa kushirikiana na Seif Mgelwa na Giliad Elihuruma, kwa pamoja walidai kutenda makosa hayo kinyume na kifungu cha 196 na 197 vya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16.

Mahakama hiyo ilitumia siku mbili kusikiliza kesi sita za mauaji zilizowahusisha washtakiwa 16, huku 11 ambao majina yao yametajwa, walipatikana na hatia na wengine watano waliachiwa huru kutokana na ushahidi dhidi yao kuwa dhaifu.

# Katoliki nchini lamlilia Papa Benedict wa 16

**VATICAN,** ROMA

VIONGOZI mbalimbali wakiwemo Askofu Mkuu Gervaz Nyaisonga, Rais wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Mbeya, wametoa salamu za rambirambi kutokana na kifo cha Papa mstaafu Benedict XVI.

Katika ujumbe wao walioutoa jana, walitoa salamu za pole kwa waliyemuita Baba Mtakatifu Fransisko na Kanisa zima, wakimshukuru Mungu kwa maisha mazuri ya mja wake, huku wakimtakia Papa huyo pumziko la milele.

"Ulimwengu mzima umepokea kwa masikitiko makubwa habari za kifo cha Papa Mstaafu Benedict XVI kilichotokea alfajiri ya 31 Desemba 2022 Mungu ampe pumziko la milele," walisema.

Viongozi wengine ni Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Munich na Frisinger alikokuwa anatoka Papa Mstaafu, ambao pia walimwombea Papa huyo pumziko la milele.

Rais wa Baraza la maaskofu Australia naye alituma salamu za rambirambi, kwa niaba ya kanisa zima, Baraza la Maaskofu Italia (CEI), Hungaria, Ujerumani na Shirikisho la Mabaraza ya Maaskofu Ulaya.

Wengine ni ujumbe kutoka kwa Askofu Mkuu, Justin Welby wa Kanisa la Kianglikani Canterbury, Uingereza na Baraza la Maaskofu Katoliki wa Uingereza na Walles.

Umoja wa Wabudha Italia pia walituma ujumbe wao wakionyesha uchungu na kuungana na Kanisa Katoliki la Italia na ulimwengu kwa ajili ya kifo cha Papa Mstaafu Benedict XVI.

Walieleza kuwa wanamkumbuka alivyo kuwa na wazo la kina na utafiti wa ki-Mungu na umakini wa majadiliano ya kidini, na kwamba kimo chake kama msomi mzuri kililingana na upole wake.

Pia walibainisha kuwa kujiuzulu kwake katika kiti cha upapa ilikuwa ni ishara iliyoshangaza ulimwengu mzima na jumuiya ya waamini katika imani yeyote.

Inaelezwa kuwa ujumbe mwingi kutoka katika jamii mbalimbali Duniani, viongozi wa vyama vya kisiasa pia walielezea masikitiko na shukrani kwa Papa mstaafu kwa yote aliyotendea kanisa lote, dini zote bila ubaguzi na kwa jamii nzima.

**Chanzo: VATICAN NEWS**

# Wafurahia kuondokana na adha ya maji

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKAZI 39,424 wa kata za Kilakala na Bigwa katika Manispaa ya Morogoro, wameondokana na adha ya maji baada ya uzinduzi wa mradi katika tangi la Bigwa uliogharimu Sh. Bilioni 2.4 kukamilika.

Mmoja wa wananchi hao, Suzana Ditto, alisema awali walilazimika kutembea umbali mrefu wa hata kilometa saba hadi 10 kutafuta huduma ya maji na pengine kununua maji ya madumu yanayotembezwa mitaani yakiuzwa Sh. 500 hadi 600 kwa dumu la lita 20.

Alisema anaishukuru serikali kupitia kwa Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, kupeleka maombi ya kero ya maji iliyodumu kwa takriban miaka 10.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), Tamimu Katakweba, alisema mradi wa maji Bigwa-Bohmela ulianza kutekelezwa Desemba Mosi, 2020 na kukamilika Juni 30, mwaka jana.

Alisema mradi huo unahudumia maeneo ya Bigwa - Kisiwani, Bohmela, Mwanzo Mgumu, Bigwa- Ualimu, Bigwa-Sokoni, Bigwa - Sisters, Misongeni, Bigwa - Lukuyu, Bigwa- Makuti, Bigwa - Relini na mtaa wa Chuo Cha Maendeleo.

Mbunge Abood aliishukuru serikali kwa kuitikia na kumjibu kilio cha maji katika Manispaa ya Morogoro ambayo ilikuwa kero kubwa kwa wananchi.

"Ilikuwa kila siku lazima nipokee simu za malalamiko ya maji kwenye kata za Kilakala na Bigwa. Sasa nimeanza kupumzika, sizipati simu zao. Ni jambo la kujivunia uwapo wake Rais Samia na Waziri wa Maji (Jumaa Aweso)," alisema.

Akizindua mradi huo, Aweso aliwataka wahandisi wa maji kuhakikisha wanatoa huduma za maji kwa wateja wanaoomba haraka na kuepusha maombi ya wateja kukaa muda mrefu bila majibu hadi waanze kulalamika.

Waziri alisema kuna utaratibu mbovu wa kuchelewa kutoa huduma za maji kwa wateja bila kuwa na sababu yoyote jambo ambalo si sahihi kwa watoa huduma hasa za serikali kwa jamii.

Aweso aliagiza watoa huduma za maji kuweka ushirikiano na wananchi wakati wa kutoa huduma ili kuepusha malalamiko ya wananchi kuzidishiwa bili.

# Namna Tanzania ilivyojizatiti kukabili UVIKO-19, ebola

**Na Elizabeth Zaya**

UGONJWA wa ebola ulioripotiwa katika nchi jirani ya Uganda ni miongoni mwa mambo yaliyotishia Tanzania mwaka 2022 kwa kuzingatia ujirani na nchi hiyo.

Ugonjwa wa UVIKO-19 licha ya kuripotiwa tangu mwaka 2020 nchini, mwaka jana uliwakumba baadhi ya watu huku serikali ikiudhibiti kwa kuendelea kuhimiza wananchi wake kuchanja kupunguza athari zaidi.

Taarifa za ugonjwa wa ebola kuingia Wilaya ya Mubende nchini Uganda, zilizua hofu kwa Tanzania na kuchukua tahadhari hasa kwenye mipaka yake.

Wilaya ya Mubende iko umbali wa kilomita 230 kwenda mpaka wa Mutukula kupitia Masaka na kilomita 220 kutoka Kampala hadi Mutukula mkoani Kagera na mwingiliano wa shughuli za kiuchumi na kijamii kupitia mipaka rasmi na isiyo rasmi.

Baadhi ya mikoa iliyotangazwa na Serikali ya Tanzania kuwa kwenye tishio la ugonjwa huo ilikuwa ni Kagera, Mwanza, Geita, Mara na Kigoma.

Mikoa mingine ilikuwa ni Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Songwe, Mbeya na Dodoma kama mikoa iliyokuwa katika hatari ya kati kutokana na mwingiliano wa viwanja vya ndege na vituo vya mabasi yanayotoka nchi jirani.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, Septemba 28, mwaka jana akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, alisema japokuwa ugonjwa huo haukuingia, lakini Tanzania ilikuwa kwenye hatari kubwa kupata kutokana na ukaribu wa eneo lililoathirika.

Tanzania ilichukua hatua za haraka ikiwamo kupeleka timu ya wataalamu ya kukabiliana na magonjwa ya milipuko katika mikoa iliyo kwenye hatari zaidi na maeneo yote ya mipaka.

Serikali ilitoa agizo kwa wakuu wa mikoa yote nchini na halmashauri kuandaa mpango wa kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo, kuimarisha ufuatiliaji na kutoa taarifa ya wanaohisiwa kuwa na dalili za ugonjwa huo katika maeneo yao kupitia mfumo wa magonjwa ya mlipuko na yanayopewa kipaumbele (IDSR).

Ili kuhakikisha waganga wakuu wa mikoa wanatoa taarifa sahihi kwa wakati kwa Mganga Mkuu wa Serikali kuhusu tetesi za watu wanaohisi kuwa na dalili za ugonjwa huo.

Pia, kufuatilia ukaguzi wa afya za wasafiri wanaoingia nchini hususani kutoka nchi zilizoathirika, kuimarisha timu za haraka za kukabiliana na magonjwa ya mlipuko ndani ya mikoa yao.

Ilijipanga kuanza kutoa elimu kwa wananchi kuhusu ugonjwa huo na jinsi ya kujikinga, iliandaa na kuimarisha vituo vya matibabu ya wagonjwa kwa kila halmashauri, kuhakikisha dawa zipo.

Uwapo wa dawa, vifaa tiba na kinga kwa ajili ya wagonjwa na watumishi wa afya katika maeneo yote muhimu.

Wataalamu waliweka kambi katika maeneo mbalimbali ya mipaka na mazingira ya kila mtu kunawa mikono kwa maji tiririka katika ngazi ya kaya, taasisi, sehemu za biashara, stendi za mabasi, shuleni, nyumba za ibada na maeneo yote ya mikusanyiko na iliimarisha timu za haraka za uratibu ngazi zote ikiwa ni pamoja na kufanya mafunzo kwa timu mbalimbali za wataalamu, kuimarisha uchunguzi wa wasafiri katika maeneo ya mipaka hususani yenye mwingiliano mkubwa na nchi ya Uganda.

Serikali iliimarisha huduma za upimaji katika Mkoa wa Kagera na kuweka huduma za maabara tembezi, kuhakikisha uwapo wa vituo vya kuwahudumia wagonjwa watakaothibitika, ilipita nyumba kwa nyumba kutoa elimu na iliimarisha mfumo wa usafirishaji wa sampuli.

Kadhalika, kwa upande wa UVIKO-19, mwaka jana visa vya wagonjwa kuripotiwa nchini viliendelea ingawa hakukuwa na madhara makubwa kutokana na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na serikali kukabiliana na mlipuko huo ikiwamo kuleta chanjo nchini.

Hadi kufikia Desemba 2, mwaka jana, jumla ya wagonjwa wapya 442 walithibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO-19, lakini hakuna aliyelazwa na jumla ya watu 29,123,387 kati ya walengwa 30,740,928 ambao ni sawa na asilimia 94.7 walikuwa wamepata dozi kamili ya chanjo ya ugonjwa huo.

Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani, Charles Kitwanga, aliipongeza serikali kwa namna ilivyojipanga mwaka jana kudhibiti ugonjwa wa ebola na kutoa ushauri wa kuboresha zaidi eneo la majanga.

Alisema ni muhimu kusikiliza ushauri wa kitaalamu unaohusu mambo hayo na kuufanyia kazi haraka.

Kitwanga ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Misungwi alisema ni muhimu pia kuweka mfuko maalumu wenye rasilimali watu na fedha za kutosha ambao utakuwa tayari kwa ajili ya kukabiliana na majanga ya aina yoyote wakati wowote na kwa haraka.

“Nadhani hapa tujifunze kwa kile kilichotokea pia katika Mlima Kilimanjaro, ule mto uliowaka na tukio lililotokea kule mkoani Kagera kwa ajali ya ndege,” alisema Kitwanga.

“Kwenye eneo la ebola tulishuhudia serikali ilifanya vizuri, lakini katika matukio haya mawili la moto kwenye Mlima Kilimanjaro na ajali ya ndege mkoani Kagera haya tulijifunza kwamba bado hakukuwa na utayari wa haraka wa kukabiliana na matukio haya.

“Inawezekana rasilimali watu ilikuwapo, lakini je, kulikuwa na uwezeshwaji wa haraka wa kuhakikisha watu wanafika eneo la janga au tukio? Kwa hiyo ni vyema kukawa na mfuko wa fedha za kutosha ambao kila mwaka unakuwa tayari na hata kama hakujatokea tukio mwaka huo, inahamishwa na kupelekwa mwaka unaofuata, usiguswe na ikiwezekana tupunguze kuwa na matumizi makubwa kwenye baadhi ya maeneo ili fedha hiyo tuweke kwenye majanga.”

Mkurugenzi Mtendaji wa zamani wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, Kijo Bisimba, alisema ni vyema mikakati ya kukabiliana na masula ya majanga inapopangwa isiwe ya muda mfupi.

“Ni vema mikakati ya majanga inapopangwa isiwe ya muda mfupi, waiandae iwe endelevu maana milipuko ipo tu, wawe na kitu kinaitwa ‘preparedeness’ wakati wote, pasiwe na hali ya kupoa kama ambavyo masuala ya COVID-19 na kipindupindu yameanza kusahaulika.”


Canara Bank (Tanzania) Lt

(Together we can build a better li

## PUBLICATION OF INTEREST RATES, FEES AND CHARGES

**PURSUANT TO REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS DISCLOSURE REGULATION, 2014 AND REGULATION 40(3)(a) OF THE FINANCIAL CONSUMER PROTECTION 2019.**

| | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| **A. SAVINGS BANK** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges | | | | |
| a) Monthly | | FREE | | FREE |
| b) Interm | | TZS 4,300.00 | | $ 5.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | | FREE | Up to 5000 | FREE |
| | | | Above 5000 | 0.26% |
| 5. Cash Deposit Charges | | FREE | | FREE |
| 6. Balance Confirmation certificate | | TZS 12,800.00 | | $ 6.00 |
| 7. A/c Closure charges | | TZS 12,800.00 | | $ 13.00 |
| 8. Activation of Dormat A/c | | TZS 5,100.00 | | $ 6.00 |
| **B. CURRENT ACCOUNT** | | | | |
| 1. Monthly Maintanance Charges | | FREE | | FREE |
| 2. Non Maintanance of Minimum Balance | | FREE | | FREE |
| 3. A/C Statement Charges a) Monthly | | TZS 4,300.00 | | $ 5.00 |
| b) Interm | Fixed | TZS 4,300.00 | Fixed | $5.00 |
| | plus For each page | TZS 500.00 | For each page | $1.00 |
| 4. Cash Withdrawl Charges | UPTO 25 MILLION | FREE | Upto 5000 | FREE |
| | ABOVE 25 MILLION | 0.11% | 5000 to 10,000 - | 0.26% |
| | | | Above 10,000 | 0.43% |
| 5. Cash Deposit Charges | UPTO 50 MIO | FREE | Upto 10,000 | FREE |
| | ABOVE 50 Million | 0.11% | > 10,000- | 0.26% |
| 5. Balance Confirmation certificate | | TZS 21,200.00 | | $13.00 |
| 6. Stop Payment Charges | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| 7. Cheque Clearing Charges | | | | |
| a) Inward | | TZS 1,300.00 | | $1.00 |
| b) Outward | | FREE | | FREE |
| 8. Cheque Return Charges | | | | |
| a) Inward | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| b) Outward | | TZS 25,500.00 | | $13.00 |
| 9. A/c closure charges | | TZS 21,200.00 | | $17.00 |
| **C. MOBILE BANKING CHARGES** | | | | |
| **1. Cash Withdrawal** | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS 1,700.00 | | NA |
| 101,000 to 200,000 | | TZS 2,600.00 | | NA |
| 201,000 to 400,000 | | TZS 4,300.00 | | NA |
| 401,000 to 600,000 | | TZS 5,100.00 | | NA |
| 601,000 to 999,000 | | TZS 6,800.00 | | NA |
| **2. Funds Transfer/Mobile Wallet** | | | | |
| Upto 100,000 | | TZS 500.00 | | NA |
| 101,000 to 250,000 | | TZS 900.00 | | NA |
| 251,000 to 500,000 | | TZS 1,700.00 | | NA |
| 501,000 to 1,000,000 | | TZS 4,300.00 | | NA |
| 1,001,000 TO 10 Mn | | TZS 8,500.00 | | NA |
| **Mobile Banking Services** | | | | |
| A) Monthly Subscription Charges | | TZS 500.00 | | NA |
| B) PIN Request | | TZS 2,200.00 | | NA |
| **D. LOCKERS RENT YEARLY** | | | | |
| 1.SMALL | | TZS 296,700.00 | | NA |
| 2. MEDIUM | | TZS 508,500.00 | | NA |
| 3. BIG | | TZS 635,600.00 | | NA |

| E. REMITTANCES | TZS | | USD | |
|---|---|---|---|---|
| 1. TISS | | TZS 8,450.00 | | EQUIVALLENT TO TZS 8450 |
| **2. E Remittances** | | | | |
| Upto USD 1000 or Eq. TZS | | TZS 17,000.00 | | $ 9.00 |
| 1001 to 5000 | | TZS 20,400.00 | | $ 11.00 |
| 5001 to 10000 | | TZS 40,700.00 | | $ 22.00 |
| 10,001 and above | | TZS 84,800.00 | | $ 43.00 |
| **3. SWIFT** | | | | |
| **a) Swift Outward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | | $ 39.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | | $ 51.00 |
| above 10,000 | | NA | | $ 77.00 |
| **b) Swift Inward** | | | | |
| Upto 5,000 | | NA | | $ 11.00 |
| 5,001 to 10,000 | | NA | | $ 16.00 |
| above 10,000 | | NA | | $ 26.00 |
| **F. LOAN/ADVANCES RELATED CHARGES** | | | | |
| 1. Processing Charges | Upto 5 Mio - | TZS 21,200.00 | Upto 5,000 - | $85.00 |
| | 5Mio to 10 Mio - | TZS 169,500.00 | 5000 to 10,000 - | $170.00 |
| | 10 Mio to 25mio - | TZS 339,000.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.28% | 20,000 to 500,000 - | 1.28% |
| | >500mio--* (*minimum 7.5mio) | 1.06% | >500,000--* (*minimum 7,500) | 1.06% |
| 2. Documentation Charges | Upto 100 MILLION | FREE | Upto 50,000 | FREE |
| | >100 Mio (-Min 300,000) | 0.26% | >50,000 - (Min 150) | 0.26% |
| 3. Upfront fee on Term Loan | Upto 5Mio - | TZS 21,200.00 | Upto 20,000 - | $255.00 |
| | 5 Mio to 10 Mio - | TZS 169,500.00 | 20,000 to 500,000 - | 1.53% |
| | 10Mio 25mio - | TZS 381,400.00 | >500,000--* (*minimum 9000) | 1.28% |
| | 25 mn to 500 mio - | 1.53% | | |
| | >500mio--* (*minimum 9mio) | 1.28% | | |
| 4. Inspection Charges | Upto 100 Mio - | TZS 21,200.00 | Upto 50,000 | $22.00 |
| | >100 mio - | TZS 42,400.00 | >50,000 | $43.00 |
| 5.Credit Reference Report Charges from D&B Tanzania | TZS | TZS 101,700.00 | | $43.00 |
| 6.Pre-payment penalty | Calculated as %ge pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% | of pre-paid amount in the case of takeover of liability by other | 1.70% |
| **G. Guarantees (Local & International)** | | | | |
| Bonds & Guarantees | ( Min TZS 75,000) | 1.02% | | 1.02% |
| Bonds & Guarantees with 100 % Cash Margin | per quarter (Min TZS 75,000) | 0.43% | | 0.43% |
| **H. LETTER OF CREDIT** | | | | |
| **Import Letter of Credit (per qrtr of Part thereof)** | | | | |
| Opening commission | NA | | ( Min $ 200) | |
| LC amendment Commission | NA | | ( Min $50 max 350) | 1.02% |
| Swift charge for LC opening | NA | | | 0.34% |
| Swift charge for other message/amendments | NA | | | $34.00 |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | $34.00 |
| LC cancellation charges | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Non payment of Bills on due date | NA | | Till Payment | 1.02% |
| **Export Letters of Credit (per quarter or part thereof)** | | | | |
| Advising commission | NA | | | $119.00 |
| Confirmation Commission | NA | | ( Min $150) | 0.43% |
| Negotiating bills under LC | NA | | (Min $75+cuourier+int) | 0.43% |
| Reimbursement claim paid | NA | | ( Min$75) | 0.43% |
| Extensions - Commissions | NA | | ( Min $200) | 1.02% |
| Collection of Export LC | NA | | (Min) $75+cuourier+int | 0.43% |
| Amendments | NA | | | $64.00 |

### OTHER DISCLOSURES(VIAMBATANISHI)

| | TZS | USD |
|---|---|---|
| 1. Base or Prime Lending Rate | 16 | 7 |
| 2. Maximum spread above Base or Prime Lending Rate | 5 | 5 |
| 3.Penal Interest | | |
| a. For non compliance on Terms of Saction | 3% p.a over regular rate of interest | |
| b. For Overdrawing/Excess drawing due to non payment of interest/installment/charges | 5% p.a over regular rate of interest | |
| 4. Deposit Rates | | |
| a. Current account | Nill | Nill |
| b. Savings bank deposit | 3.00% | 1.00% |

**i. Fixed Deposits of TZS**

| Amount in TZS | up to TZS 50 Million | Over TZS 50 Million | Above 100 Million |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 3.50% | 4.50% | 5.50% |
| 91-180days | 4.50% | 5.50% | 6.50% |
| 181-364 days | 5.50% | 7.00% | 7.50% |
| Above 1 year | 8.00% | 8.25% | 8.50% |

**ii. Fixed Deposits of USD**

| Amount in USD | up to USD 50,000 | Over USD 50,000 | Over USD 100,000 |
|---|---|---|---|
| 30 -90days | 1.50% | 2.25% | 2.50% |
| 91-180days | 2.00% | 2.75% | 3.25% |
| 181-364 days | 2.50% | 3.00% | 3.50% |
| Above 1 year | 3.00% | 3.50% | 4.00% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| JOHN CHARLES | GM-OPERATIONS | SIGNED | 04-01-2023 |
| SALMA MRISHO | HEAD TREASURY AND TRADE FINANCE | SIGNED | 04-01-2023 |
| KAUSHENDRA TIWARI | GM-CREDIT | SIGNED | 04-01-2023 |

217215301

Canara Bank (T) Ltd, Head Office Dar Es Salaam Branch,Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania , 2112532, www.canarabank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuandika matusi kwenye mitihani utovu wa nidhamu

**MATUSI** kujiri katika matokeo ya mitihani ya kidato cha pili na darasa la nne yaliyotangazwa jana ni ishara kuwa baadhi ya wanafunzi wamekosa nidhamu na umakini kwenye masomo na matokeo yake kuandika lugha isiyofaa.

Hali hiyo imejitokeza baada ya Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), Athumani Amasi, kutangaza matokeo ya mitihani ya kidato cha pili na darasa la nne iliyofanyikia Oktoba/Novemba, mwaka jana.

Matukio ya wanafunzi kuandika matusi au kuchora picha badala ya majibu ya maswali wanayoulizwa kwenye mitihani hiyo ni dalili kuwa wapo darasani, lakini hakuna umakini kwenye masomo.

Vile vile, wazazi au walezi wanapaswa kufuatilia maendeleo ya masomo ya watoto wao kila siku kwa kuwauliza maswali ya walichofundishwa shuleni na kuangalia madaftari yao kujua kama wanaenda sawa na wanachofundishwa.

Katika matokeo hayo imebainika kuwa wanafunzi 279 wamefutiwa matokeo, kati yao 82 ni wa darasa la nne, na 213 ni wa kidato cha pili baada ya kufanya udanganyifu na 14 wa kidato cha pili kuandika matusi.

Baraza la Mitihani limeamua kufuta matokeo yote ya wanafunzi waliobainika kufanya udanganyifu na walioandika matusi katika upimaji wa kitaifa wa kidato cha pili mwaka 2022.

Lawama zimeenda kwa baadhi ya wazazi na walezi wanaodaiwa kuwadanganya wanafunzi, watoto wao kwa mbinu tofauti ili wafaulu.

Wazazi hao wanatakiwa kuwaacha watoto wao wafanye mitihani kwa uwezo wao na kama wakiandaliwa vizuri, hakuna kitakachoshindikana, watafanya vizuri na kufaulu.

Tabia ya baadhi ya wazazi kuwanunulia mitihani watoto wao ili waweze kufaulu mitihani, haiwasaidii kwa kuwa mwanafunzi atajaza majibu na kufaulu, lakini akimaliza shule hakuna atakachoelewa.

Ni vyema mtoto aachwe ajisomee ili aelewe anachojifunza hata akitoka shule anakuwa na maarifa ya kile alichofundishwa na kukielewa.

Mitihani mingine wanayouziwa wanafunzi si ya kweli matokeo yake anapokutana na maswali ambayo hakuyatarajia anaishia kuchora picha na kuandika matusi kama ilivyobainika katika matokeo yaliyotangazwa jana.

Katika matokeo hayo, Darasa la Nne, wanafunzi 1,320,700 kati ya 1,592,235 wamefaulu kwa madaraja tofauti, huku wasichana wakiwa ni asilimia 84.76 na wavulana 81.03.


Idadi ya wanafunzi waliofanya vizuri inatia moyo na ingeweza kuongezeka kama wanafunzi wote wangezingatia walichofundishwa na kuacha kutegemea mitihani ya udanganyifu.

Kadhalika idadi ya wanafunzi wa kidato cha pili, 539,645 waliofaulu kati ya 633,537, imeonesha jinsi wanafunzi walivyoonyesha bidii katika masomo na wachache ambao hawakuwamo kwenye orodha hiyo, wangeweza kufanya vizuri kama wangezingatia walichofundishwa na walimu wao.

Uzingatiaji wa masomo kwa wanafunzi ni jambo muhimu sana, ndio maana serikali iliamua kufanya mitihani ya darasa la nne na kidato cha pili ili kuangalia kama wanafunzi wanakwenda na wanaelewa wanachofundishwa badala ya kumuacha aendelee mpaka darasa la saba na kutoka akiwa mtupu kichwani.

Mitihani ya majaribio ina umuhimu wake inamsaidia mtoto kujielewa, mzazi kumfahamu mtoto wake na mwalimu kujua upungufu alio nao mwanafunzi wake ili aweze kumsaidia afanye vizuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Christina Mwakangale

## Muungwana Lazima Nilonge

# Fikra kubwa za uwekezaji mkubwa zitalivusha taifa mgawo maji, umeme

**MARA** zote katika mafanikio yeyote huanza ndoto, mtazamo na hata kutazama na kujifunza kutoka kwa wengine. Ndipo linapokuja suala la uwekezaji.

Uwekezaji, aidha wa muda mfupi, kati na mrefu hufanyika popote hata kwa mataifa ambayo sasa yameendelea, kwa kuwa vipaumbele katika jamii kwanza ni huduma zao, ikiwamo maji na nishati.

Tanzania, imo kwenye orodha ya hazina hizo, kwa kujaliwa miongoni mwa nchi duniani hususan barani Afrika, ambazo zimezungukwa na vyanzo vya asili vya maji, yaani Maziwa Makuu, achilia mbali Bahari ya Hindi na mito mikubwa kama Msimbazi, Ruaha na Rufiji.

Maziwa hayo ni Ziwa Victoria, Nyasa na Tanganyika ambayo kijiografia yamekaa kikanda, kwa maana Kaskazini, Magharibi na Kusini huku Masharíki chanzo kikuu kikiwa Bahari ya Hindi.

Mito ndio usiseme iliyopo kwenye mikoa, wilaya yenye ukubwa wa kutosha, ikiwamo Ruaha, Msimbazi, Rufiji, Ruvu na mingine mingi midogo iliyojaaliwa maji karibu msimu wote wa mwaka.

Ziwa Tanganyika, lenye urefu kilomita za mraba 32,900 ipo Kanda ya Ziwa, pia Ziwa Nyasa lina kilomita za mraba 29,600, hali kadhalika Ziwa Rukwa lenye ukubwa wa kilomita za mraba 5,760.

Kwa mujibu wa takwimu za Wikipedia, Ziwa Natron, Manyara, Burigi zote kwa ujumla, zinakadiriwa kuwa na kilomita za mraba za kutosha.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa), pamoja na shirika la umeme nchini - Tanesco, mwezi uliopita walitangaza mgawo wa maji kwa maeneo mengi ya mji wa Dar es Salaam na hata Pwani wanaotegemea chanzo cha maji cha Ruvu Juu na chini na umeme pia nchi nzima.

Mfano, nchi ya Libya iliyoongozwa na Muamar Gadaffi, ilitengeneza mto bandia 'Great Man Made River' na kufuta taswira ya uhaba wa maji kwenye nchi hiyo ambayo ipo Kaskazini mwa bara la Afrika.

Nchi hiyo kwa kiwango kikubwa, imetawaliwa na Jangwa la Sahara, kwa makadirio mto huo bandia, ndio mradi mkubwa zaidi wa uhandisi kuwapo duniani.

Mradi umetawaliwa na mfumo mkubwa wa mabomba na mifereji ya maji, ambayo pia inajumuisha visima zaidi ya 1,300 na kina cha zaidi ya mita 500, hutoa huduma miji ya Tripoli, Benghazi, Sirte na mingine, kusambaza mita za ujazo 6,500,000 kwa siku moja.

Pia, mto huo umo kwenye 'Ajabu la Nane Duniani' na mwaka 2008, kitabu cha kumbukumbu cha Guinness kiliutambua mto huo, kama mradi mkubwa zaidi wa umwagiliaji duniani.

Mnamo Septemba Mosi mwaka 2010, ni tarehe ya kumbukumbu ya kufunguliwa sehemu kuu ya mto huo bandia wa Libya na mradi huo unazidi miradi mikubwa ya ujenzi, gharama yake ni dola bilioni 25.

Wapo watakaodhani kwamba hatua hiyo utekelezaji wake ni mgumu mahali pengine, hiyo si sawa kwa kuwa utaratibu na vipaumbele muhimu ni kutatua changamoto kwenye jamii na suluhisho la kudumu.

Hata ipite miaka kadhaa ya utekelezaji ni bora, kwa kuwa suluhisho litakuwa la kudumu. Yaani vyanzo vya maji viwepo kusiwepo na ndoto ya aina hii, kipi bora, mikakati ya muda mrefu ya mgawo wa maji ambao athari zipo wazi, kwanza, kushuka uchumi miongoni mwa jamii na mlipuko wa maradhi.

Pia, ikumbukwe ripoti mpya iliyochapishwa na Shirika la Afya Dunian (WHO) mwaka 2017, kwa niaba ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Maji, inaonya nchi nyingi ambazo hazijaongeza kasi ya kutosha kwa kutenga fedha kutumika ili kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), kwa matumizi ya maji safi.

Ripoti hiyo inasisitiza kwamba nchi zinapaswa kuongeza jitihada za kutambua vyanzo vipya vya fedha ili kuhakikisha upatikanaji wa maji safi ya kunywa na kudhibiti magonjwa ambayo yanasababishwa na watu kunywa maji machafu.

WHO kupitia Idara ya Afya ya Umma, Mazingira na masuala ya kijamii, ikasema karibu watu bilioni mbili wako hatarini kuambukizwa kipindupindu, kuhara damu, kupata homa ya matumbo na polio kutokana na kunywa maji machafu ambayo yanaweza kuwa na mchanganyiko wa kinyesi.

Shirika hilo linasema, maji machafu ya kunywa yanakadiriwa kusababisha vifo vya zaidi ya watu laki 500,000 kila mwaka.

# Mwandishi aachiwa huru kesi ya rushwa

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Arusha imemwachia huru Mwandishi wa Gazeti la Jamhuri, Hyasinti Mchau, baada ya kubaini hakutenda makosa aliyoshtakiwa nayo ya kushawishi na kupokea rushwa ya Sh. milioni mbili kutoka kwa mfanyabiashara.

Mchau aliachiwa huru hivi karibuni mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Bittony Mwakisu baada ya kupitia ushahidi wa pande zote mbili.

Mchau alikuwa akidaiwa kutenda kosa kati ya Desemba 25 na 26 mwaka 2021 jijini Arusha.

Inadaiwa alishawishi na kupokea rushwa ya Sh. milioni mbili kutoka kwa Salehe Salim Saleh, kama kishawishi ili asichapishe tuhuma za uwindaji haramu zinazomkabili.

Katika kesi hiyo, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) iliwakilishwa na mawakili wa serikali Hamisi Simbano, Hellen Osajuki, Reuben Maduhu na Halima Saidi wakati upande wa utetezi uliwakilishwa na Wakili Ally Mhyellah.

Upande wa Jamhuri ulikuwa na mashahidi wanne na mshtakiwa alijitetea kwa kukana mashtaka yanayomkabili.

Mchau katika ushahidi wake, alidai ni mwandishi kwa miaka 27 na kwamba kesi hiyo ilikuwa ya kutengenezwa kwa lengo la kumfanya asiendelee na uchunguzi wake kwa ajili ya kuandika habari za tuhuma zinazomkabili Saleh.

Saleh katika ushahidi wake alidai aliambiwa anajihusisha na uwindaji haramu kupitia Kampuni yake iitwayo Sunset Tarangire yenye ofisi zake maeneo ya Kijenge, Arusha. Alidai kibali chao ni kwa ajili ya Hifadhi ya Selous na wilayani Kiteto.

Saleh alidai kuwa Desemba 23, 2021 alipokea simu kutoka kwa mwandishi huyo wa gazeti la Jamhuri akataka rushwa ya Sh. milioni mbili na asipompa fedha hizo picha zake kuhusu uwindaji haramu anaofanya zitatoka gazetini.

Desemba 24, 2021 alidai kuwa aliripoti Takukuru na Desemba 26 alipopigiwa simu na mshtakiwa, alikwenda TAKUKURU akapewa noti 20 za Sh. 10,000 zenye thamani ya Sh 200,000 za mtego.

Baada ya kusikiliza ushahidi huo na utetezi wa mshtakiwa mahakama iliona ushahidi wa shahidi wa nne pamoja na vielelezo umekosa sifa.

Mahakama hiyo ilisema kwa kutumia kifungu namba 235 (I) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022 ilimwachia huru mshtakiwa.

"Kwa kutumia kifungu hicho Mahakama inamwachia huru mshtakiwa kwa makosa yote mawili, suala la uwindaji haramu kuna mamlaka inayoshughulikia masuala hayo, "ilisema sehemu ya hukumu hiyo.

Mshtakiwa aliachiwa huru na ilisema kwa upande ambao haukuridhika wanayo haki ya kukata rufaa.

# Polisi yawataka wazazi, walezi kulinda watoto

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi nchini limewataka wazazi na walezi kuimarisha malezi ya familia, ili kuwaepusha watoto dhidi ya ukatili na kujiingiza kwenye uhalifu na matukio mengine yasiyo na maadili.

Wito huo ulitolewa jana jijini Dodoma na Mrakibu wa Polisi wa Kamisheni ya Polisi Jamii, Dawati la Ushirikishwaji wa Jamii, Dk. Ezekiel Kyogo, baada ya kutembelea kituo cha kulelea watoto wenye mahitaji maalum cha Chigongwe Family.

Alisema sio jambo zuri kwa wazazi kutelekeza watoto wakiwamo wenye mahitaji maalum na kuwataka watimize wajibu wa malezi.

"Nitoe angalizo kwa wazazi kama umekaa ukapanga kumleta mtoto duniani basi uwe una wajibu wa kumwangalia tena kwa umakini kabisa, usifikirie utamleta mtoto halafu umwache azagae mtaani wengine wamchukue, hiki kitendo ni kibaya sana," alisema Dk. Kyogo.

Alikipongeza kituo hicho na wadau wengine kwa kujitolea kuwasimamia watoto wenye uhitaji maalum.

Alisema wanaishirikisha jamii katika hatua ya awali ya kuzuia uhalifu mapema kabla haujatokea na wanafanya hivyo kwa sababu huko ndiko matatizo yanakotokea.

"Sisi Jeshi la Polisi tunajenga uhusiano na jamii ndiyo maana tupo, peke yetu hatuwezi kuona changamoto zote zilizoko kwenye jamii, lakini ili kutatua matatizo yaliyoko huko kama watoto wa mitaani na makundi ya kihalifu hatuwezi kufanya peke yetu," alisema na kuongeza:

"Kwa ushirikiano uliopo baina ya taasisi za serikali, ustawi wa jamii, wadau, wanahabari na jamii kwa ujumla, kwa umoja wetu ndio tunaweza tukatatua changamoto za uhalifu," alisema Dk. Kyogo.

Mmoja wa watoto wanaopatiwa malezi kwenye kituo hicho, Paul Charles, alisema licha ya kutoka kwenye mazingira magumu, kwa sasa jamii imejitokeza kuwasaidia kwa kuwapatia hifadhi na mahitaji mengine ya msingi.

Mrakibu Msaidizi wa Polisi wa Dawati la Usalama Wetu Kwanza, Manase Dotto, alisema wanaendelea kuwalinda watoto, huku akiwahimiza kuendelea kutoa ushirikiano na kuripoti vitendo vyovyote vya ukatili watakavyofanyiwa au kukutana navyo.


Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationship beyond banking*

**Fully owned subsidiary of Bank of India (Public Sector Bank)**

**DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019**

**MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)**

Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on Digital Transactions)
(The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)

**A. REMITTANCE –OUTWARD**

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| **TISS Remittance** (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS | TZS 10,000 |
| | Remittance -USD | USD 10 |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

**B. REMITTANCE –INWARD**

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

**C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES**

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | -- | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | -- | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | -- | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | -- |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |

**D. Other Common Charges**

| Item | Charges TZS A/c | Charges USD A/c |
|---|---|---|
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000 Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3 Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

**E. CLEARING SERVICES**

| Item | Charge/Fees TZS A/c | Charge/Fees USD A/c |
|---|---|---|
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection -USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

**CREDIT MATTERS**

| | Charge/Fees | |
|---|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 | |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) | |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. | |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. | |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil | |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. | |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1. No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2. Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. | |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1. Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2. Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3. Interchangeability of limits.<br>4. Change in project/items of Machinery<br>5. Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6. Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7. Approvals for mergers & amalgamations.<br>8. Any other miscellaneous credit related approvals. | |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** | |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** | |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time | |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** | |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1. No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. | |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1. Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2. Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3. Interchangeability of limits.<br>4. Change in project/items of Machinery<br>5. Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6. Restructuring, Rephasement of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7. Approvals for mergers & amalgamations.<br>8. Any other miscellaneous credit related approvals.<br>1. | Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** | |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** | |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time | |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** | |

| | | |
|---|---|---|
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof** | |
| Inspection charge | TZS 30,000 per visit/inspection or at least once in quarter whichever is higher.<br>**Note:-**<br>1. Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>**Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. | Inspection charge |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** | Issuance of No objection certificate (NOC) |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. | 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount | Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** | Earmarking of Limits |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | | |
| **D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)** | | |
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge)** | USD Facility | |
| | USD 5 | |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | |
| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | | |
| Guarantee Commission | | |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate | Guarantee against 100% cash margin |
| Swift Charges | **As Applicable** | Swift Charges |
| Postages | **As Applicable** | |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** | |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil | |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** | |
| | | **1. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>**2. Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** |
| **Imports :-** | | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 30/- | |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) | |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 | |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 | |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 | |

**OTHER DISCLOSURES (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)**

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| **2.0** | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| **3.0** | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| **4.0** | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | Up to USD 10,000 | Up to TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.00% | 5.75% |
| | Over 6 months | 2.50% | 6.75% |
| | | Over USD 10,000 | Over TZS 10,000,000 |
| | 6 months | 2.50% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.00% | 7.25% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 03.01.2023 |
| 2. | Mahadhil Mansoor | Head of Finance | Signed | 03.01.2023 |
| 3. | Allen Richard | Internal Auditor | Signed | 03.01.2023 |

217205702




Askofu wa Kanisa la Good News For All Ministry, Dk. Charles Gadi, akiongoza maombi ya kumwombea Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu mikutano ya vyama vya siasa ili kuliunganisha taifa jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Mchungaji Andrew Thomas (kushoto) na Katibu wa kanisa hilo, Mchungaji Bezalel Massawe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaandaa kongamano la kodi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

SERIKALI kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, imeanzisha Kongamano la Kodi Kitaifa litakalowashirikisha wadau mbalimbali ikiwamo sekta binafsi ili kajadili namna ya kuboresha sera za kodi, kuchochea ukuaji wa uchumi, biashara na uwekezaji nchini.

Hayo yalisemwa jana na Kamishna wa Sera wa Wizara ya Fedha na Mipango, Elijah Mwandumbya, katika mkutano na wanahabari ulifanyika jijini hapo.

Mwandumbya alisema kongamano hilo litarahisisha ukusanyaji wa maoni ya wadau kwa ajili ya maboresho mbalimbali ya sera za kodi na kuongeza ushirikishwaji wa makundi hayo katika utunzi wa sheria.

"Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango, ina jukumu la kuratibu upatikanaji wa maoni ya wadau, kuchakata maoni hayo na hatimaye kuyawasilisha kwenye Kamati ya Ushauri wa Kodi, mapendekezo mbalimbali ya sera za kodi yanayotarajiwa kufanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) cha Kanuni za Bajeti za mwaka 2015," alisema.

Mwandumbya alisema katika kongamano hilo litakalokutanisha wataalamu wa uchumi, fedha na kodi nchini, mada mbalimbali zitawasilishwa na kujadiliwa ikiwa ni pamoja na hali ya uchumi duniani, fursa na athari zake kwenye sera za uchumi, uwekezaji na biashara nchini.

Aliongeza kuwa mada zingine zitakazowasilishwa na kujadiliwa ni mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali pamoja na hali ya ulipaji kodi kwa hiari na changamoto zake katika mazingira ya uchumi, biashara na uwekezaji nchini.

Kamishna Mwandumbya alibainisha kuwa kongamano hilo la kipekee pia litajadili mchango wa sekta ya fedha katika kukuza uchumi, biashara na uwekezaji wakati huu wa changamoto za uchumi duniani.

Mwandumbya alitoa rai kwa waalikwa wote wa kongamano hilo litakalofunguliwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Januari 11, katika ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC) jijini Dar es Salaam, kushiriki kikamilifu katika kutoa michango na maoni yao ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

# Mbunge aruhusu wananchi kwenda mikutano upinzani

**Na Thobias Mwanakatwe**

MBUNGE wa Songwe, Philipo Mulugo, amewataka wananchi wa jimbo hilo kwenda kusikiliza sera za vyama vya upinzani pindi vitakapoanza kufanya mikutano ya hadhara.

Amesema wafanye hivyo ili kupima wenye sera zenye mashiko kwa kuwa ndio ushindani wa kisiasa.

Mulugo alisema hayo juzi wakati akizungumza kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika kijiji cha Saza ambao aliutumia kumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa.

"Vyama vya upinzani wakianza mikutano yao nendeni mkawasikilize sera zao wanasemaje. Mle ndani watasema Mulugo aliahidi barabara ya lami, Mulungo muongo sana lakini mwakani wataanza kuona lami inapikwa mtaona pumba na mchele, ndiyo maana ya ushindani wa kisiasa," alisema.

Mulugo alisema wakati wa mkutano huo hivyo vyama vya upinzani vizungumze hoja na sio matusi, siasa za uchochezi ambazo hazina mantiki kwa nchi.

"Na nyie vijana wa CCM msilete fujo kwa vyama vya upinzani ongezeni kwa hoja msibishane kwa maneno machafu yasio na maana," alisema.

Juzi, Rais Dk. Samia alitangaza kuondoa rasmi tangazo la kuzuia mikutano ya hadhara na kuruhusu vyama vya siasa kuanza kufanya mikutano hiyo kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria na kanuni.

Rais Samia alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na viongozi mbalimbali wa vyama vya siasa nchini. Amesema ni haki ya vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara na kuwataka kutumia nafasi hiyo kufanya siasa za kistaraabu na za kujenga badala ya kubomoa nchi.

"Wajibu wenu vyama vya siasa ni kufuata sheria na kanuni zinavyosema, lakini kama waungwana na wastaarabu niwaombe sana tunatoa ruhusa ya mikutano, twendeni tukafanye siasa za kistarabu, za kupevuka na kujenga na si kubomoa."

Aidha, Rais Samia amesisitiza kuwa utaratibu wa kufanya mikutano hiyo utaendelea kwa kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi ili kupata vibali huku akisema kwa hali ilivyo sasa vibali hivyo vitaruhusiwa.

# Kigogo RAHCO ataka nyaraka halisi kujitetea

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni Hodhi ya Rasilimali za Reli (RAHCO), Benhadard Tito, anayekabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi, ameuomba upande wa Jamhuri umpatie nyaraka tisa na halisi ili kuzitumia katika utetezi wake.

Aidha, amedai kuwa kama watashindwa kumpatia nyaraka hizo zikiwamo barua mbalimbali zilizotumika katika mradi wa Njia ya Reli ya Kisasa (SGR) wenye thamani ya Sh. trilioni 15, mahakama imruhusu atumie nakala. Tito aliwasilisha ombi hilo jana kupitia Wakili wake, Jeremiah Mtobesya, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rhoda Ngimilanga, wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya mshtakiwa kujitetea.

Mtobesya alidai kuwa ni mara ya pili upande wa Jamhuri unapinga ombi lao la kuwapatia nyaraka hizi na inasikitisha sana kwa sababu mashtaka ambayo anashtakiwa nayo, yanatengenezwa na serikali.

"Mashtaka yanatengenezwa serikali yaani yanatengenezwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na kuruhusu TAKUKURU (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa) kuendesha kesi kwa niaba yake," alidai Mtobesya.

Wakili huyo alidai kuwa taarifa waliyoitoa ya nyaraka ambazo wanazitaka ama zinatoka wizarani au ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), kwa hiyo wanaweza kuwapatia nyaraka halisi.

Akijibu hoja hizo, Wakili wa Serikali Imani Mitume, alidai kuwa katika taarifa hiyo haijaonesha ni nyaraka zipi na hakuna uthibitisho wa nyaraka hizo kama kwao zipo na pia hawajawasilisha hati ya ushahidi kuonyesha zipo kwao. Baada ya Hakimu Ngimilanga kusikiliza hoja hizo, aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 9, mwaka huu kwa ajili ya uamuzi mdogo.

Katika kesi ya msingi, Tito na washtakiwa wengine walikuwa wanakabiliwa na mashtaka manane yakiwamo uhujumu uchumi, matumizi mabaya ya madaraka, kula njama na kuisababishia RAHCO hasara ya Dola za Marekani 527,540.

Ilidaiwa kuwa Februari 27, 2015 katika ofisi za RAHCO Wilaya ya Ilala, wakati akitekeleza majukumu yake, akiwa Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Tito alitumia vibaya nafasi yake kwa makusudi kwa kuiajiri Kampuni ya Rothschild (South Africa) Proprietary Limited. Ilidaiwa kuwa kampuni hiyo iliajiriwa kama mshauri wa mradi wa kuboresha ukanda wa reli ya kati Tanzania kwa njia moja bila kupata kibali cha awali cha Bodi ya Zabuni ya RAHCO, kitendo ambacho kilikuwa ukiukaji wa Sheria ya Ununuzi.

Kati ya Machi 12 na Mei 20, 2015, katika ofisi za RAHCO, Tito alidaiwa kutumia nafasi yake vibaya kwa kutia saini barua ya kuteua kampuni hiyo ya Afrika Kusini na kushindwa kuwasilisha mkataba wa huduma za ushauri kati ya kampuni hiyo na RAHCO kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.

# Kunenge kuvalia njuga migogoro ya ardhi Pwani

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amesema ili miradi inayopangwa itekelezeke ni lazima kuwekwe mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na kumaliza migogoro ya ardhi katika mkoa huo.

Kunenge aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye kikao cha bodi ya barabara kilichofanyika mjini Kibaha na kuhudhuriwa na wajumbe kutoka katika wilaya za mkoa huo wakiwamo wabunge, wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wenyeviti wa halmashauri.

Alisema kama migogoro hiyo haitaondolewa tatizo litabaki pale pale na utekelezaji wa miradi hautafanikiwa kama ilivyopangwa.

"Tumechoka migogoro ya wakulima na wafugaji hili ni jambo ambalo kama hatutaliondoa vikwazo vitaendelea kubaki pale pale, tunaenda kuanzisha ranchi ambayo wafugaji wataelekezwa mifugo ya kuwa nayo na pia watakuwa na fursa ya kulima majani hapo," alisema.

Kunenge alisema kwa kufanya hivyo, itaondoa vikwazo vya miradi inayopangwa kutekelezwa kwa wakati kwa kutokwamishwa na migogoro hiyo.

"Tumeona dhamira ya rais wetu kufungua mkoa wetu, ni wajibu wetu sisi kuangalia barabara zenye tija, tuangalie mkoa wetu kwa ujumla wake, tunajua nchi yetu ina vipaumbele vingi, lazima tupendekeze miradi yenye hoja, na inayokubalika yenye kuwagusa wananchi na tija kiuchumi," alisisitiza.

Meneja wa Wakala wa Barabara Mkoa wa Pwani (TANROADS), Mhandisi Baraka Mwambage, alisema mpango wa kazi unaoendelea kwa mwaka 2022-2023 wamepokea Sh. bilioni 47.022.

Alisema, kuna maelekezo ya serikali ya kupendezesha miji na mikoa kazi inaendelea kwa baadhi ya maeneo ikiwamo Kisarawe-Minaki, Mafia-Kilindoni, Bagamoyo Mjini, Kibaha-Chalinze-Segera, Vikindu-Mkuranga na Ikwiriri-Nyamwage.

Baraka alisema kwa upande wa kazi ya kupunguza msongamano na kuboresha barabara ya Mailimoja eneo la ATM-Pichandege, Vikindu-Kisemvule na kwamba katika miradi ya maendeleo Sh. bilioni 23 kwa ajili ya ukarabati zilitengwa na kwa sasa wamefikia asilimia 60 ya utekelezaji.

# Serikali yataka vivutio utalii Dar kutangazwa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, amewataka maofisa habari/ uhusiano na mawasiliano wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuongeza kasi ya kutangaza vivutio vya utalii ili kuifungua Dar es Salaam kiutalii.

Hatua hiyo ni kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kutangaza utalii kupitia filamu ya Royal Tour.

Masanja aliyasema hayo jana baada ya kukutana na maofisa habari katika kikao kazi kilichofanyika kwenye Ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), jijini Dar es Salaam.

Alisema ni lazima kuifungua Dar es Salaam kiutalii kwa kuwa ndio lango kuu la kupokea wageni kutoka nchi mbalimbali duniani.

"Lazima kila mwezi tuwe na tukio la kiutalii jijini Dar es Salaam na tufanye kwa kushirikiana".

Aidha, alisema ni jukumu la kila taasisi kuhakikisha inatangaza vivutio vyote bila kubagua nyingine.

"Taasisi zote za Wizara ya Maliasili na Utalii zinatunza, zinahifadhi na zinaendeleza utalii hivyo tunachotakiwa kufanya ni kumuunga mkono Rais ili kile alichokianzisha kilete matokeo chanya," alisisitiza.

Aliwataka maofisa hao kutenga bajeti za kutangaza vivutio vya utalii vya maeneo yao ya kazi kupitia vipeperushi na kuviweka katika maeneo yanayotembelewa na wageni.

"Vipeperushi vinatakiwa vionekane katika maeneo yote ambayo watalii wanafika hapa jijini Dar es Salaam kama hoteli, viwanja vya ndege na magari yanayobeba abiria "madereva taxi" wanaopokea watalii ili kuvutia watalii wengi zaidi. Vipeperushi hivyo viwe na vivutio vyote vya utalii vya maeneo yote ya taasisi za wizara ambazo ni TAWA, TANAPA, TFS na Makumbusho ya Taifa.

Kadhalika amezitaka taasisi za wizara hiyo kuitumia fursa ya meli inayoleta watalii nchini kutangaza ujio wake kwa kualika waongoza watalii kushiriki kuwapokea na kuwatembeza katika vivutio mbalimbali vilivyoko kwenye jiji hilo.

Aliwataka maofisa hao kuisemea wizara kwa nguvu moja ili kufikia malengo ya kuongeza idadi ya watalii nchini.



Kijana akimbebea mteja tenga la nyanya katika Soko la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. Gharama ya kulitoa ndani soko hadi nje ni Sh. 1,000. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wahandisi waagizwa kufikishia maji wananchi wanaoishi kwenye chanzo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amewaagiza wahandisi wa maji Wilaya na Mkoa wa Morogoro, kuhakikisha wananchi wa Kijiji cha Bagilo, Kata ya Tegetero wananufaika na mradi.

Mradi wa maji wenye thamani ya Sh. bilioni 23 unatarajiwa kuzifikia kata saba na vijiji 19 kabla hayajaenda kwenye maeneo mengine.

Waziri Aweso alisema hayo jana baada ya kutembelea mradi wa Morong'anya alipopata malalamiko kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, Hamisi Taletale, kuwa pamoja na kujengwa kwa mradi huo mkubwa eneo la Tegetero, wananchi wake hawatanufaika.

Aweso aliagiza, kabla maji hayajaenda kwenye maeneo mengine lazima yafike kwa wananchi wa eneo husika ili nao wanufaike na waridi wanukie na Tegetero wametoa chanzo cha maji wanapaswa kunufaika nayo. Aliwataka wahandisi wazingatie wananchi wanaotoa chanzo cha maji na wawe na dizaini za kuzingatia.

Pia, aliwataka kufanya tathmini ya uhakika ili wananchi wapate maji na kuwasaidia wengi.

"Kubwa nawaomba ndugu zangu mradi huu ni mkubwa sana, umetumia pesa nyingi sana, naomba muulinde na muutunze uwe endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo ili waje kuona matunda yaliyofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

"Matokeo tuliyoyapata na adha zake yawe mafunzo sababu tumeshuhudia maeneo mengi yanakauka sababu ya athari za mazingira kutokana na moto kwa sababu mazingira yana kawaida ya kulinda ukiyatunza na usipoyatunza yatakuadhibu," alisema.

Naye Mbunge wa Jimbo hilo, Hamis Taletale, alitoa hoja ya kijiji hicho kukosa majisafi na salama licha ya kuwapo kwa chanzo katika eneo hilo ambayo yanapelekwa kwenye maeneo mengine.

Kaimu Mkurugenzi Bonde la Maji Wami Ruvu, Martin Kasambala, alisema jumla ya miti 500 imepandwa katika eneo la kuzunguka chanzo hicho, kati ya miti 17,000 inayotarajiwa kupandwa ili kufikia lengo la Rais Samia la kupanda miti milioni mbili katika maeneo mbalimbali.

# UWT yampongeza Samia kuruhusu mikutano kisiasa

**Na Hamida Kamchalla,**

TANGA

UMOJA wa Wanawake wa Tanzania (UWT), umeungana na wito wa Rais Samia Suluhu Hassan, wanasiasa kutumia ruksa ya mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa kwa kufanya siasa za kistaarabu, kupevuka na zenye kujenga na kuacha matusi na kashfa.

Akiongea na waandishi wa habari katika ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Tanga, Mwenyekiti wa UWT Taifa, Mary Chatanda, alisema Rais ni mpenda haki na ndio maana maamuzi matatu aliyoyachukua juzi kwa vyama vya siasa yataendelea kukuza amani ya nchi.

"Siasa ni mwelekeo mpya wa nchi yetu katika kuihami demokrasia yetu, sisi tunasema hakika mama Samia ni neema kutoka kwa Mungu, kilio chetu UWT siku zote ni kuona nchi yetu ikiwa na utulivu, amani na yenye haki baina ya wananchi wake na serikali yao," alisema Chatanda.

"Rais Samia amechonga palio, wajibu wetu sote wanasiasa na wananchi wote ni kulifuata kwa unyenyekevu, tusimkatishe tamaa, vijana, kinamama hata wazee, sote tuwe wamoja tujenge nchi yetu, UWT inawasihi viongozi wanawake ndani ya vyama vya siasa, kuonyesha mfano katika hili kwa kutanguliza ustaarabu, kuheshimiana, utu wakati wote wa mikutano hiyo ya hadhara na kamwe pasitokee viongozi wa vyama vya siasa kubeza na kutweza utu wa mwanamke au wa mtu mwingine."

Aidha, alisema UWT inawahimiza viongozi wanawake wa vyama mbalimbali kuandaa mikutano mingi ya hadhara ili kupokea kero mbalimbali zinazowagusa wanawake kwa kuwa wanakabiliwa na kero zinazofanana bila kujali itikadi zao.

Alisema katika mikutano hiyo wanaoendeleza hatua mahususi za kuchukua kwa serikali ili kumkomboa mwanamke kiuchumi, kijamii na kisiasa, pia wamefurahishwa na uamuzi wa serikali kuridhia mapendekezo ya kikosi kazi ya kufanya marekebisho ya sheria kadhaa ndani ya nchi kwa nia ya kuimarisha demokrasia zaidi ambayo yatahusisha wananchi.

"Tuna imani marekebisho hayo pia yatazingatia masuala ya usawa wa kijinsia katika kuongeza uwakilishi wa wanawake kwenye siasa na uongozi kuanzia kwenye vyama vya siasa kama ambavyo tunashuhudia namna Rais wetu Dk. Samia Suluhu Hassan anavyojitahidi kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye uongozi ndani ya serikali yake na chama anachoongoza cha CCM," alisema.

Alisema kwa niaba ya wanawake wa Tanzania wanaunga mkono uamuzi wa kukwamua mchakato wa marekebisho ya Katiba na wanahimiza amani na utulivu wakati wote wa kusubiri serikali kukamilisha taratibu zote za kuanza mchakato huo.

"Tunaendelea kuwaomba Watanzania kuendelea kumwamini Mheshimiwa Rais na kumuunga mkono kwani ana dhamira njema ya kujenga taifa linaloongea lugha moja ambalo kila mmoja anashiriki."

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), Mkoa wa Tanga, Mohamed Salim maarufu Ratco, alitoa wito kwa viongozi wa vyama vya siasa kuwa na mipaka katika kutandaza sera zao wanapokuwa kwenye mikutano yao.




Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake CCM Taifa, Mary Chatanda, akisalimiana na wajumbe wa UWT Mkoa wa Tanga jana kabla ya kuongea na waandishi wa habari kuhusu kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuruhusu vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# ...Wananchi walivyopokea uamuzi kuruhusu mikutano

**Na Elizabeth Zaya**

WANANCHI mbalimbali wametoa maoni mtandaoni kuhusu uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kuruhusu mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa nchini na kuahidi kuanza kwa mchakato wa Katiba Mpya.

Wananchi hao waliandika kwenye ukurasa wa Ikulu wa 'Youtube' wakati Rais Samia akihutubia jana, wengi wakipongeza hatua hizo kwamba zinakwenda kulijenga na kuliimarisha taifa kidemokrasia.

Thobias Kichere aliandika; "Uamuzi uliofanywa na Rais Samia ni mwema kwa kuwa mema ya leo ndio mstakabali mwema wa kesho wa taifa, huku akiongeza kwamba Katiba mpya ni msingi wa yote."

Kalumbu GuIdeon, alipongeza hatua hiyo na kumtaka Rais kusonga mbele.

Sempa Prudence alisema; "Rais Samia ana nia ya dhati ya kuipeleka Tanzania katika demokrasia ya kweli, hiyo ni hatua muhimu katika siasa ya Tanzania akiamini hotuba yake ni umoja, amani na mshikamano." Matayo Zebedayo alisema: "Huu ni mwanzo mzuri wa kujenga Tanzania mpya chini ya Rais Samia Suluhu." Naye Wilson Baraka alisema anawaamini viongozi waliowakilisha katika mchakato wa kufanikisha jambo hilo na akisisitiza kwamba Katiba Mpya na mikutano ya hadhara ni sasa.

Mwingine aliyejiita Tanzanite, alisema haamini kama kweli kutakuwa na mikutano ya hadhara wala kupatikana kwa Katiba mpya, wakati Ferdiana Brastus akisema kwamba ili kuwe na uwiano sawa, lazima Ofisi Msajili wa Vyama vya Siasa, ibadili namna sahihi ya uendeshaji wa chombo hicho akisema ofisi hiyo imekuwa chachu ya kuvuruga vyama vya upinzani.

Rubibi Kassim, alimpongeza Rais Samia kwa kuruhusu mikutano ya hadhara huku Rabie Mbise, akisema Rais amefanya jambo la maana kuruhusu mikutano hiyo ya hadhara na kusisitiza Katiba mpya ni muhimu na Tume Huru ya Uchaguzi.

Ladislaus Tumbu alisema: "Kama yote yaliyosemwa na Rais Samia yatafuatwa anaamini nchi itaendelea, ni wajibu wa watendaji wa serikali kutekeleza yatakayoonyeshwa na wakosoaji, uchambuzi yakinifu ukifanyika maendeleo ni ya Watanzania wote."

Ryner Linuma, alisema jambo la msingi analoona ni Katiba Mpya na kuomba ipatikane kabla ya mwaka 2024 akisisitiza inayohitajika ni Katiba mpya na si marekebisho, huku Patrick Kalimoja akiandika haki ya mikutano ipo kikatiba na sio huruma ya rais.

Edson Massawe alisema; "Katiba ni mchakato na endapo Rais atakuwa msikivu kila kitu kitakwenda vizuri."

Seleman Emanuel alisema anaona ni suala la muda, mikutano ya hadhara itatoa uharaka wa Katiba mpya na Tume Huru ya Uchaguzi.

Dioniz Kipanya, alisema Katiba wanayoitaka ni yenye maoni ya wananchi, wakati Laurent Balama, alisema "Hakuna Katiba hapo mkazunguke kwenye majukwaa tu."

Ferdiana Brastus, alisema Katiba izingatie matakwa ya wananchi sio ya watawala na kuna mambo mengi ya kurekebisha ili kuwawajibisha watawala wakati Mamuu Lolo akisema-rasimu ya Katiba ya Warioba ndiyo kila kitu.

Catherine Malila alimpongeza Rais Samia na atabaki kuwa alama ya upatanisho wa nchi, huku akiamini kwamba mwanamke ni nguzo ya amani kwa familia na taifa kwa ujumla.

# Wakataa viongozi wao mbele ya mbunge

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WANANCHI wa Kijiji cha Manga, Manispaa ya Singida wamewakataa viongozi wa kijiji hicho akiwamo Mwenyekiti na Mtendaji mbele ya Mbunge wa Singida Mjini, Ramadhani Sima na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa Singida, Jeshi Lupembe, wakiwatuhumu ufujaji wa fedha za kijiji.

Wananchi hao walimtaka mkurugenzi na mbunge waondoke nao wakati wa mkutano wa hadhara ulioitishwa na mbunge huyo.

Mbunge aliitisha mkutano huo juzi baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa Mtendaji wa Kijiji, Reuben Njou, amewachangisha maelfu ya fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyoo vya shule ya sekondari mpya ya kijiji hicho kinyume na utaratibu.

Mbunge Sima aliamuru fedha hizo warudishiwe wananchi 18 waliotoa Sh. 30,000 kila mmoja kati ya 124 waliotakiwa kuzitoa katika kijiji hicho.

Sima alichukua hatua ya kutoa fedha zake kwa ajili ya kusaidia kumalizia ujenzi wa vyoo hivyo vya wanafunzi vyenye matundu manane katika shule mpya ya sekondari ya Manga. Katika mkutano huo wananchi walieleza ubadhirifu wa fedha za mradi wa ujenzi wa daraja na viongozi wa kijiji hicho waliingia mkataba na mkandarasi wa kubeba mawe kutoka eneo la kijiji tripu 33 na wao kudai ni tripu 10.

Madai mengine yaliyoibuliwa ni ubadhirifu katika ukusanyaji wa mapato mnada wa kijiji hicho na kumuomba Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Lupembe kuwaweka watu wengine ili kubaini makusanyo yanayokusanywa ambayo yatakuwa tofauti na yale yanayokusanywa.

Kero nyingine iliyoibuliwa dhidi ya Ofisa Mtendaji huyo ni kujifanya Mungu mtu kutowasikiliza wananchi na katika mikutano ajenda zote kuziendesha yeye bila ya kuwahusisha wajumbe wa kijiji.

"Mkurugenzi huyu mtendaji ni mwajiriwa wa ofisi yako unaweza kumpa kazi hata ya kupanga mafaili katika ofisi yako tunaomba uondoke naye sisi hatumtaki hapa kijijini," alisema Samweli Kitiku mkazi wa kijiji cha Manga."

Kero nyingine walidai ni utoaji ajira za muda mfupi kama wakati wa chanjo na sensa ya watu na makazi kuwa vijana wengi waliopata fursa hiyo walikuwa ni ndugu na jamaa wa watumishi wa serikali ya kijiji ambao vijana wa maeneo hao hawakupata fursa hiyo.

Baada ya kupokelewa kwa kero hizo na nyingine Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida alitangaza kumwondoa mtendaji huyo katika kata hiyo huku Mbunge Sima akitoa majibu ya kero hizo kwa ufasaha.

# Manyara yadorora uandikishaji watoto

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara, umeandikisha kwa asilimia 63 pekee, wanafunzi wa darasa la awali 29,072 hadi kufikia Desemba 31, mwaka jana, ambayo ilikuwa tarehe ya ukomo iliyowekwa na serikali.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa jana na Ofisa Elimu wa Mkoa huo, Halfan Masukira, kati ya walioandikishwa wavulana ni 15,151 na wasichana ni 13,921. Alisema matokeo yalikuwa ni kuandikisha wanafunzi wa darasa la awali 46,494.

"Tuliweka matokeo ya kuandikisha wanafunzi wa darasa la awali kwa wavulana wawe 23,726 na wasichana wawe 22,768 lakini hatukufika huko kutokana na sababu mbalimbali, ambazo nyingine ziko nje ya uwezo wetu," alisema.

Kuhusu uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza, Masukira alisema mkoa huo umeandikisha wanafunzi 57,176 wakiwamo wavulana ni 29,227 na wasichana 27,949.

Wanafunzi wote hao wanatarajia kuanza masomo yao kati ya Januari 7 na 9, mwaka huu, kwa mujibu wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978, mzazi au mlezi anayeshindwa kumwandikisha mtoto wake shule, anaweza kuchukuliwa hatua, ikiwamo kifungo au kulipa faini itakayotajwa na mahakama.

Vilevile, ofisa elimu huyo, alieleza kuwa elimu ya awali, inamwandaa mwanafunzi kwenda elimu ya msingi.

# MAREMA yajivunia kukoma utoroshaji madini

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

MWENYEKITI wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Justin Nyari, amesema kutokana na kutambua thamani ya madini, wachimbaji wa madini ya tanzanite, kwa sasa hawajihusishi na vitendo vya utoroshaji wa madini hayo.

Akizungumza jana katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani hapo, alisema tangu serikali ilipowabana wachimbaji kutorosha madini hayo, hali sasa ni shwari na taratibu zinafuatwa kama kawaida.

"Kwa sasa tunafurahi sana kuona wachimbaji wa madini ya tanzanite wanatambua umuhimu wa rasilimali hii kwa taifa na hawajihusishi na vitendo vya utoroshaji wa madini," alisema Nyari.

Alisema wachimbaji madini hayo wakishapata uzalishaji wanakwenda ndani ya ukuta na kufanyiwa tathmini kisha utaratibu mwingine wa kuuza unafuatwa na siyo vinginevyo.

Pia alisema serikali imejenga ukuta unaozunguka machimbo ya migodi ya madini ya tanzanite, hivyo ni vigumu kwa wachimbaji kutoroka na madini.

"Pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Madini, pia kuna ulinzi mkubwa wa vyombo vya ulinzi na usalama ndani ya ukuta huo na upekuzi huwa unafanyika, hivyo si rahisi wachimbaji kutorosha madini hayo," alisema Nyari.

Kauli ya Nyari ilipata wafuasi, baada ya mchimbaji mdogo wa vito hivyo, Sokota Mbuya, kueleza baadhi ya watu wamekuwa wakipotosha kuwa kuna watu wanaotorosha madini hayo ilihali si kweli.

"Mchimbaji hawezi kutorosha madini kwenye ukuta kwa kuwa kuna ulinzi wa wanajeshi kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa (TISS), askari polisi, Uhamiaji na kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)," alisema Sokota.



Waziri wa Madini, Dk. Dotto Biteko, akizungumza na wachimbaji wadogo katika mgodi wa dhahabu wa Isonda wilayani Nyang'hwale, Geita juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbunge aahidi usajili kituo cha malezi ya yatima

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MBUNGE wa Hai (CCM) mkoani Kilimanjaro, Saashisha Mafuwe, ameahidi kumaliza urasimu unaofanywa na baadhi ya watumishi wa umma kukipiga danadana usajili wa kituo cha malezi ya yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Rolini.

Kituo hicho kilichoko eneo la Kijiji cha Kwa Sadala, kimekosa usajili wa kutambuliwa na serikali kwa miaka 24 sasa, licha ya kujikita kutoa huduma isiyo na faida.

Mafuwe aliahidi kukisaidia kituo hicho kupata usajili wake, alipokwenda kukitembelea na kugawa misaada ya kibinadamu kwa watoto hao jana.


"Nitahakikisha mwaka huu, mnapata usajili ili mwendelee kutoa huduma kwa mujibu wa sheria. Hizi danadana niachieni, maana huduma mnayoitoa hapa ni huduma ya kuwasaidia watoto wenu wa Kitanzania wakue katika maadili na kupata elimu na mnamsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kupata watu wema," alisema. Mbunge huyo alionyesha kutoridhishwa na urasimu huo, baada ya kusomewa taarifa kwamba kituo hicho kilichoanzishwa 1999 hakijapata usajili, licha ya kuomba kupatiwa usajili mara kwa mara.

Alikwenda kituoni hapo kuwapa misaada mbalimbali, kama mchele, sukari, sabuni na nguo kwa ajili ya sherehe za mwaka mpya.

Awali katika risala yake, Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Rosmin Njau, alisema tatizo kubwa walilonalo kwa sasa, ni kituo hicho kutosajiliwa ili waweze kufanya huduma kwa upana zaidi.

"Ni kweli tatizo hili la usajili ni la muda mrefu, tumeomba bila mafanikio. Wadau wanashindwa kutusaidia, kwa sababu hatuna usajili. Ikafika mahali ikabidi kituo tukiendeshe kama familia, kwa kulima mashamba ya mahindi na mpunga, kwa ajili ya chakula na kupata ada na matumizi mengine," alisema Njau.

Alisema katika kituo hicho kwa sasa kina watoto 34, ambapo kati yao wavulana ni 20 na wasichana 14. Diwani wa Masama Kusini, Cedrick Pangani, alimpongeza mbunge huyo kwa kuona umuhimu wa kuleta vyakula na nguo kwenye kituo hicho katika kata yake, huku akiwaomba wadau wengine kuiga mfano huo wa Mafuwe.





# Wapata ahueni kusafiri masafa

**Mwandishi Wetu,** SAME

WAGONJWA waliokuwa wakisafirishwa kwa zaidi ya saa moja kutoka Same hadi Moshi Mjini kufuata huduma za dharura, sasa wamepata ahueni baada ya serikali kukamilisha ujenzi wa jengo la huduma za wagonjwa wa dharura katika Hospitali ya Wilaya ya Same.

Kabla ya kukamilika kwa jengo hilo lenye uwezo wa kuchukua wagonjwa wa dharura 80 kwa wakati mmoja, wakazi wa Same walikuwa wakitegemea huduma hiyo Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Mawenzi na Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC).

Akizungumzia mradi huo jana, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Same, Dk. Alex Philemon, alisema jengo hilo limegharimu Sh. milioni 300 ambazo zimetolewa na serikali.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya hiyo, Dk. Ibrahimu Sembua, alisema awali huduma hiyo haikuwa inatolewa kwa mpangilio mzuri lakini kwa sasa huduma zitakuwa za uhakika.

"Same iko kwenye barabara kuu ya Dar/Moshi/Arusha na mara nyingi ajali zikitokea kwenye barabara hiyo. Majeruhi hupelekwa hospitali ya wilaya na kwa kuwa hapakuwa na jengo la huduma za wagonjwa wa dharura, majeruhi walikuwa wanapelekwa Mawenzi au KCMC," alisema.

Kitengo cha wagonjwa wa dharura, kazi yake ni kuona wagonjwa wote wa dharura na kuwaimarisha kabla ya kwenda wodini au chumba cha upasuaji au wodi ya wagonjwa mahututi.

Pia kazi yake ni kufanya huduma za uchunguzi za dharura, kutoa huduma ya dharura kuokoa maisha ya wagonjwa, mafunzo ya utoaji huduma za dharura kwa wafanyakazi wa idara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Anastazia Tutuba, alisema kwa sababu ya umbali, huduma hiyo ilikuwa inahatarisha maisha yao, hivyo wanaishukuru serikali kwa kuwa sasa huduma hiyo itapatikana hospitalini hapo.

# Kortini madai kukutwa na nyara za serikali

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

WATU sita wakazi wa Wilaya ya Handeni, mkoani Tanga, wameburuzwa kortini kwa madai ya kukutwa na nyama ya tandala na digidigi, ambazo ni nyara za serikali.

Washtakiwa hao, wakiwamo watatu wa familia moja, walifikishwa jana katika Mahakama ya Wilaya hiyo, wakikabiliwa na shtaka kumiliki nyara hizo zenye thamani ya Sh. milioni 110.

Akisoma hati ya mashtaka, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Kasimili Msofe, alidai kuwa washtakiwa watatu, ambao ni Omari Kigogo (baba), Mahadia Nyemo (mke) na Nuru Kigogo (mtoto) mwenye umri wa miaka 17, wanashtakiwa kwa kukutwa na nyama ya tandala na digidigi, zenye thamani ya Sh. milioni sita.

Kesi hiyo inasikilizwa na Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Handeni, Veronica Siyao.

Mwendesha mashtaka Msofe alidai kuwa washtakiwa hao walikutwa na nyara hizo bila kuwa na kibali cha mamlaka husika ambayo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA). Baada ya maelezo ya kosa kusomwa mahakamani hapo, Hakimu Siyao aliwahoji washtakiwa kama wanakubali kosa wanalokabiliwa nalo na kila mshtakiwa alikana kisha hakimu akasema haki ya dhamana kwa washtakiwa wote iko wazi.

Washtakiwa wote sita, walikamilisha taratibu za kupata dhamana na Hakimu Siyao aliwapa dhamana hadi hapo kesi yao itakapotajwa Februari 14, mwaka huu.

Wakati huo huo, watu wengine watatu wakazi wa wilaya ya Kilindi, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Handeni, wakidaiwa kukutwa na meno manne ya tembo.

Kwa mujibu wa Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Sefi Makono, wanaokabiliwa na kosa hilo ni Ramadhan Yahya, mkazi wa Kibirashi, Kidabo Mganga, mkazi wa Mgera (wote wa wilaya ya Kilindi) na Zuberi Shaban, mkazi wa Kwaluala, wilaya ya Handeni.

Kesi hiyo, pia inasikilizwa na Hakimu Mkazi wa Wilaya ya Handeni, Veronica Siyao.

Washtakiwa hao wanadaiwa kukamatwa katika matukio tofauti, wakisafirisha nyara hizo za serikali.

Katika maelezo ya kosa, meno hayo ya tembo yametajwa kuwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 104.

Kumiliki nyara za serikali ni kinyume cha kifungu cha 86 (1), 2(b) cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori Na. 5 ya Mwaka 2009, kikisomwa pamoja na Aya ya 14 ya Jedwali la Kwanza na Kifungu cha 57 (1) na 60 (2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi, Sura ya 200 iliyofanyiwa Marejeo Mwaka 2002.



Muuza kuku akiwatoa kwenye tenga jana kwa ajili ya kuwauzia wateja Mtaa wa Majengo Shimoni wilayani Muheza, mkoani Tanga. Mmoja aliuza kwa Sh. 6,000. **PICHA: STEVEN WILLIAM, MUHEZA**

# Serikali yaanza kufuatilia vitendo ukatili wa kijinsia

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adofu Mkenda, amesema wizara yake imeanza kufanyia kazi vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto vinavyoendelea kuchipua kwa kasi katika idara, taasisi na sekta ya elimu inayosimamia kisera.

Prof. Mkenda, ambaye ni Mbunge wa Rombo (CCM) mkoani Kilimanjaro, alieleza mpango huo wa wizara jana alipokutana na Jumuiya za Kiislamu.

"Hivi sasa katika jamii yetu kuna visa vingi vya unyanyasaji wa kijinsia, hivyo Wizara ya Elimu (Sayansi na Teknolojia), kwa kushirikiana na viongozi wa dini, wazazi na walezi, wana jukumu la kuhakikisha tunazuia visa hivyo.

"Tumekuwa tukisikia visa vingi vya unyanyasaji wa kijinsia. Sijui ni kwa sababu sasa hivi ni rahisi sana kupata taarifa au ni dunia imeharibika zaidi. Kwa vyovyote vile tunajukumu la kuhakikisha kwamba tunazuia vitendo hivi," alisema.

Waziri huyo alisema kila mmoja analo jukumu la kuhakikisha anakuza maadili ya watoto na kwamba kazi kubwa kwa sasa iko Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kuzuia kinachoendelea katika maeneo mbalimbali yanayotoa huduma za elimu. Kutokana na mkakati huo, Waziri Mkenda alisema tayari wizara yake imeshakutana na mawaziri wengine wa kisekta jijini Dodoma na kufanya uamuzi wa kuanza utekelezaji wake ili kuwalinda watoto.

Waziri Mkenda aliungwa mkono na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu, aliyeshauri wabunge kuisukuma serikali kupeleka bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria inayotoa fursa kwa washtakiwa wanaofanya ukatili kuachiwa kwa dhamana.

Sheria inayopigiwa kelele ifumuliwe ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kwa kuwa inatoa nafasi kwa washtakiwa wa makosa ya ukatili wa kijinsia kutamba mitaani, licha ya kufanya makosa yanayovunja haki za binadamu.

Alisema kumekuwapo na mmomonyoko mkubwa wa maadili, ambapo watu wamegeuka kuwa wanyama na kufanya mambo kama hawana akili.

ALHAMISI JANUARI 5, 2023
AFYA NA MAZINGIRA




Ukurasa 16

**Angalizo; Ulivyo umakini, njia panda katika uwepo wa aloevera nchini**



Ukurasa 20

**Mtu mrefu anayekua kila siku,mbioni kumpiku mshindi Guiness**

# Kutojua kunawa mikono kwa ufasaha kunavyoeneza magonjwa ya mlipuko

**Na Mackriner Siyovelwa**

WAKATI dunia ikikumbwa na magonjwa ya mlipuko yanayotokea na kuleta madhara makubwa kwa binadamu kama Ebola na Covid 19, unawaji wa mikono na usafi kunaelezwa kuwa njia muhimu ya kukabiliana na magonjwa hayo.

Shirika la Umoja wa Mataifa Linaloshughulikia Watoto, (UNICEF) kupitia ripoti yake, linaeleza inakadiriwa kuwa kati ya kila watu watano, watatu pekee ndio wana vifaa vya kunawa mikono, huku asilimia 43 ya watu duniani hawana vifaa vya kutumia vyenye maji safi na sabuni majumbani mwao.

**UMUHIMU UKOJE?**

Tafiti mbalimbali zilizofanyika, zinaeleza kuwa mikono ni kiungo kikubwa katika kueneza magonjwa ya mlipuko yanayotokea katika maeneo mengi duniani, hususani Afrika na mfano wa magonjwa hayo ni Covid 19 na Ebola, ambayo imeshambulia jamii.

Kwa mujibu wa Said Chibwana, mtaalamu wa Kinga na Udhibiti wa Maambukizi, kutoka asasi ya Jamii Bora Health, kutumia mikono, kunamuwezeha mtu kupata kirahisi ugonjwa huo kwa namna ya kujishika machoni, puani, mdomoni au kugusa maeneo ambayo wadudu wanaweza kuingia mwilini kirahisi.

"Pia ni rahisi kuambukiza wengine hasa wale ambao atakuwa karibu nao kwa muda huo mfano ofisini, nyumbani au hata mtaani kwa kuwagusa ikiwa wapo katika mazungumzo, ya kupeana salamu" anafafanua Chibwana

**NINI KINAKWAMISHA?**

Kwa muktadha uliopo inaelezwa kuwa watu wanashindwa kunawa ikiwa yapo mambo mengi na sababu mbalimbali ambazo husababisha watu kutonawa mikono kabisa au kutonawa kwa usahihi

Chibwana anasema, watu wengi hawafahamu namna sahihi ya kunawa mikono, hivyo kufanya waendelee kusambaza vijidudu kutokana na kwamba wanabaki navyo.

"Wengi hawajui kunawa mikono kwa usahihi na matokeo yake badala ya kuondoa uchafu na vijidudu huendelea kubaki navyo na kuvisambaza zaidi," anafafanua na kuongeza:

"Kuna swala la mazoea na utamaduni wa unawaji wa mikono ambalo nalo kwa Tanzania ni tatizo kubwa, kwani inaelezwa takribani asilimia 50 ya watu hawana utamaduni huo."



Mtu akinawa mikono. **PICHA: MAKTABA.**

**JAMII INASEMAJE?**

Katika dodosa za Nipashe mtaani kuzungumza na baadhi ya wakazi wa mkoani Dar es Salaam, kufahamu uelewa wa jamii katika suala zima la kujikinga na magonjwa ya mlipuko kwa kunawa mikono ilivyo.

Mkazi wa Tandale, Maria Mussa, anasema "unawaji mikono bado ni kitendawili na kwa mazoea ambayo tumekuwa nayo mtu hunawa mikono pale anapokwenda kula chakula au anapokuwa na uchafu unaoonekana.

"Mwingine akiona mikono haina uchafu unaoonekana kwa macho anaweza kula chakula bila kunawa. Jamii yetu tangu makuzi ya utoto wetu, hatukufunzwa kunawa mikono na ni jambo ambalo unapaswa kulizingatia mara kwa mara."

**NINI KIFANYIKE?**

Kukirejewa Mtalamu wa Kinga na Udhibiti wa Maambukizi, Chibwana anashauri jamii kufanya kampeni nyingi zitakazojengea mazoea na tabia ya kunawa mikono kila mara, kwa kufanya jambo hilo kuwa sehemu ya maisha yao ya kila siku.

Mtaalamu wa afya, Dk. Joseph Hokororo, anayetumika katika nafasi ya Mratibu wa Kinga na Udhibiti wa Maambukizi Wizara ya Afya, anasema tahadhari ya kunawa mikono iliyochukuliwa wakati wa uviko 19, inapaswa kuendelezwa wakati wote kwa kuwa bado magonjwa ya mlipuko yanaendelea kutokea na mengi yanahusisha usafi, pia kunawa mikono.

Kupitia kuwapo kwa hali hiyo, Maria alishauri serikali kuanzisha mitaala au mfumo ambao utawajenga watoto kuanzia elimu ya awali, kuona unawaji mikono ni jambo la muhimu na la kuzingatiwa.

"Mtoto anavyokuwa, anakuwa na tabia hiyo na kizazi kinachokuja kitafanya hivyo kuwa kama tabia muhimu na sio jambo ambalo unaweza kufanya, mpaka kuwepo mlipuko wa magonjwa au sekta ya afya kutumia nguvu kubwa kuwahamasisha watu kunawa mikono," anatamka mdau wa afya kwa jina moja la Maria.

Anahitimisha kwa kauli: "Hilo pia linaweza kubadili tabia ya jamii kwa kutumia watoto sababu wanaweza kuhamisha tabia hiyo kutoka shuleni na kuipeleka nyumbani na hivyo kupelekea jamii nzima kubadilika taratibu."

AFYA

# Teknolojia ya IVF inavyosimama nchini na kutoa majibu kwa wagumba wahitaji

**Na Christina Mwakangale**

KUKUA teknolojia kunatajwa kuirahisishia jamii huduma ya afya, jambo ambalo awali majibu yake yalibeba sura ya kitendawili, hususan kwa nchi zilizopo Kusini mwa Jangwa la Sahara (SSA).

Kwenye toleo la Alhamisi wiki iliyopita, safu hii ilizungumzia tatizo la ugumba, likiwa na mzizi mkuu wa kibaiolojia, sasa limepatiwa majibu ya teknolojia iitwayo 'IVF' kuitatua.

Teknolojia ya IVF iligundulika zaidi ya miaka 40 nchini Uingereza, sasa matumizi yake yanashika kasi Afrika na hadi mwaka jana watoto waliozaliwa kwa njia hiyo duniani wako milioni nane, ikitoa suluhisho kwa wa ama waliokwama au kuchelewa kushika ujauzito.

Mtaalamu bingwa wa 'kutengeneza watoto' kiteknolojia (Embriologist) kutoka Hospitali ya Kairuki Green ya jijini Dar es Salaam, George Tryphone, ana ushuhuda wa walioshindwa kupata ujauzito zaidi ya miaka 20 hadi 30, wamewezeshwa.

"Walengwa ni familia ambazo zipo katika makundi mawili, walio katika umri wa kuzaa iwe kwa wanawake au wanaume, kundi la pili ni wanaohitaji kutafuta mtoto waliopo kwenye mahusiano ama ndoa," anasema bingwa huyo.

Anafafanua mchakato wake na aina husika, unategemea iwapo walengwa wanataka kufuata taratibu za upandikizaji za IVF, kwa kuwa huchunguzwa kutambua tatizo, kisha kunafanyika tiba ya awali kabla ya kuumbwa mtoto na anasema, maandalizi hutegemea; njia ndefu ni muda wa mwezi mmoja na wiki kadhaa na njia fupi, itakuwa wastani mwezi mmoja pekee.

"Kwa hapa nchini Julai mwaka huu (2022), tumeweza kuwafanyia huduma kinamama 10 na kati yao, saba walifanikiwa, lakini wengine watatu hawakufanikiwa kutokana na changamoto mbalimbali, kwa sababu kila mtu ana tatizo lake na hilo haliwezi kuendana na la mtu mwingine, tunajipanga, kuwarudia tena," anaeleza mtaalamu huyo.

**HUDUMA ILIVYOANZA**

Tryphone anasema, msukumo kwao kuanzisha IVF ni wa muda mrefu, kwa muasisi wa taasisi, Marehemu Dk. Hubert Kairuki, mwaka 1982 alipokuwa nchini Canada na ikaendelezwa baadaye na Dk. Clementina Kairuki, bingwa wa magonjwa ya kinamama, sasa akizama zaidi katika changamoto za uzazi na anatafiti kinamama wengi matatizo yao ya uzazi.

"Tatizo linapofika kwa wataalamu na mnakuta hamuwezi kulitatua, inabidi mtu atoke aende




Wataalamu wa afya, katika kituo kinachotoa huduma ya uzazi kwa kwa njia ya IVF, jijini Dar es Salaam. **PICHA ZOTE: MPIGA PICHA WETU.**

nje na gharama yake huwa ni kati ya Sh. milioni 30 na zaidi hata akienda huko inakuwa haina uhakika. Unakuta anaenda hajapata na anatamani anarudi tena akajaribu na unakuta wengine ni watumishi wa umma, kachukua mkopo wake sasa inakuwa gharama juu ya gharama.

"Kutokana na tatizo hilo, mwaka 2016 hospitali (Kairuki) ikaamua kuleta huduma hiyo nchini na kuanza ujenzi wa kituo hicho maalum kwa IVF, huduma ikaanza rasmi mwaka huu, Februari, kuandaa hao 10 na Julai, wakatoa toleo la kwanza, Oktoba mwaka huu tutatoa batch nyingine.

"Kwenye huduma hiyo iliyohusisha kinamama 10, kati yao saba wakafanikiwa kupata ujauzito na mmoja mwenye umri wa miaka zaidi ya 50 amepata huduma mjamzito, Mtanzania. Tunapokea wanaohitaji huduma kutoka hata nje ya nchi, mfano, Comoro, DRC (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) na wote hawajawahi kupata watoto kwa vipindi tofauti, mwingine miaka 10 na zaidi,' anaeleza Tryphone an anataja wataalamu wenzake wamenolewa kwa miaka mitatu kwenye stadi za IVF katika nchi za; India, Sctotland, Hispania na Uingereza.

**MAHITAJI YA HUDUMA**

Bingwa huyo anasema hadi sasa mahitaji, yanaongezeka kila siku kutoka kwa wanaofika kwao hospitalini, akisema ni huduma inayohitaji siku mbili za mazungumzo kati ya wenza, tabibu bingwa na mwanasaikolojia, ili kupata maelezo na utayari wao.

Anasema, wapo wanawake hufika hospitalini bila ya wenza na wanahitaji mtoto, akisema mbegu zipo zinazotolewa na wanaume wachangiaji wa kujitolea, kama vile ilivyo kwa damu.

Tryphone anasemakinachotokea kwenye mwili wa mwanamke tangu akiwa tumboni mwa mama yake, akiba ya mayai ni nyingi na anataja makadirio inafika milioni sita akiwa utotoni na hupungua kufika milioni moja.

Anandelea: "Hadi mtoto wa kike anafikia hatua ya kubalehe, mayai yanakuwa yamepungua na kufika laki sita au nne na kila mwezi unavyooenda siku zake, mayai yanazidi kupungua. Watu hudhani mwanamke hupoteza yai kila mwezi, hapana! Mwanamke huweza kupoteza mayai mengi mwezi mmoja yanakuwa hadi 10 au 15 hata 20."

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, kadri umri wa mwanamke unavyosonga, idadi ya mayai hupungua, na kibaolojia mwanamke hatengenezi mayai, bali hupunguza kila mwezi.

"Mwanamke uolewe, usiolewe, uzae au usizae vyovyote vile kumbuka unayapoteza mayai kila mwezi kupitia siku zako kibaolojia. Unapofika 'levels' (kiwango) miaka 49 au 50 na kuendelea 'reserve' (akiba) inakuwa imepungua sana," anasema, akimlinganisha na mwanaume anayetengeneza mbegu kila baada ya siku 90 maisha yote, zikiwa na ubora kulingana na mlo wake, akimudu kumpa mwanamke ujauzito.

Bingwa huyo anasema mwanamke anapofika miaka 50 au zaidi, akiba ya mayai humuishia na siku zake za hedhi hukoma, lakini si kwamba hawezi kupata ujauzito, bali mtihani ataunganishwa na yai lipi.

"Kwa hiyo akiba ya mayai ikiisha sio suala muhimu, mfuko wa kizazi si bado upo, hapo ndipo huyu mwanamke anachohitaji ni yai la ziada kutoka kwa 'donor' (mchangiaji) na kisha linachanganywa na mbegu ya mwanaume, mimba tayari," anaeleza bingwa huyo.

**WANAWAKE WAGUSWA**

Gladness Mathias (47), mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, anasema tangu alipoona na kusikia taarifa, zikiwamo za mitandao ya kijamii kuhusu huduma ya upandikizaji mimba 'IVF' nchini, alivutiwa na kutaka kujua gharama na huduma yenyewe.

"Nilibahatika kupata mtoto mmoja miaka kama 10 imepita ingawa kila ninapotaka kutafuta mwingine na mume wangu imepita muda, tuseme imeshindikana. Niliwahi kwenda kwenye moja ya hospitali binafsi ipo jijini hapa hapa, gharama zake kubwa mno," anasema Gladness akitaja gharama hiyo wastani wa Sh milioni 15 hadi 18.

"Hapo watakaomudu gharama ni wenye fedha au matajiri, hayo mamilioni kwa mkupuo mmoja natoa wapi? Ingekuwa milioni mbili au tatu, ningesema nitadunduliza kwenye shughuli zangu na mume wangu au hata tukope, watoto ni faraja," anasema mama huyo.

Theonista Brighton (45), anasema hajawahi kupata mtoto, ila anatamani kuwa mama na alipofika penye matabibu, ikabainika njia pekee inayomfaa kitabibu ni kupitia IVF. Anaeleza: "Nilidhani ni kati ya huduma zilizomo kwenye orodha zinazotolewa na Bima ya Afya (Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya). Mimi Mtanzania wa kawaida Sh. milioni 15 naitoa wapi?," anasema Theonista.

Joseph Kayinga, mtaalamu wa Ustawi wa Jamii na Mshauri wa Mahusiano ya Familia, Malezi na Watoto kutoka Asasi ya Hero, anasema ni kawaida, binadamu yeyote hujiandaa kuwa ama mama au baba aitunze familia tangu utotoni.




Sehemu kunakopatikana huduma ya IVF jijini Arusha.

AFYA

# Hiki ndicho kichocho; muuaji wa kimyakimya, asiyefahamika vizuri

## • Namna kuu wanavyoambukizwa watoto..

**Na Waandishi Wetu**

KATIKA jamii, husikika sana kuhusu maradhi kichocho. Katika eneo la Ziwa Victoria, maradhi hayo yanatajwa kuwa juu zaidi, yakipewa alama ya hatari zaidi.

Je, hicho kichocho ni nini? Kimsingi, ni ugonjwa wa vimelea wa papo kwa papo na sugu unaosababishwa na minyoo midogo jamii iitwayo Shistosoma, inayoishi kwenye mishipa midogo ya damu mwilini mwa binadamu. Kichocho kinaweza kutokea katika namna mbili; moja kupitia mfumo wa utumbo na pili, katika mfumo wa mkojo.

Uambukizaji wake unatokana na mzunguko; mwenye minyoo anapojisaidia hovyo haja kubwa au ndogo, mayai ya wadudu hao yanaingia kwenye maji yaliyotuama kama mabwawa na dimbwi, kando ya ziwa au mito. Mayai hayo huanguliwa kuwa viluilui, kama konokono kwenye maji yaliyotuama, kisha huingia na kuongezeka ndani ya mwili wa konokono.

Viluilui hivyo hutoka ndani ya konokono, vinaingia ndani ya saa 48 vinakuwa hai, kisha kupenya kwenye ngozi na kuingia mwili wa binadamu aliyegusana na maji hayo.

Hapo, bila ya kuchukuliwa tahadhari za kujikinga dhidi ya mazingira kama vile kuoga, kuogelea, kufua, kuosha vyombo, kulima mashamba ya mpunga au miwa, kunabaki kuwa hatari zaidi.

Baada ya siku kadhaa, viluilui hubadilika kuwa minyoo kamili na vinaishi kwenye mishipa ya damu mwilini. Minyoo ya kike hutoa mayai na baadhi husafiri kwenda kwenye kibofu au utumbo, kisha baadae kinapatikana kwenye kinyesi au mkojo kuweza kuendeleza mzunguko wa maambukizi.



Picha mbili zenye mazingira rafiki yanayokaribisha maradhi kichocho. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

### DALILI ZAKE

Dalili za kichocho ni pamoja na kupata homa, kukojoa mkojo wenye matone ya damu, maumivu wakati wa kukojoa, pia sehemu ya chini ya tumbo au kitovu, au penye maumivu misuli ya mwili.

Pasipo kutibiwa ipasavyo, kichocho huendelea kuwapo mwilini mwa binadamu kwa muda mrefu hata miaka mingi na kumletea athari za kiafya. Kuna watu wengi wanaotambua dalili kama vile; kuvimba tumbo, ini kupanuka au kuharibika, utumbo mkubwa na figo kuathirika .

### MADHARA YAKE

Watu walioko kwenye madhara wanatajwa kuwa ni watoto wenye umri wa kwenda shule, ambao hawajaanza shule na watu wazima, sababu kuu ni kugusa maji.

Watoto hatari yao, zaidi inagusa upungufu wa madini chuma mwilini, ukuaji duni, kudumaa na uwezo mdogo wa kujifunza. Pia, kunatajwa madhara mengine kwa makundi yote ni, matatizo ya vibofu vya mkojo, pia figo kwa wanajamii wengi.

Kichocho kinatajwa kuwa na namna ya kimya kimya, kwenye afya za wanajamii. Mfano, mtu mwenye kupata tatizo la figo ni ngumu sana kutambua kuwa ni sababu ya ugonjwa wa kichocho ambao hakutibu kwa wakati hivyo leo kuleta madhara makubwa kwenye figo.

Pia, kwa aliyeathiriwa na kukosa matibabu ya kichocho kwa wakati, huwafanya wahusika wanatumia fedha nyingi, hata kuna wakati wagonjwa huangukia kwenye kifo. Hadi sasa kuna kundi kubwa la wanaopoteza rasilimali na maisha kutokana na kichocho.

### KINACHOENDELEA DUNIANI

Kwa ngazi ya dunia, kichocho kinatajwa kati ya magonjwa zaidi ya 20 yasiyopewa kipaumbele na takribani watu milioni 750 wanaishi katika maeneo yenye maambukizi makubwa, yakiwaweka hatarini kuambukizwa na inakadiriwa watu milioni 25 duniani wana kichocho.

Zaidi ya asilimia 90 ya watu walioambukizwa ugonjwa wa kichocho wanatajwa na takwimu wanaishi Kusini mwa Jangwa la Sahara, katika bara la Afrika.

Tafiti za awali kuanzia mwaka 2004, zinasema Tanzania iko katika nafasi za juu za ukubwa wa maambukizi ya ugonjwa kichocho, baada ya Nigeria katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, kuna wengi nchini Tanzania wameshaambukizwa ugonjwa huo.

Pia, kichocho nchini kinatajwa kimeenea sana sehemu nyingi na kuna tofauti ya maambukizi kati ya mikoa na ndani ya wilaya zake, zikitofautiana kasi ya kushamiri kati ya moja na nyingine. Maeneo ya Kaskazini Magharibi mwa nchi, ambako ndiko mwambao wa Mashariki na Kusini Mashariki mwa nchi, visiwa vya Unguja na Pemba kunatajwa kuwapo kwa wingi.

Hata hivyo, kuanzia miaka ya 2000, Shirika la Afya Duniani (WHO), kwa kushirikiana na serikali, pia wadau wamekuwa wakiongeza juhudi kupambana dhidi ya maradhi hayo duniani, ikiwamo nchini Tanzania.

Ni juhudi za pamoja, pia kampeni za kutoa kingatiba kwa watoto wenye umri wa kwenda shule. Mfano, serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Afya, kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo hufanya kampeni ya kugawa dawa aina ya Praziquantel kwa watoto wenye umri wa kwenda shule (miaka mitano hadi 14).



### NINI KIFANYIKE?

Kichocho kinaepukika, kwa kubadili baadhi ya tabia na kuendeleza zilizo chanya katika kujikinga. Kimsingi, ni ugonjwa unaosumbua jamii kila siku na namna inavyojiendesha.

Inatajwa ni muhimu kwa jamii, kuhakikisha inakuwa makini dhidi ya ugonjwa huo, hata ikabadili tabia hatarishi zinazongeza uwezekano wa maradhi mitaani.

Muhimu kwa watu ni kujihami kwa mengi kiafya, ikijumuisha kumeza kingatiba kila mara zinapotolewa kwenye jamii au shuleni, kujenga na kutumia choo kwa haja kubwa na ndogo na kuvaa vifaa kinga kama buti za mvua wakati wa kufanya shughuli kwenye maji yaliyotuama kama madimbwi, mabwawa na kando ya mito au ziwa.

Ligine linahusu suala la kutoa elimu kwa umma na kuueleza umuhimu wa kwenda penye kituo cha tiba kupata huduma stahiki, dhidi ya ugonjwa kichocho mapema kabla halijawa kubwa zaidi au kufikia hatua ya kushindwa kutibika.

Mfano, inapofikia figo inashindwa kufanya kazi kutokana na kichocho, pia kunatakiwa jitihada zaidi na kufuata ushauri unaotolewa na watoa huduma za afya; kuzuia watoto kuoga na kuogelea kwenye madimbwi ya maji yaliyotuama, pia kusafisha na kuondoa wadudu aina ya konokono katika maeneo yanayowazunguka na vyanzo vya maji.

Hali kadhalika kuna la muhimu, kutumia dawa kwa wakati na usahihi, bila ya kupuuzia ushauri wanaopewa na wataalamu wa afya.

**.Waandishi wa makala hii: Stephen Mbwambo (0752-814803) ni Ofisa Mpango katika Mpango wa Kudhibiti Magonjwa Yaliyokuwa Hayapewi Kipaumbele, Idara ya Huduma za Kinga na Wizara ya Afya na Pankras Luoga (0757645746), Mhadhiri Msaidizi wa Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).**

MAZINGIRA

# Angalizo; ulivyo umakini, njia panda katika uwepo wa aloevera nchini



Mtumiaji aloevera akiburudika nayo. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

**Na Waandishi Wetu**

ZAO la Aloevera limekuwa maarufu sana na sio geni kwa umma. Mtu akipita ama mitaani au kwenye basi, hata kwingineko hilo liko bayana.

Hiyo inatokana na kuongezeka matumizi ya bidhaa hiyo, ikishika nafasi ya kuwavutia watumiaji wa bidhaa hizo kuwa ni za asili, nzuri na zisizo na madhara.

Wanajamii wengi wamekuwa wakinaswa katika mtego huo na kununua bidhaa hizo hasa zile zinazosemekana kuwa na Aloevera ndani yake. Kwa umma kupata historia na elimu ya ndani zaidi juu ya mimea aina ya Aloe na kujua kuna aina nyingi za mimea hiyo. Inatajwa, kuwa na uwezo wa kusaidia jamii kuangukia usemi wa jumla "nenda katumie Aloe au Aloevera utapona".

Mmea aina ya Aloe ni mzuri kwa afya ila swali kubwa ni "aina gani ya Aloe ni nzuri kwa tatizo lako la afya ulilonalo?". Kwani kila aina ya 'Aloe' inatajwa kuwa tofauti na nyingine hata kama yote huonekana kama sawa, kiuhalisia ni tofauti kabisa.

Kwa mfano, kuna aina za mimea ya Aloe haina ladha na wala sio chungu, ila kuna aina nyinginezo ni chungu (inachacha) sana, pia ina sumu. Kwa hiyo, ni muhimu kwa jamii kuchukua tahadhari katika matumizi ya mimea ya aina ya Aloe nchini na nje ya mipaka.

**KULIVYO NCHINI**

Aloe (shubiri) ni mmea wa kijani kibichi ambao unaweza kutofautishwa kwa urahisi na aina zingine za mimea kwa majani yenye uteute na na yenye miba miba kama msumeno.

Aloe Vera ndio aina inayojulikana zaidi nchini Tanzania, japo kuna takribani aina 630 duniani. Tafiti zinaonyesha, nchini Tanzania kuna aina 52 kati ya hizo, 24 zinapatikana Tanzania Bara, Zanzibar na kuna aina nyingine za Aloe zinapatikana katika maeneo mengine ya nchi.

Asili ya juisi ya majani, huruhusu uhifadhi wa juu wa maji kwenye sehemu ya ndani kama uteute, ikiwa ni sehemu ya njia ya kukabiliana na hali ya ukame.

Aina, nyingi za Aloe hutoa majimaji ya manjano wakati jani linakatwa. Geli na majimaji ya manjano daima huwa na kemikali ambazo zinaweza kuwa chanzo cha dawa kwa jamii mbalimbali za watu, ingawa baadhi zinasadikika kuwa sumu na nyingine sumu hiyo hudhihirika mtu anapo kunywa kwa kiwango cha juu.

Nchini Tanzania, ni aina mbili tu zilizoripotiwa kuwa na sumu na nyingine zinatakiwa kuchukuliwa kwa tahadhari katika dozi ndogo.

**MATUMIZI YAKE**

Mmea wa Aloe una historia ndefu zaidi ya matumizi katika dawa za jadi duniani kote, ikianzia kwa Wasamaria zama za miaka BC 2100. Jamii nyingi za Kiafrika, hutumia aina za Aloe zinazopatikana katika mazingira yao ya karibu, kwa madhumuni anuwai, hasa dawa za binadamu na mifugo, vipodozi, kama maua, uzio, kutengeneza pombe, kuwaachisha watoto kunyonya na katika mila za kitamaduni.

Hadi sasa, matumizi ya aina ya Aloe yameenea katika dawa za jadi na dawa za kisasa za hospitalini kutokana na uwezo wa kukabiliana na magonjwa ya wanyama pamoja na hali ya afya ya binadamu kama vile; kuvimba, maumivu ya maungio na mifupa (arthritis), kisukari, maambukizi ya bakteria na fangasi.

**ALOE VS UMAARUFU**

Kwa kuwa watu wengi hasa vijana, wanataja aina ya Aloe kama ;Aloevera' badala ya kutumia majina ya lugha asilia, matumizi yake ya asili na Kiswahili yameonekana yanapungua.

Kikubwa ni kwamba, Aloevera haipatikani katika ardhi ya Tanzania kama mmea wa asili. Hiyo, inatajwa kutokana na jina lake kama chapa ya bidhaa na kutambulika zaidi kwa mmea huo kimataifa, kuliko aina zingine za Aloe.

Kwa watu wengi, hilo sasa linatumika kama jina la kawaida kwa aina yoyote ya Aloe inayopatikana nchini.

**TISHIO KUPOTEA**

Isipokuwa Aloevera, inalimwa kwa wingi duniani, aina nyingine sasa zinatishiwa na ukusanyaji na uvunaji holela usiozingatia kanuni na biashara haramu.

Hiyo inatokana na mahitaji yake kuongezeka kila siku na kuwa makubwa kama dawa na kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za kibiashara. Inashangaza kujua kwamba, karibu robo (23%) ya aina za Aloe ziko hatarini kupotea, kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Kimataifa wa Uhifadhi wa Mazingira ( (IUCN)).

Pia, utafiti wa Fredrick Ojija na wenzake nchini Tanzania uliotoka mwaka jana (na kuchapishwa kwenye Jarida la Afrika Kusini la Mimea) juu ya hali ya mgawanyo, tabia na uhifadhi wa mimea ya aina za Aloe zilizopo hatarini kutoweka, ilionyesha kuwa Aloe boscawenii, Aloe flexilifolia, Aloe leptosiphon and Aloe dorotheaeni baadhi ya aina za aloe zilizo hatarini kutoweka nchini.

Zaidi, ni kutoka kwa mtafiti Siri Abihudi, mwaka juzi anasema hali ya uhifadhi na mitazamo ya jamii juu ya aina za mimea ya Aloe inaonesha kuwa aina 22 zipo hatarini kutoweka nchini.

Pia, inatajwa shughuli za kibinadamu kama vile uchomaji moto kwa makusudi, uvunaji asali kwa kutumia moto, upanuzi na usafishaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo katika maeneo yenye maliasili, makazi ya watu na uvunaji wa Aloe kupita kiasi, huleta vitisho vya upotevu wa aina za Aloe duniani.

**ALOE NA MAZINGIRA**

Aina za Aloe zinaweza kuokolewa na kuhifadhiwa, ili kutotoweka porini ikiwa zitalimwa kwenye mashamba na bustani za nyumbani. Watunga sera wanasema wanaweza kutumia tafiti mbalimbali za mmea huu kujua ni aina gani kati ya aina nyingi za Aloe zilizo hatarini, kutoweka na zinazostahili kulindwa.

Kwa kuzingatia uhaba wa rasilimali zilizopo na idadi kubwa ya aina za Aloe zilizo hatarini kutoweka, ni muhimu kuongeza juhudi za uhifadhi.

**.Waandishi; Siri Abihudi (+ 255 682 746625), ni Mhadhiri Msaidizi, Taasisi ya Dawa Asili , Chuo Kikuu cha Sayansi na Tiba Muhimbili, na Pankras Luoga (0757645746), Mhadhiri Msaidizi wa Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini wa chuoni hapo.**



Mmea aloevera katika sura tofauti za matumizi.

AFYA

# Kamanda Trafiki atoa darasa la mtaji elimu barabarani unavyonusuru uhai

**Na Halfani Chusi**

KATIKA nyendo za Jeshi la Polisi kukabili usalama wa watu na mali zao, imebainika katika maeneo yanayowaumiza kichwa wahusika ni katika kukabili, uhalifu wa kijambazi na wizi, hali kadhalika usalama barabarani, kwa maana ajali za vyombo vya moto na wanaotembea kwa miguu.

Bado kuna kumbumbu wakati fulani akitimiza mwaka mmoja wa utendaji wake, aliyekuwa Inspekta Jenerali wa Polisi Saidi Mwema, alitaja kwamba alipiga hatua kubwa kukabili matukio ya ujambazi, akibakiwa zaidi na changamoto iliyomuumiza kichwa wakati huo, kuhusu udugu wa ajali barabarani na matukio yake kutopungua.

Hadi sasa, inafafanuliwa kwamba katika kumaliza ajali za barabarani, muhimu hasa ni lazima elimu iwe kipaumbele, kwa rika zote za umma na mahsusi watoto, ambao wanapokuwa barabarani usalama wao unakuwa hatarini zaidi.

Ingawa iko bayana zaidi ni vigumu kufikia nadharia 'vifo sifuri vya ajali kwa mwaka,' lakini jitihada za kuwafikishia watumiaji wa barabara elimu sahihi ya namna sahihi inatajwa muhimu katika kupunguza matukio hayo.

Hilo haliishii kwa wenye magari pekee yao, bali watembea kwa miguu nao wanahitaji elimu ya namna ya kutumia barabara, pindi wanapokuwa katika mizunguko yao katika mazingira ya barabarani.

Katika hilo, Mkuu wa Polisi kitengo cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Ramadhani Ng'anzi anasema ajali nyingi za barabarani zinatokea kwa baadhi ya madereva kutokuzingatia sheria na baadhi ya askari wa jeshi la polisi kupokea rushwa kuruhusu chombo kibovu kutembea barabarani, kitu anachokitaja kuwa sumu ya ajali kutokea

"Tunatamani ajali hata moja isitokee na huwa tunaomba Mungu dereva anapotoka nyumbani asubuhi arudi salama kama alivyoondoka, lakini silaha yetu kubwa katika kupambana na ajali hizo, ni kutoa elimu kila siku bila kuchoka

"Kingine ni kufanya kazi kwa kujituma, kwa trafiki hawa wanafanya kazi saa 24, ukitoka asubuhi nyumbani unamuona barabarani na ukirudi kazini jioni unamkuta tena, kwa hiyo hawa nao ni nguzo muhimu katika kupambana na ajali," anasema na kuongeza: "Jeshi la Polisi na taasisi mbalimbali na wadau wa maendeleo vikiungana kwa pamoja tunaweza kuzuia ajali hadi kufikia sifuri"



Mkurugenzi wa Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani (TARSI), Maliki Barongo kushoto, akiwa kwenye picha ya pamoja na Inspekta Msaidizi wa Polisi Violet Hoja (katikati) na kushoto ni Hashim Rajabu, Mkuu wa Programu wa taasisi hiyo, baada ya kumaliza kutoa elimu katika Shule ya Sekondari, Mivumoni iliyoko Kinondoni.

**VYANZO VYA AJALI**

Kamanda huyo, alisema ajali za barabarani husababishwa na mambo mengi, ikiwamo kutumia ulevi kwa waendesha magari. SACP Ramadhani Ng'anzi anaendelea: "Sababu nyingine ni mwendokasi ukiwa kasi ukipata ajali madhara yake huwa ni makubwa kuliko ukiwa katika mwendo mdogo.

"Lakini, wengine hawapendi kufunga mkanda wanapotumia usafiri wa umma hiki nacho pia ni chanzo cha ajali na vifo. Usipofunga mkanda gari likipata ajali unaweza kujikuta umetokeza mbele kwenye kioo cha dereva, sasa hapo lazima madhara utakayopata yatakuwa makubwa sana tofauti na yule aliyefunga mkanda."

Pia, kunatajwa sababu nyingine ni kuendesha gari mtu akiwa amezama katika mitandao ya simu, pia kusikiliza muziki na kucheza kwenye gari. Hapo Kamanda Ng'anzi anaeleza kuwapo ajali zinazosababishwa na ubovu wa chombo cha moto.

Aidha, mkuu huyo ana angalizo, kwamba kabla ya mwedeshaji kuingia barabarani, anatakiwa kukagua chombo chake kama kinaweza kumudu mikiki ya barabarani ndipo akiruhusu kuingia barabarani.

Pia, ana mtazamo kwamba, ajali zingine hutokana na ubovu wa barabara kukiathiri chombo cha moto, vyote hivyo anataja alama za barabarani kwa baadhi ya maeneo, pamoja na hali ya hewa hasa maeneo yenye utelezi.

**WADAU WANAVYOJITOKEZA**

Taasisi inayojihusisha na Mpango wa Usalama Barabarani (TARSI), ilizindua kampeni ya elimu kwa wanafunzi walioko shuleni juu ya masuala ya usalama barabarani, jambo ambalo limekuwa na mafanikio makubwa na kuzifikia shule nyingi.

Mkurugenzi wa Taasisi Hiyo, Maliki Barongo anasema wamechagua kuwafikishia elimu wanafunzi walioko shuleni kwa kuwa asilimia kubwa maisha yao wanatumia barabara.

Anasema mpaka kufikia sasa wameshazifikia shule 15 nane za msingi na saba za sekondari akibainisha kuwa jumla ya wanafunzi waliopata mafunzo ya moja kwa moja ni 1,125.

"Tumeshazifikia shule nyingi za msingi na sekondari wengi wao wamepata elimu ya usalama barabarani na imewaokoa wanaweza kujiepusha na ajali.

"Baadhi ya shule ambazo tumezifikia ni Shule ya Msingi Bongoyo, Makumbusho, Oysterbay, Mivumoni na Shule ya Sekondari Makumbusho, Ananasifu iliyoko Kinondoni, Osterbay hizo ni chache kati ya tulizozifikia lengo ni kuifikia Tanzania nzima" anasema na kuongeza;

Anafafanua kuwa ajali za barabarani si kuiachia serikali pekee bali ni la kuungwa mkono na kila mdau kwa sababu madhara yake ni makubwa sana

"Hili ni jambo mtambuka ambalo kwa kiasi kikubwa kwa ukubwa wake linapaswa kuungwa mkono na wadau wengine wa maendeleo taasisi inapojitokeza kutetea uhai wa mtu ni kiashiria tosha kwa miaka ya baadae tutamaliza kabisa vifo vitokanavyo na ajali za barabarani.

"Mwili wa binadamu hauna spea, kwa hiyo watumiaji wa barabara pamoja na madereva zingatieni sheria, ukiona taa nyekundu barabarani imewaka, hata kama hakuna gari usivuke subiri mpaka taa ya kijani," anaelimisha kwa darasa mfano.

Mkurugenzi huyo anasema mbali na kufanya jambo zuri ambalo linaungwa mkono na wazazi pamoja na maelfu ya watanzania lakini bado anakabiliana na ufinyu wa bajeti.

"Wadau kujitokeza kutuunga mkono kwa kutufadhiri ili tuweze kuwa na nguvu ya kuifikia kila shule kwa sasa tumeanza kutoa elimu katika wilaya ya Kinondoni lakini tunatamanai kuifikia mikoa yote ya Tanzania.

"Tunaamini kwa namna tulivyojipanga na wataalamu waliobobea katika utoaji wa elimu ya usalama barabarani elimu tunayotoa itaiwezesha nchi kupunguza vifo vitokanavyo na ajali za barabarani kwa kiwango kikubwa"

**WANAFUNZI WALIOELIMISHWA**

Katika kufahamu umuhimu wa elimu hiyo Nipashe ilimtafuta mwanafunzi kutoka katika Shule ya Sekondari Mivumoni, Buthaina Salum, anayekiri kupata mafunzo, pia akibainisha kuwa yamemuongezea uelewa juu ya usalama barabarani.

Mwanafunzi mwingine Mary Kato, alisema kwake limekuwa jambo kubwa sana katika maisha yake hakuwahi kufikiria kupata elimu hiyo ameyaona makosa mengi ambayo alikuwa anayafanya wakati anatumia barabara.

"Nimebaini nilikuwa nina mapungufu makubwa katika kutumia barabara kwa sababu nilikuwa sizifahamu sheria za kuzingatia ninapotaka kuvuka mfano nilikuwa sifahamu zile taa zina maana gani, sasa nimejua.

Anatoa mfano, hakujua maana ya pundamilia na vitu vingine vingi.



Inspekta Msaidizi wa Polisi, Afande Violet Hoja akitoa elimu ya usalama barabarani kwa wanafunzi, ikiwa ni sehemu ya kutimiza wajibu wao kwa kushirikiana na Taasisi ya Mpango wa Usalama Barabarani. **PICHA ZOTE:HALFAN CHUSI**

AFYA

# Benki Dunia yasitiri wanafunzi kwa kuzijengea shule 49 vyoo maalum

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

TATIZO la ukosefu wa chumba maalumu shuleni kwa ajili ya kujistiri hedhi wanafunzi kwa kike ni kikwazo kikubwa katika kufanya vizuri kwenye masomo yao kutokana na kukosa baadhi ya vipindi hasa wanapoingia kwenye siku zao.

Shule ya Msingi Mahembe wilayani Shinyanga, ni ambayo awali wanafunzi wake walikuwa wakikabiliwa na tatizo la ukosefu wa chumba cha kujistiri na kusababisha kukosa vipindi vya masomo.

Benki ya Dunia baada ya kuona tatizo hilo, wakaamua kutoa fedha kwa shule za msingi 49 mkoani humo, kujenga matundu 1,000 ya vyoo ambayo yatazingatia chumba maalumu kwa ajili ya wanafunzi wa kike kujistiri na kutokosa vipindi vya masomo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mahembe wilayani Shinyanga Prosper Enias, anasema walipokea fedha kutoka benki kuu ya dunia Sh. milioni 39 kwa ajili ya ujenzi wa matundu 31 ya choo kwa kuzingatia pia na chumba maalumu cha wanafunzi kujistiri.

Anasema ujenzi wa matundu ya vyoo ulianza mwaka jana, na wanafunzi wameanza kuvitumia vyoo hivyo na kuachana na vile vya zamani ambavyo vilikuwa vibovu na kuhatarisha afya zao.

Mwalimu Mlezi wa Hedhi Salama, shuleni hapo Tatu Ramadhani, anasema kabla ya shule hiyo kujengewa matundu ya vyoo na ukosefu wa chumba maalumu cha hedhi, wanafunzi wa kike walikuwa wakiomba ruhusa kila mara na wengine kuwa watoro sababu ya kuingia siku zao.

Anasema kutoka hapo awali katika shule hiyo kutokuwa na chumba maalumu, utoro kwa wanafunzi wakike ulikuwa mkubwa sababu ya kukosa sehemu ya kujisafisha, na kuamua kubaki nyumbani na kusababisha kukosa vipindi vya masomo.

"Chumba maalumu cha kujistiri hedhi shuleni ni muhimu sana, sababu kinapokosekana wanafunzi wa kike hushuka kitaaluma sababu ya kukosa vipindi vya masomo yao wanapoingia kwenye siku zao," anasema Ramadhani.

"Baada ya kujengewa chumba maalumu cha hedhi shuleni hapa na uwekaji wa Taulo za kike kwenye chumba hicho, hakuna utoro tena kwa wanafunzi wa kike, sababu wanapata huduma zote hapa hapa shuleni na wanafanya vizuri kwenye masomo yao," anaongeza Ramadhani.



Wanafunzi wa mkoani Shinyanga wakiwa na moja ya huduma walizopewa kuwasitiri masomoni. **PICHA: MTANDAO.**

### MWANAFUNZI AFUNGUKA

Mwanafunzi wa shule hiyo (jina tunalo), anasema kutokana na hapo awali shule yao kutokuwa na chumba maalumu cha kujistiri, alikuwa akibaki nyumbani hadi hapo siku itakapoisha na kurejea shuleni tena.

Mwanafunzi mwingine naye anasema, mazingira ya vijijini upatikanaji wa taulo za kike ni vigumu ambapo hapo awali walikuwa wakitumia vitambaa kwa kuchana nguo, hivyo kukaa navyo siku nzima bila ya kujisafisha wakiwa na hedhi na kuamua kurudi nyumbani na kuacha kwenda shule. "Shuleni hapo awali hapakuwa na chumba cha kujistiri hedhi wala maji ya kujisafisha na ukikaa na kitambaa kutwa nzima kina washa, hivyo unaamua kurudi nyumbani na siku inayofuata siende shule nabaki tu nyumbani," anasema Bundala.

Anasema lakini sasa hivi baada ya kuwapo na chumba hicho maalumu cha kujistiri hedhi na maji ya kutosha huku wakipewa taulo za kike shuleni hapo kwa ufadhili wa benki ya dunia, hawakosi tena vipindi vya masomo na wamekuwa wakifanya vizuri kitaaluma.

Mzazi Mpelwa Kubini, anasema watoto wao wanapoamua kubaki nyumbani kwa ajili ya kujisitiri hedhi, hawawazuii sababu ya mazingira ya shule kutokuwa rafiki kwao kwa kukosa chumba maalumu cha hedhi.

Anasema kiusafi mwanamke anapokuwa katika hedhi na kutumia vitambaa anapaswa abadilishe mara kwa mara kwa ajili ya usafi na akishinda na kitambaa hicho kutwa nzima ni hatari pia kwa afya yake na hata kupata fangasi sehemu zake za siri.

"Tunashukuru wadau hawa wa maendeleo kwa kujenga chumba maalumu cha wanafunzi kujistiri hedhi hapa shuleni na watoto wetu siyo watoro tena bali wanahudhuria shule kila siku hata kama wakiwa katika siku zao,"anasema Mpelwa.

Mratibu wa mradi wa ujenzi wa matundu ya vyoo kwa shule za msingi mkoani Shinyanga, Dedani Rutazika kutoka Ofisi ya Elimu mkoani humo, anasema chumba maalumu cha hedhi salama ni mkombozi kwa wanafunzi wa kike kufanya vizuri kitaaluma.

Anasema mradi huo wa ujenzi wa matundu ya vyoo na chumba maalumu cha kujistiri hedhi kwa wanafunzi wa kike umetekelezwa katika shule 49 za msingi na utanufaisha wanafunzi zaidi ya elfu 50, katika halmashauri tatu ambazo ni Kishapu, Ushetu, Msalala na Halmashauri ya wilaya ya Shinyanga.

"Maelekezo yaliyotolewa kwenye ujenzi wa matundu ya choo katika shule hizi za msingi 49 mkoani Shinyanga na benki ya dunia ni kujenga pia chumba maalumu kwa ajili ya wanafunzi wa kike kujistiri hedhi na kuwapatia taulo za kike, lengo wasikose vipindi na kufanya vizuri kitaaluma,"anasema Rutazika.

Anafafanua kuwa mwanafunzi wa kike anapoingia katika siku zake, na kushindwa kuhudhuria masomo shuleni, hukosa vipindi kwa muda wa siku tatu na wengine hadi siku tano sawa na wiki nzima na lazima afanye vibaya sababu kapitwa na vipindi.

### BENKI DUNIA

Mwakilishi wa Benki ya Dunia nchini Tanzania Rwegoshora Makaka, anasema ukosefu wa vyumba vya kujistiri shuleni kwa jinsia ya kike, ni miongoni mwa vikwazo vikubwa katika kukuza elimu ya mtoto wa kike, na kutaka taulo za kike ziwekwe kwenye vyumba hivyo muda wote, ili kuwaondolea usumbufu wanafunzi.

"Naomba taulo za kike ziwepo kwenye chumba maalumu cha hedhi muda wote na siyo mwanafunzi aje kuomba kwa mwalimu, wengine wanaweza kuona aibu na kuamua kutoroka kwenda nyumbani, hapo tunakuwa hatujatibu tatizo," anasema Makaka.

MAZINGIRA

# Ulivyo utashi wa mazingira, miliki, utetezi ardhi na nafasi ya mama



Kinamama wakiwajibika shambani., **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

WAKATI harakati za vikundi vya haki za binadamu na vile vya msaada wa kisheria zinalenga wanawake kuondoa vizuizi vya kumiliki ardhi kwa hatimiliki ya jadi, yako maeneo mengi ambako wanawake wanafuata mkondo tofauti.

Mtihani wa umiliki wa ardhi kwa mwanamke mara nyingi unajitokeza mume anapokufa, halafu ndugu zake wanataka wao ndiyo wakabidhiwe milki, kiukoo. Zamani au katika jadi huyo mjane alikuwa anarithiwa vile vile na ndugu wa karibu wa marehemu mumewe.

Kuingia kwa janga la Ukimwi kulivuruga mpangilio huu wa jadi kwani haikuwa tena rahisi umrithi mke wa mtu aliyekufa kwa Ukimwi, na hata angekufa bila ugonjwa huo, mjane asingejua kama anayetaka kumrithi ana ugonjwa au hapana. Ikawa ni kama kutegeana na kunyanyapaa, hali ambayo inabadilisha kinachotazamiwa katika mila, kuwa mwanamke anaridhika na huyo mwanamume anakuwa na furaha kwa fursa hiyo. Sera ya jadi ikahamia katika kumwacha atumie shamba na wanawe, asiolewe.

Ila zipo koo ambako baadhi ya wahusika wanajiongeza, hasa pale ardhi inapokuwa na thamani kubwa, eneo bora la mazao ya biashara, kwa mfano mkoani Morogoro. Hapa sera kificho ikawa ni kumfukuza mjane na akikaidi anadhurika kimazingara na wanae wanatawanyika,au wakibaki kwa ndugu zao wa karibu wanakuwa watumwa;. Ni watoto ambao watasoma endapo shule ni bure na ni lazima kumpeleka mtoto shuleni.

Ndiyo mazingira ambayo wanaharakati wamejaribu kuyatatua kwa kulenga vipengele vya sheria ya ardhi, na kwa sehemu kubwa wanaweza kusema wamefaulu, kwani wanawake wanaachiwa kutumia ardhi bila manyanyaso ya wazi. Tatizo linaweza kutokea endapo suala la urasimishaji lipo, kwani ardhi haiwezi kumilikishwa kwa huyo mwanamke au mjane kwa hatimiliki ya jadi, kwani hali hiyo itampa haki zaidi ya alizonazo kwa kuolewa ndani ya ukoo ule. Atazaa na yeyote ammilikishe mwanae.

Jambo ambalo pia halifikiriki ni mwanamke huyo amkaribishe mtu wa kutoka kwingine akae naye, na mtu huyo awe kama ndiyo mmiliki wa ardhi wakati siyo wa ukoo huo. Ni masuala ya wazi katika sheria ya umiliki ardhi kimila lakini wanaharakati wanaona ni vizuizi tu vya kuwabagua wanawake, hivyo wanalenga mikondo ya sheria. Wakati mmoja Rais Samia Suluhu Hassan akapania kuwapa tafu (mkutano wa miaka 25 ya asasi ya utetezi kisheria kwa wanawake barani Afrika - WILDAF), akisema sheria za unyanyasaji wa kijinsia ziwe na meno, zing'ate.

Endapo sheria hizo zingepewa meno katika eneo la umiliki wa ardhi, jadi ingefutwa yote kwani haitambui jinsia katika suala la ardhi ila ukoo. Kinachofuata ni katazo la jadi (na dini) la mwanamke kuolewa au kuzaa na mtu asiye mume wa ukoo huo wakati angali katika ardhi hiyo, jambo ambalo wanaharakati, wasiotambua jadi, wangefuta. Wanawake wanajua suala hilo haliwezi kutatuliwa kwa urahisi, hivyo wanatumia njia za kununua ardhi ili kumiliki, na si kusukumana katika vikao vya mabaraza ya ardhi vijijini au wilayani kwa umiliki. Kimsingi wanataka kuwa na ardhi yao, si kupigania kurithi.

Huu ni upande mwingine wa 'karata' ya hakiardhi kwa upande wa wanawake ambayo inatoa majibu ya haraka zaidi kwa suala la mwanamke kuwa na ardhi. Ni kuachana na kununua ardhi pale inapopatikana, au kama mwanamke husika ana kipato au msaada mwingine, kujipatia hata kiwanja ambako anaweza kujenga kibanda, akae na wanae.

Ni sehemu ya maendeleo ya uchumi na mabadiliko katika soko la ardhi ambako wengi kati ya wanaonunua vipande vya ardhi ni wanawake, kwa ajili yao na wanaowahusu kama jamaa zao walikozaliwa, au watoto waliowazaa. Hapo hauna suala la kuwa na mume kwani ni kurudisha upya mtego wa jadi.

Kimsingi harakati inayoendeshwa na vikundi vya kisheria inalenga kuboresha mfumo wa jadi kuweka haki sawa kwa wanawake, kwa kusita kuangalia mfumo huo machoni, kuwa jadi msingi wake ni ardhi ya ukoo.

Pale Sheria ya Ardhi na Sheria ya Ardhi ya Vijijini ya Mwaka 1995 inazungumzia vijiji, kinacholengwa hapo si eneo tu la kijiji ambako ndani yake wako wanaume na wanawake walio na haki sawa ila tu jambo hilo halizingatiwi hasa katika urithi, wakati ni koo ndiyo msingi wa vijiji hivyo. Ardhi ya aina hiyo hurithishwa kutoka baba kwenda kwa mwanae wa kiume, aoe mke aendeleze familia hiyo, basi.

Hisia ya watetezi wa kisheria kimsingi, inaendana na ile ya sheria ya ardhi kwa upande mmoja na sheria ya ardhi ya vijiji kwa upande mwingine, yaani kwa hisia kuwa kila mtu (nje ya wanaokaa mijini na hawana mizizi vijijini) ni mrithi au mwezeshaji wa urithi. Kwa lugha nyingine wanaume ni warithi watarajiwa hasa kwa kugawana mashamba au maeneo ya mashamba vijijini, halafu wanawake huolewa ili kuwezesha koo hizo kwenda mbele.

Suala la usawa kati ya watoto wa kiume na wa kike katika kugawa ardhi ya baba yao halina maana katika jadi; ulemavu tu wa kuielewa jadi unaleta mzozo kama huo.

Kwa maana hiyo jadi haiwezi kuoanishwa na harakati za usawa wa kijinsia katika ardhi ya ukoo, na ukweli ni kuwa wanawake wengi tayari wameshafuata 'plan B' ya kufuatilia dhamira ya kuwa na ardhi ambayo haihusiani na kuolewa.


Ni miongoni mwa wanawake wanaofanya biashara, au wana ajira nzuri kuweza kununua ardhi na kuweka kitu hapo, au wanastaafu na kutumia mafao yao kwa umiliki wa ardhi. Ni wanawake ambao wanaingia katika biashara ya ardhi na uwekezaji, kilimo cha kisasa na ujenzi wa nyumba mijini, pango za biashara.

Ukizungumza na wanawake walio na ardhi utagundua kuwa wanajua hawawezi kurithi ardhi ya ukoo na kuiuza, ila kama tayari ilikuwa imenunuliwa hapo mwanzo, hivyo ni mali ya mtu binafsi. Urithi wa ardhi unatofautiana ila kila aina ya urithi inatawaliwa na jadi kwa kiwango fulani, kwa mfano mwanamke akiwa na ardhi au nyumba mjini atapendelea zaidi kumrithisha mwanae wa kiume au mwana wa kiume wa ndugu yake wa karibu, ili iendelee kuwa mali ya familia anapokuwa hayupo tena. Ila mrithishwa huyo anaweza kuuza mali hiyo wakati wowote kwani haipo katika ukoo, haina dhamana kwa vizazi vijavyo.

Washirika wa soko la ardhi na wanaohitaji umiliki wa aina hiyo tofauti na ule wa vijiji ni wengi, kwani mtu akishakaa mjini na kuwa na mali huku, inabidi aangalie mara mbili kama anahitaji tena umiliki wa ardhi, kwa maana ya shamba, kijijini. Anapokuwa na ngazi tofauti ya kitabaka na walio vijijini, anatakiwa awe mfadhili tu wa shughuli hizo, aachie shamba la kijiji kwa ndugu zake. Endapo haelewi jambo hilo anang'ang'ania umiliki, anaweza kuharakishwa kuliachia kama ilivyo kwa mjane pale mumewe akifariki na hana watoto wakubwa wa kiume wa kulinda maskani ibaki kwa familia hiyo.

Ina maana kuwa katika kauli ya mwisho umiliki wa ardhi wenye tija ni ule unaoanzia katika biashara, kwa kununua shamba au kiwanja. Nje ya kuuza kiwanja mara mbili katika maeneo yenye msongomano, jambo linaloweza kumpotezea nguvu na raslimali na hata kuhatarisha usalama au maisha yake, mfumo huu ni bora zaidi. Hata maeneo ya vijijini, kutokana na ongezeko la watu, yanabadilika hatua kwa hatua kuondoka katika hali ya mashambani kuwa miji tarajiwa. Pale biashara zinapoongezeka, walio karibu na miji midogo wanatangulia kuuza ardhi, halafu walio ndani zaidi watafuata baadaye.

# Mtu mrefu anayekua kila siku, mbioni kumpiku mshindi Guiness





**Na Mwandishi Wetu**

ILIANZA fununu za mwanaume mrefu zaidi duniani, anayepatikana Kaskazini mwa nchini Ghana. Hospitali ya eneo la Kaskazini mwa Ghana, ilimwambia Sulemana Abdul Samed (29), wakati wa uchunguzi wake wa hivi karibuni kwamba, alikuwa amefikia urefu wa futi tisa na nchi sita ( 9 ft 6in) kwa kipimo kingime ana urefu wa mita 2.89.

Hiyo inamfanya kuwa mtu mrefu zaidi duniani, lakini kulikuwa na changamoto, kwamba kliniki ya kijijini haikuweza kuwa na uhakika wa urefu wake kwa sababu haikuwa na zana sahihi za kupimia.

Alipogunduliwa na ugonjwa wa gigantism unaomfanya kukua kwa kasi kubwa miaka michache iliyopita, kijana huyo alikuwa akihudhuria klikini ya kila mwezi.

Muuguzi aliyeshtuka hali hiyo, akamwambia: "Umekua mrefu kuliko mizani."

Hilo limemfanya kujulikana zaidi kwa jina la utani Awuche, linalomaanisha "Twende" kwa lugha ya Kihausa.

Hakushangaa kusikia yeye ni mrefu zaidi, ikizingatiwa kuwa hajawahi kuacha kukua, lakini ilisababisha mshangao kwa wafanyakazi, ambao hawakuwa wamejiandaa kwa hali kama hiyo.

Muuguzi wa zamu akamwita mwenzake, ambaye naye alimwita mwingine kuomba msaada. Baada ya muda fulani si muda kundi la wauguzi na wasaidizi wa afya walikusanyika ili kutatua kitendawili cha kuamua urefu wake.

Muuguzi mmoja alipendekeza watafute nguzo na kuitumia kama nyongeza juu ya fimbo yao ili kupima urefu wake - na hivi ndivyo walivyofikia makadirio yao.

ANAENDELEA KUKUA

Miezi michache iliyopita, Awuche akisafri Kaskazini mwa Ghana, umaarufu wake ulienea: "Jinsi wanavyonipima, siwezi kusema kila kitu ni sawa,"

Awuche anakiri kufurahishwa na mpango wa kupatiwa kipimo kamili, ana viatu vyake vya kandambili kubwa maalum zitokanazo na matairi ya gari.

Katika kumpima, mmoja wa wapimaji alipanda juu ya stuli ya kufikia urefu wa Awuche, ili aweze kuweka alama ukutani kwa kipande cha makaa.

Baada ya kuthibitisha mstari, ukanyooshwa utepe wa kupimia urefu huo, yeye akiwa na tabasamu kubwa"

Rekodi ya mtu mrefu zaidi aliye hai ana urefu wa futi 8 na inchi 2.8, akiwa na futi moja zaidi, akirejewa Sultan Kosen (40) anayeishi Uturuki, akishikilia rekodi ya Dunia ya Guinness.

"Bado ninakua mrefu. Nani anajua, labda siku moja naweza kufikia urefu huo pia," Awuche alisema - bila kukerwa hata kidogo na tofauti ya takwimu aliyopewa na hospitali.

**ULIMI UNAOKUA**

Ongezeko hili la urefu lilianza kuonekana alipokuwa na umri miaka 22, baada ya kumaliza shule ya upili.Alikuwa akifanya kazi kwenye bucha, akiweka akiba ya pesa za kusoma katika shule ya udereva.

Lakini aliamka asubuhi moja akiwa amechanganyikiwa: "Niligundua ulimi wangu ulikuwa umepanuka mdomoni mwangu kiasi kwamba sikuweza kupumua," anasimulia.

Alitembelea duka la dawa la mahali hapo kupata dawa, hata hivyo siku kadhaa baadaye aligundua kuwa kila sehemu nyingine ya mwili wake ilikuwa imeanza kuongezeka ukubwa.

Wakati familia na marafiki kutoka kijijini kwake walipotembelea jiji hilo, wote walisema juu ya kasi ya ukuaji wake na ilikuwa wakati huu aligundua kuwa polepole alikuwa akigeuka kuwa jitu.

Alianza kuwa juu ya kila mtu - na alitafuta msaada wa matibabu kwani ukuaji ulileta shida zingine. Amebaki na mgongo uliopinda isivyo kawaida, mojawapo ya dalili kuu za hali yake, ugonjwa wa Marfan, unaoathiri tishu-unganishi za mwili.

Pia, inasababisha miguu mirefu isiyo ya kawaida.Matatizo makubwa zaidi yanahusisha kasoro za moyo.



Madaktari wanasema anahitaji kufanyiwa upasuaji katika ubongo wake ili kuzuia ukuaji huo. Lakini bima ya afya ya umma ya Ghana, haiwezi kulipia hilo. hapa anahitajiwa takriban, Dola 50 (Sh. 115,000)

Matatizo yake ya kiafya hatimaye yalimlazimu kurejea kijijini kwao kwa miaka sita akiachana na ndoto zake za kuwa dereva.

"Nilikuwa napanga kwenda shule ya udereva, lakini hata ninaporudisha kiti nyuma, siwezi kushikilia usukani... siwezi kunyoosha mguu wangu kwa sababu goti langu litagonga gurudumu."

Sasa anaishi na kaka yake- na anajikimu kimaisha kwa biashara ndogo ya kuuza masalio ya simu za rununu .

Urefu wake pia umepunguza maisha yake ya kijamii.

"Nilikuwa nikicheza soka kama vijana wengine wote, nilikuwa mwanariadha lakini sasa siwezi hata kutembea umbali mfupi," alieleza.

Mtu Mashuhuri

Lakini Awuche haruhusu matatizo yake yamwangushe. Amejawa uchangamfu huku umbo lake jembamba likipita katika njia zenye vumbi za kijijini - akitabasamu huku watu wakimuita.

Kundi la wazee jirani humsifu kuwa mtu mashuhuri.

"Kwa kawaida nitasema: 'Ndiyo njoo karibu' - tunasimama na kupiga picha nzuri," Awuche anasema akiishukuru sana familia yake kwa msaada wao.

**•Kwa mujibu wa BBC.**



# Wahakikishiwa kulipwa fidia maeneo ya hifadhi

**Na Grace Mwakalinga,**

MBARALI

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Eliamani Sedoyeka, amewahakikishia wananchi wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, waliondolewa kwenye maeneo ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kulipwa fidia kulingana na maeneo waliyokuwa wakiishi.

Alitoa kauli hiyo juzi baada ya kukagua kazi ya uwekaji wa alama za mpaka na uthaminishaji wa mali za wananchi waliomo ndani ya Hifadhi ya Taifa.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Iyala eneo ambalo uthaminishaji unaendelea, alisema wizara inatambua na kuthamini kazi kubwa wanayoifanya ya uzalishaji mali kupitia kilimo.

"Baada ya kukamilisha kazi ya uthaminishaji wananchi watalipwa fidia zao na kwenda maeneo mengine kwa ajili ya kuendelea na shughuli za uchumi kupitia kilimo na ufugaji," alisema Prof. Sedoyeka.

Katibu wa Kamati hiyo, Yassin Sharif alisema wametoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa uwekaji mipaka ili kuondoa taharuki na kujenga uelewa kwa wananchi.

Alisema mpaka sasa mawe 405 yameshawekwa umbali wa mita 500 kwa mawe madogo na kilometa moja kwa mawe makubwa yenye urefu wa kilometa 202, kwamba kilometa 350 zinatarajiwa kuwekewa mipaka.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema kazi hiyo inakwenda vizuri licha ya vikwazo katika baadhi ya maeneo ikiwamo kung'olewa mawe na kukwanguliwa rangi zilizopakwa.

Kutokana na tatizo hilo aliiomba Kamati ya Ulinzi na Usalama kufanya doria za mara kwa mara katika maeneo yote yaliyowekewa mipaka.

Dereva bodaboda akiendesha pikipiki akiwa amevaa kandambili jambo linalodaiwa ni hatari kwa usalama wake. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wachimbaji madini walia ukosefu umeme migodini

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WACHIMBAJI wa madini ya dhahabu wilayani Chunya, wanalazimika kutumia mafuta ya taa na dizeli katika shughuli zao hali ambayo hutumia gharama kubwa kununua nishati hiyo ili kazi zao zifanyike.

Kutokana na hali hiyo, Mbunge wa Jimbo la Chunya mkoani Mbeya, Masache Kasaka ameuomba Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (REA) kuharakisha ujazilizi wa nishati hiyo katika maeneo yote ya shughuli za uchimbaji ili kuokoa gharama.

Kasaka alisema maeneo mengi yenye shughuli za uchimbaji wa madini hayana huduma ya nishati ya umeme, hivyo kuzinduliwa usambazaji wa umeme kutasaidia maeneo hayo kufikiwa.

"Nawaomba sana REA muyafikie maeneo yote yanayofanya shughuli za uchimbaji madini ili kuwapunguzia gharama ya matumizi ya ununuzi wa nishati kama vile mafuta ya taa na dizeli ambapo hulazimika kutumia jenereta kufanya shughuli hizo usiku na mchana, uwapo na umeme utapunguza gharama na kuongeza ufanisi," alisema Kasaka.

Mitaa na vitongoji 3,000 vya Mkoa wa Mbeya vinatarajiwa kufikiwa na huduma ya umeme baada ya REA kuzindua usambazaji mkoani humo, lengo likiwa ni maeneo yote kupata nishati hiyo.

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini alisema kuwa maeneo yote ambayo hayakufikiwa na umeme katika awamu hii yatapata nishati hiyo.

Alisema gharama ya umeme huo zitakuwa ni Sh. 27,000 kwa kila kaya, hivyo aliwatahadharisha wananchi kutokubali kuongezewa gharama kupata nishati hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa REA, Mhandisi Hassan Said, alisema Sh. bilioni 10.5 zitatumika kukamilisha mradi huo ambao utakamilika katika kipindi cha miezi 18 kuanzia sasa na kumtaka mkandarasi wa mradi huo kushirikiana na viongozi wa maeneo ya miradi.

Alisema kilometa 147 zitafikiwa na umeme wa REA ambapo wateja 3,127 wataunganishiwa huduma ya nishati hiyo, sambamba na ufungaji wa vituo 61 kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma.

Mkandarasi anayetekeleza mradi huo kutoka Kampuni ya Derm Electrics Tanzania Limited, Mhandisi Peter Mbwambo, alimhakikishia Dk. Tulia kuwa hadi Desemba mwaka huu watakuwa wamekamilisha kilometa zote 147 za mradi.

Alisema licha ya kudai kumaliza Desemba lakini wataendelea kuwa eneo la kazi kama mkataba unavyoonesha kipindi cha miezi 18 kutoa huduma mbalimbali kwa wateja wenye uhitaji.

Wakazi wa Mtaa wa Mtakuja ulioko Kata ya Iganjo Halmashauri ya Jiji la Mbeya, walisema mradi huo umekuja wakati muafaka kwani kutokana na ukata wa fedha walishindwa kuunganishwa na umeme wa kutoka TANESCO.

# Wanaume wanaopigwa na wake zao watakiwa kuripoti

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WANAUME mkoani Mbeya wamehamasishwa kuripoti matukio ya vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa na wenza wao bila kuogopa, ili kukomesha wimbi la vitendo hivyo.

Mkurugenzi wa Shirika la Freedom House nchini, Daniel Lema, alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu mwitikio wa wanaume katika kuripoti matukio ya ukatili kwenye vyombo vya sheria.

Licha ya kuhamasisha wanaume kutoogopa kuripoti vitendo wanavyofanyiwa alidai baadhi ya sheria zinampa nguvu zaidi mwanamke kuliko mwanaume katika kudai haki hali inayosababisha kukosa ujasiri wa kuripoti pindi wanapotendewa.

Alisema wanashindwa kudai haki za msingi pindi wanapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na haki nyingine kwa sababu sheria zilizoko zinampa nafasi zaidi mwanamke. Alisema hali hiyo inasababisha wanaume kukaa na dukuduku moyoni kutokana na kukosa msaada wa kisheria na nasaha na hatimaye kufanya maamuzi ambayo yanagharimu maisha yao na wengine.

"Kwa sasa wanaume wanakosa nguvu ya kufanya maamuzi na kuchukua hatua kutokana na sheria zilizoko kutowapa nguvu ya kudai haki zao ukilinganisha na wanawake ambao wana majukwaa na taasisi mbalimbali za kuwasemea na kuwapatia msaada wa kisheria, tunahitaji na sisi tupatiwe madawati na majukwaa ya kusemea tunayopitia," alisema Lema.

Alisema faida ya kuwapo kwa majukwaa yanayotetea na kulinda haki za wanaume itasaidia kupatikana kwa haki na usawa baina ya mwanaume na mwanamke lakini itapunguza vitendo vya ukatili ikiwamo mauaji, ubakaji ulawiti na vipigo. Mkurugenzi wa Shirika la Empower Youth Prosperity (EYP), Ipyana Mwakyusa, alisema wanaume wanapaswa kueleza magumu wanayopitia ili kujadiliana namna ya kuyakabili.

Alisema wanapaswa kujadili namna ya kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo kuiomba serikali kufungua majukwaa mbalimbali ili kuwasaidia wanaume kuwasilisha vikwazo vyao.

"Ni muhimu kuwasaidia wanaume kufunguka na kuweka mikakati ya pamoja katika kujiponya na matatizo mbalimbali ndani ya ndoa zao kama vile afya ya akili," alisema Mwakyusa.

Mkurugenzi wa Nasaha Hub, Sylvester Mwashiuya, alisema msongo wa mawazo kwa wanaume umechangia kwa kiasi kikubwa kufanya maamuzi ambayo yanagharimu maisha yao na wengine.

Alisema hali hiyo inatokana na kukosa sehemu ya kutoa dukuduku zao na kupata tatizo la afya ya akili ambalo ndilo linaongoza kwa wanaume wengi ambao huchukua maamuzi ya kujiua.







Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (kulia), akimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Chacha (katikati), walipokutana kikazi wilayani humo juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wajasiriamali wampongeza Samia kuruhusu mikutano

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAJASIRIAMALI mkoani Dodoma wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kuviruhusu vyama vya siasa nchini kufanya mikutano ya hadhara baada ya kuwapo kwa zuio la muda mrefu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo, Katibu wa Wajasiriamali Mkoa wa Dodoma, Christopher Dioniz, alisema hali hiyo itasaidia kuongeza ushindani katika medani za kisiasa nchini.

Alisema kitendo cha serikali kuruhusu mikutano ya vyama vya siasa kutasaidia kujiimarisha kutokana na ukosoaji utakaokuwa ukifanywa na wapinzani kupitia mikutano yao ya hadhara.

"Lakini mikutano ya vyama vya siasa itaisaidia serikali kujitathmini kutokana na kukumbushwa na wapinzani ahadi zake ambazo iliahidi katika Ilani ya uchaguzi kupitia chama kilichoingiza madarakani,"alisema Dioniz.

Aidha, alisema kuruhusiwa kwa mikutano hiyo kutachochea maendeleo ndani ya nchi kutokana na kuwapo kwa uhuru wa kuikosoa serikali katika utekelezaji wa mambo mbalimbali na vyama pinzani kujiimarisha kisiasa tofauti na ilivyo sasa.

"Tunaipongeza sana serikali kupitia Rais Samia Suluhu Hassan kwa kauli yake ya kuruhusu kuanzia sasa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara ili kujiimarisha kwa kuendelea kukutana na wanachama wao na kujitengenezea wanachama wapya," alisema.

Kadhalika, aliwashahuri viongozi wa vyama vya siasa nchini kuitumia vizuri fursa hiyo kwa kufanya shughuli zao bila kuwapo kwa uvunjifu wa sheria zilizoko.

"Kama Rais Samia alivyotoa angalizo kuwa wanasiasa wafanye shughuli zao kwa mujibu wa sheria na siyo kuitumia vibaya fursa hiyo kwa kuanza kufanya mikutano ambayo italeta uvunjifu wa amani na kubaguana,"alisema Dioniz.

Vilevile alisema kufanyika mikutano ya hadhara ni haki ya vyama vya siasa kisheria hivyo ni wajibu wao kuhakikisha kuwa wanailinda haki hiyo.

Marufuku ya kufanyika kwa mikutano ya vyama vya siasa nchini ilitolewa mwaka 2016 muda mfupi baada ya kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Tano.

Rais Samia juzi alitangaza kuruhusu mikutano hiyo Ikulu Dar es Saalam, alipokuwa akihutubia mkutano wa viongozi wa vyama vya siasa zaidi ya 19.

Kwenye mkutano huo Rais Samia alisema: "Nimekuja kutangaza kuondoa zuio la mikutano ya hadhara na ninasema kwamba sasa linaondoka."

Hata hivyo, alisema mikutano hiyo ni haki kisheria kwa vyama vya siasa kuiendesha huku akisisitiza kuwa serikali imejipanga kutekeleza wajibu wake wa kuilinda mikutano hiyo.

# RC awatangazia kiama wazazi watakaowaficha wanafunzi

**Na Ibrahim Joseph,** CHEMBA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amewataka wazazi na walezi wa wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu wa masomo kuhakikisha watoto wao wanaripoti kwenye shule walizopangiwa kwa wakati.

Aidha, amesema serikali itawafuatilia wanafunzi wote watoro wakati shule zitakapofunguliwa na mzazi au mlezi atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Senyamule, alitoa agizo hilo jana alipokuwa akizungumza na baadhi ya wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika wilayani hapo.

Aidha, aliwataka wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka huu kuhakikisha wanafika shuleni ndani ya muda uliopangwa na serikali na siyo vinginevyo.

"Serikali yetu ya Mkoa wa Dodoma itahakikisha inawafuatilia mwanafunzi wote watoro waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza pamoja wale wa vidato vingine,"alisema Senyamule. Kadhalika, alisema serikali imeweka mazingira mazuri kwa kujenga vyumba vya madarasa na hakuna mwanafunzi aliyechaguliwa atacheleweshwa masomo.

Senyamule alisema ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa mkoa huo umekamilika na wanafunzi wote wataanza masomo yao kwa wakati.

Vilevile aliwataka wananchi hao kuzitumia mvua zilizoanza kunyesha msimu huu wa masika kwa kupanda mazao yanayostahimili hali ya hewa ya kanda ya kati ili kusiwapo na uhaba wa chakula. Senyamule aliwataka wananchi kutumia mbolea wakati wa kupanda ili kufanikiwa katika kilimo hicho.

Alisema serikali imetoa ruzuku kwenye mbolea hivyo wasipochangamka kuagiza mikoa mingine watachukua kwa sababu wanauhitaji mkubwa.

Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Chacha, alisema wilaya hiyo imejenga vyumba vya madarasa ya sekondari 46 kutokana na fedha walizopewa na serikali.

Alisema wilaya hiyo ilipokea Sh. milioni 920 ambazo zitatumika kwa ajili ya ujenzi na kununua samani za shule.

Chacha alisema ujenzi huo ulianza Septemba 2021, na wanatarajia kukamilisha kwa asilimia 100 ifikapo Januari 15, mwaka huu.

Hata hivyo alisema pamoja na kukamilisha ujenzi huo kuna baadhi ya shule walikuwa bado hawajakamilisha samani za madarasa hayo, lakini wanatarajia hadi siku ya kufunguliwa kwa shule zitakuwa zimekamilika.

# Rasimu ya uboreshaji kilimo, uzalishaji chakula yaandaliwa

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

SERIKALI imeandaa rasimu ya utekelezaji wa mkakati maalum wa kitaifa wa uboreshaji wa kilimo hai na uzalishaji wa vyakula asilia nchini utakaozinduliwa na kuanza utekelezaji Juni mwaka huu.

Kilimo hai ni mfumo wa jumla wa usimamizi wa uzalishaji ambao unakuza na kuimarisha afya ya mfumo ikolojia wa kilimo, ikijumuisha bayoanuwai, mizunguko ya kibaiolojia, na shughuli za kibiolojia za udongo.

Vyakula asilia ni bidhaa zinazotokana na mfumo wa usimamizi wa shamba ulioidhinishwa kwa kutumia mbinu za ufugaji wa ardhi na mbinu za mwongozo wa kibaiolojia badala ya pembejeo za awali.

Mkakati huo wa kitaifa unatarajia kutekelezwa kwa kipindi cha miaka nane, unaratibiwa na Wizara ya Kilimo unalenga kujenga uelewa kuhusu kilimo hai kwa wakulima na wadau husika, kwa kuongeza uzalishaji wa tija, pamoja na soko la bidhaa za mazao ya kilimo hai nchini.

Miongoni mwa mambo mengine, mkakati huo unalenga kuhakikisha nchi inakuza kilimo cha asili ili kutoa fursa muhimu kwa umma kuchagua ama kutumia vyakula vinavyotokana na kilimo asili, au vile vinavyotokana na kilimo cha mfumo wa kawaida.

Akifanya mahojiano maalum na Nispahe jana, Mwenyekiti wa mkakati huo, Mshauri wa Sera na Mratibu wa Kitaifa wa Ushirikishwaji wa Vijana katika Kilimo katika Wizara ya Kilimo, Revelian Ngaiza, alisema mkakati huo ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya kitaifa ya kilimo hai kama ilivyoainishwa katika Sera ya Taifa ya Kilimo, 2013 (NAP 2013).

Alifafanua kabla ya kuandaa rasimu ya mkakati huo, walifanya ziara maalumu katika maeneo yote ya ikolojia ya kilimo nchini ili kubaini ufanisi wa wakulima kwenye kilimo hai lakini upatikanaji na soko la mazao ya kilimo hai.

Alisema: "Tulifanya utafiti huo wa kina katika mikoa kadhaa, ikiwamo Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Mbeya, Songwe, Singida, Simiyu, Mwanza, Tabora, Katavi, Kigoma, Kagera, Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Morogoro na Dar es Salaam."

Ngaiza alieleza kuwa utekelezaji wa mkakati huo utahusisha masuala kadhaa, ikiwa ni pamoja na kushinikiza kuboreshwa kwa uzalishaji wa mbegu bora za kienyeji, dawa za kuulia wadudu na pembejeo.





# Msitu wa Jozani, Ghuba ya Chwaka zapandishwa hadhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MSITU wa Taifa ya Jozani na Ghuba ya Chwaka Zanzibar, zimepandishwa hadhi na kuwa hifadhi hai.

Hatua hiyo inaifanya Tanzania kuwa na misitu ya hifadhi hai mitano, miongoni mwa hifadhi hizo ni Manyara, Serengeti na Usambaa.

Kupandishwa hadhi kwa msitu huo kumetokana na jitihada na ushirikiano mzuri baina ya wanajamii na serikali katika kuendeleza uhifadhi na kukidhi vigezo vya hifadhi hai vilivyowekwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO).

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa hifadhi hiyo Makamu wa kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud alisema hifadhi hai ni miongoni mwa neema na faraja kubwa kwa watu wote katika ulimwengu ambao unaishi na fikra ya dunia.

Othman aliwataka wadau na washirika kuhakikisha kwamba hifadhi hiyo inalindwa ili kutimiza malengo ya kuisaidia Zanzibar kuongeza pato kutokana na sekta ya utalii kwa wageni wengi kutembelea msitu huo.

Alisema kwamba kutokana na umuhimu wa kuwapo kwa hifadhi hiyo sambamba na matakwa ya kisheria, Serikali ya Zanzibar imeona ni vyema kutangulia kuizindua na baadaye kuendelea na taratibu nyingine za kiutekelezaji kwa faida ya nchi na jamii kwa jumla.

Aidha, Othman alitaka kuchukuliwa juhudi za ziada kupandisha hadhi pia Msitu wa Hifadhi wa Kimaumbile wa Ngezi-Vumawimbi Pemba, ambao kwa kipindi kilichopita ulishindwa kupanda hadhi kutokana na upungufu uliosababisha kukosekana kwa vigezo muhimu vya kupandisha hadhi hiyo.

Alisema kutokana na hali hiyo kunahitajika jitihada za makusudi na Msitu wa Ngezi nao utimize vigezo muhimu vinavyohitajika ili kupanda hadhi ya kiwango cha hifadhi hai.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo, Shabani Seif Mwinyi, alisema Msitu wa Chozani ni kitovu cha hifadhi hai ya taifa na 1950, msitu huo ulitangazwa rasmi kuwa msitu wa hifadhi ukiwa na ukubwa wa hekta 2,512 na mwaka 1960 uliteuliwa kuwa Hifadhi ya Kimaumbile.

Alisema katika mwaka 2004 msitu huo ulipandishwa tena hadhi kupitia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuwa hifadhi ya taifa pekee kwa Zanzibar na ikiwa na ukubwa wa hekta 5,000.

Alisema msitu huo kwa sasa unahekta 21,274 na ina maeneo matatu makuu ikiwamo eneo la ukanda wa kiini lenye hekta 263.

Alitaja eneo lingine ni la ukanda wa kinga lenye hekta 4,227 na eneo la matumizi lenye hekta 14,684 ambalo linajumuisha matumizi yote ya binadamu ikiwamo kilimo, mifugo na makazi.

Aidha, alisema hifadhi hiyo imepata hadhi kwa kuwa na sifa tatu ikiwamo kuwapo kwa baiolojia anuwai nyingi ambazo nyingine ni adimu duniani ikiwamo kima punju, ushirikishwaji bora kwa jamii na kuwapo kwa mfumo mzuri wa mgawanyo wa faida na hasara baina ya jamii na serikali.

Alisema msitu huo ni miongoni mwa misitu muhimu ya Ukanda wa Pwani ya Afrika Mashariki inayohifadhi baiolojia anuwai nyingi na za kipekee zinazotambulika kitaifa na kimataifa.

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji na Maliasili, Shamata Shaame Khamis, alisema kuna jitihada zilizofanyika kuupandisha daraja msitu huo jambo linalochangia kuwapo kwa ongezeko kubwa la wageni wanaotembelea hifadhi.

Alisema kwa mwaka 2022 kuanzia Januari hadi Novemba, jumla ya wageni 52,666 walitembelea hifadhi hiyo na kuchangia kuingiza Sh. bilioni . 1.19, huku fedha za kigeni zilizokusanywa zikiwa zaidi ya Dola za Marekani 68,000.

Aidha, alisema katika mwaka 2021, wageni 58,902 walitembelea hifadhi hiyo na kuingiza Sh. bilioni 1.56 ikiwa ni ada za kiingilio katika kipindi cha Januari hadi Desemba.

Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dk. Menan Hunewe Jangu, alisema Tanzania ni moja wapo ya nchi 131 duniani zinazotekeleza zana ya hifadhi hai na Tanzania kuna hifadhi hai tano za msitu. Alisema miongoni mwa faida za hifadhi hai kufahamika na kujitangaza kimataifa kupitia mtandao wa kidunia, kusaidia kupata miradi mbalimbali ya maendeleo na kuwa na uchumi wa buluu na kijani na huleta fursa za kiutalii.




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman (kushoto), akifungua kitambaa kuashiria uzinduzi wa Hifadhi Hai ya Jozani Ghuba ya Chwaka katika hafla iliofanyika Mkoa wa Kusini Wilaya ya Kati Unguja, ikiwa ni shamrashamra za Miaka 59 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kulia ni Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wavuvi wachagizwa kukitumia kiwanda cha boti za Fibre

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Uwekezaji Kiuchumi, Mudrik Ramadhani Soraga, amewataka wavuvi na wakulima wa mazao ya baharini kukitumia kiwanda cha kutengeneza boti za Fibre kununua na kufanya ukarabati wa boti wakati zimeharibika. Kiwanda hicho kinamilikiwa na Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM).

Alitoa rai hiyo wakati akifungua jengo la kiwanda hicho ikiwa ni sehemu ya sherehe ya kumbukumbu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema KMKM kwa kushirikiana na mwekezaji wa kizalendo wamefanya jambo la kihistoria kuwa na ushirikiano wa kuanzisha kiwanda hicho cha kutengeneza boti ni jambo jema ambalo halitasahaulika. Alisema uanzishaji wa kiwanda hicho ni jambo zuri na linapaswa kupongezwa kwa wazalendo hao na wapiganaji wa kikosi hicho kuwa na ari kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Mwinyi kuupa msukumo uchumi wa buluu nchini.

"Hiki kiwanda kitawasaidia sana watu wetu wakitumie na naamini gharama za matengenezo na ukarabati hazitokuwa ghali ukilinganisha na matengenezo ya nchi za ng'ambo, kitumieni ni fursa nzuri kwenu,"alisema Soraga.

Aidha, alisema kuwa kiwanda hicho kina ubora kutokana na boti zote 500 alizotoa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na atazoendelea kuzitoa ni kutoka katika Kampuni ya Makame ambayo kwa sasa ndio washirika wa KMKM.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Malum za Vikosi vya SMZ, Issa Mahfudh, alisema kiwanda hicho hadi kinakamilika kimetumia Sh.milioni 96. Mkuu wa Mafunzo wa kiwanda hicho kutoka KMKM, Muhaed Suleiman Khamis alisema lengo la kujenga kiwanda hicho ni kuunga mkono Dk. Mwinyi.

# Hospitali Mnazi Mmoja kushirikiana na China kutibu macho

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa kitengo cha macho katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja, Dk. Ahmed Muumin, amesema kitengo hicho kinaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa baada ya kuanzisha utaratibu mpya.


Alisema chini ya utaratibu mpya huduma za kliniki za macho zinatolewa kwa huduma za upasuaji kwa wagonjwa wa macho kwa kushirikiana na madaktari kutoka China.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kufuatia malalamiko yanayotolewa na baadhi ya wagonjwa na wafanyakazi ambao wagumu kubadilika na kwenda na wakati wa sasa.

Alisema kitengo cha macho kimelazimika kuweka utaratibu mpya ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wagonjwa, huku kikikabiliana na matatizo ya ongezeko la idadi ya wagonjwa wa macho, upungufu wa madaktari pamoja na vifaa.

Aidha, alisema idadi ya wagonjwa waliopokelewa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja imepungua kwa mwaka 2022 ambao walikuwa 17,661 ukilinganisha na mwaka 2021 walikuwa 24,386.

Hivyo, aliwataka madaktari katika vituo vya afya vya mjini na vijijini kuwahudumia vizuri wagonjwa wa macho ili kuipunguzia mzigo hospitali hiyo.







Wajumbe wa kamati ya kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto (MTAKUWWA) katika kata za Tinde na Masengwa wilayani Shinyanga wakiwa kwenye kikao cha kupanga mikakati na kupitisha maadhimio ili kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo mimba na ndoa za utotoni, kikao hicho kiliandaliwa na Shirika la Women Elderly Advocacy and Development Organization (WEADO) juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Madereva daladala watishia kugoma kisa ushuru

**Neema Emmanuel na Rose Jacob,** MWANZA

MADEREVA wa daladala mkoani Mwanza wametishia kugoma kutoa huduma kutokana na serikali kuwatoza ushuru kila wanapovuka wilaya moja kwenda nyingine.

Wamesema endapo hali itaendelea watasitisha huduma hiyo kwa sababu kipato wanachopata ni kidogo ikilinganishwa na ushuru wanaolipa kwa kila siku.

Walitoa kauli hiyo jana wakati wakizungumza na waandishi wa habari.

Walisema kuwa daladala za kutoka Nyashishi wilayani Misungwi kuelekea Kisesa wilayani Magu zinalipa ushuru katika vituo vinne kwa siku.

Wakizungumza na Nipashe, madereva hao walisema Manispaa ya Ilemela kuanzia juzi ilipandisha ushuru huo kutoka Sh. 1,000 hadi Sh. 1,500 kwa gari moja kwa siku.

Mmoja wa madereva waliozungumza na Nipashe (jina limehifadhiwa) alisema magari yanayofanya safari zake katika wilaya nne wanalazimika kulipa ushuru katika kila kituo wanapovuka wilaya moja kwenda nyingine.

Alitoa mfano alisema gari ikitoka Nyashishi kwenda Kisesa inalipa ushuru wilayani Misungwi, Nyamagana, Ilemela na Kisesa.

Dereva mwingine, Allen Ladiansi alisema Wilaya ya Ilemela ushuru wake kuanzia jana ulipanda na kufikia Sh. 1,500 badala ya Sh. 1,000, Nyamagana Sh. 1,000, Misungwi Sh. 500 na akifika Kisesa ambayo ni Wilaya ya Magu analipa Sh. 500.

Alisema ushuru huo unalipwa na dereva na mwenye gari hahusiki nao na wala hakubali fedha zake kukatwa kwa siku.

Madereva hao walisema kwa kuwa wanatoa huduma katika mkoa mmoja, ushuru huo ungekuwa unalipwa katika kituo kimoja badala ya kulipia kila wanapovuka wilaya moja kwenda nyingine.

Walisema licha ya kulipa ushuru huo lakini maeneo mengi ya vituo ni machafu na kwamba wanaona kama fedha wanazolipa ni kubwa ikilinganisha na kipato wanachopata kwa siku.

Akizungumzia suala hilo Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Madereva wa Daladala mkoani Mwanza, Emmanuel Deus, alisema kupandishwa ushuru katika Halmashauri ya Ilemela kutoka Sh.1,000 hadi Sh.1,500, walikataa kikao cha makubaliano.

"Katika kikao tulichokaa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Ilemela ambaye aliwakilishwa na Ofisa Mipango wa Halmashauri hiyo, tulikubaliana ziondolewe bajaji ambazo zimekuwa zikikwamisha biashara ya daladala na kusababisha tukose abiria, lakini tunashangaa hawajatekeleza hilo badala yake wameanza kutoza ushuru wa Sh. 1500, jambo ambalo siyo sahihi," alisema Deus.

Alisema walikubaliana kuitishwa kikao kingine kujadili suala hilo, lakini anashangaa kuona jana wameanza kupandisha ushuru bila wao kufahamu suala hilo.

Alisema wana wanachama 3,880 ambao wote wanaendesha daladala mkoani Mwanza na kwamba yeye gari analoendesha kwa sasa analipa ushuru wa Sh. 5,500 kwa siku.

Alisema akitoka Wilaya ya Misungwi analipa Sh. 2,000, Nyamagana Sh. 2,000 na akifika Ilemela analipa Sh. 1,500.

Akizungumzia suala hilo, Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilemela, Apolinary Modest alisema suala la kupandisha ushuru wilayani humo, lilitakiwa lianze Julai 2022, lakini walikaa kikao na viongozi wa daladala wakakubaliana suala hilo lianze Januari 2023.

Alisema walifikia hatua hiyo kwa lengo la kuongeza mapato ya halmashauri hiyo ili iweze kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kuhusu kuondolewa bajaji barabarani alisema suala hili haliwezekani kwa kuwa na wao wana haki ya kufanya biashara.

# Shekhe akerwa ukiukwaji maadili walimu madrasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHEKHE wa Msikiti wa Tinde wilayani Shinyanga, Hemed Rashidi, amechukizwa na baadhi ya walimu wa madrasa wanaofanya vitendo vya udhalilishaji ikiwamo ulawiti watoto.

Alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha uchechemuzi cha kamati ya maalum ya kupinga ukatili dhidi ya wanawake na watoto kilichowakutanisha wajumbe kutoka Kata ya Tinde, Masengwa na viongozi wilayani Shinyanga kilichoandaliwa na Shirika la WEADO.

Alisema anapinga vitendo vya ukatili vinavyofanywa na baadhi ya walimu wa madrasa dhidi ya watoto na kueleza kwamba wamekuwa wakichafua Uislamu ambayo ina malengo ya kutoa mafundisho ya kiimani kwa watoto.

"Nachukizwa sana ninaposikia kwenye taarifa za habari mwalimu wa madrasa amelawiti watoto, napinga vitendo hivi, huku ni kuichafua dini," alisema Shekhe Rashidi.

Naye Mchungaji wa Kanisa la PAGT Masengwa wilayani Shinyanga, Edward Mashala, alisema vitendo vya ukatili vinapaswa kupigiwa kelele kwenye nyumba za ibada ili elimu hiyo isambae kwa watu wote.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Nice Munissy alitaka kila mtu awe mlinzi wa mwenzake na ili kufichua vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa watoto katika jamii.

Alisema serikali wilayani humo itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo, huku akiwataka watoto kutoa taarifa kwa viongozi wa baraza lao wanapooona viashiria vya kufanyiwa vitendo vya ukatili ili zichukuliwe hatua mapema kuzuia madhara yasitokee.

Ofisa Miradi kutoka WEADO, Winnie Hinaya, alisema wamekutanisha kamati hizo ili kujadiliana na kupanga mikakati mipya ya kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani Shinyanga.

# Watakiwa kuitumia mitandao ya kijamii kujenga umoja

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera wametakiwa kutumia mitandao ya kijamii kujenga umoja na mshikamano katika jamii ili kusaidia kutatua matatizo yanayowakabili.

Ushauri huo ulitolewa jana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Kagera, Toba Nguvila, wakati wa kukabidhi nyumba ya kuishi kwa Jarida Abdu (35) mkazi wa Kijiji cha Marahara katika Kata ya Maghata-Karutanga yenye thamani ya Sh. milioni 10.

Nyumba hiyo imejengwa kwa msaada wa kundi la mtandao wa Whatsapp la New Muleba Breaking News lililoanzishwa na baadhi ya wazawa wa Wilaya ya Muleba.

Nguvila alisema kuwa yapo baadhi ya makundi yanaanzishwa badala ya kubuni masuala ya kusaidia jamii, yanatumika kutukana watu na kuponda viongozi wakati kuna matatizo mengi ambayo wanaweza kuyajadili na kuweka mipango ya namna gani ya kuyatatua.

"Kwa hiyo makundi kama haya ya Whatsapp yasiwe ni siasa tu, kutukanana na kuponda watu wengine hiyo siyo sahihi, kundi hili liwe mfano wa kuigwa na mengine na ifikie hatua wahusika wafahamu kwamba wanaweza kuleta maendeleo ya mtu mmoja mmoja, jamii, mkoa na taifa kwa ujumla, kupitia ubunifu wa wanakikundi," alisema Nguvila.

Mama huyo alijengewa nyumba hiyo baada ya kupata maradhi ya kidonda sugu katika mguu wa kushoto wakati akiishi na mume wake na baada ya muda mfupi ilidaiwa alianza kunyanyaswa na kunyanyapaliwa.

Baada ya manyanyaso hayo mwanamke huyo aliondoka na kurejea nyumbani kwao huku akiwa hana msaada wa matibabu.

Mbali na kujengewa nyumba hiyo, kundi hilo pia lilitumia Sh. milioni 4.5 kugharamia matibabu ya mama huyo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando iliyoko mkoani Mwanza.

Akizungumzia tatizo hilo mama huyo alisema kuwa alifikia hatua akashindwa hata kutembea na kwamba aliishakata tamaa ya kupona na kwamba aliwahi kufanya jaribio la kujiua kwa kunywa sumu.

Akizungumza baada ya kukabidhi nyumba hiyo, kiongozi wa kundi hilo, Halfan Abubakary alisema waliamua kumsaidia mama huyo baada ya kuona video yake mtandaoni akilia na kulalamika alivyotelekezwa na mume wake baada ya kuugua.

Alisema baada ya mama huyo kurejea nyumbani kwake walikwenda kumtembelea na walipofika walikuta mazingira anayoishi siyo ya kuridhisha na wakaamua kuanza kuchanga fedha kwa ajili ya kujenga nyumba na choo.

MAKALA MAALUM

MAZIKO YA PAPA

# Hivi ndivyo hutangazwa kifo cha Papa



**Na Mwandishi Wetu**

WAUMINI wa Kanisa Katoliki Duniani na watu wa madhehebu mengine, wanaomboleza kifo cha aliyekuwa kiongozi wa kanisa hilo, Papa Benedict XVI.

Pamoja na kwamba waumini hao na jamii ya watu wote wamejawa huzuni kwa kuondokewa na mtu huyo mashuhuri, hadi anafariki dunia, hakuwa kiongozi aliyeko madarakani kutokana na kustaafu kutokana na umri pamoja na maradhi yaliyokuwa yakimsumbua. Kwa maneno mengine huyo ni papa mstaafu au kiongozi mstaafu wa Kanisa Katoliki.

Kifo chake kimeshtua dunia licha ya kwamba mara kwa mara habari za afya yake kutetereka zilikuwa zikirushwa na vyombo vya habari likiwamo Shirika la Habari la Vatican (Vatican News). Hata kifo chake, habari za kwanza zilitolewa na Vatican News.

Yako mengi ambayo yameelezwa kuhusu sifa za Papa Benedict XVI, Kiongozi wa Vatican na mzaliwa wa Ujerumani. Lakini itoshe kwamba alikuwa mmoja wa viongozi wabobezi wa kiroho katika historia ya kanisa.

Pamoja na kwamba Papa Benedict XVI, ambaye jina lake halisi lilikuwa Joseph Reitzinger, iko siri ambayo wengi hawaijui kuhusu uthibitisho wa kifo cha Papa aliyeko madarakani. Uthibitisho huo haukufanywa kwa Papa Benedict XVI kwa kuwa hakuwa madarakani wakati anafariki dunia lakini kwa walioko madarakani kuna hatua maalum hufuatwa.

Wakati Papa aliyeko madarakani anafariki dunia, kama ilivyokuwa kwa Papa John Paul II, kuna utaratibu maalum wa kuthibitisha kabla ya kutangazwa kwa umma. Inapotokea hivyo, mtu wa kwanza kupewa taarifa ni mkuu wa masuala ya utawala katika ofisi ya Papa (Vatican). Huyu kwa nafasi yake anaitwa Camarlego.

Kabla ya kuliarifu kanisa juu ya kifo cha Papa, Camarlego atasimama katika mwili wa Papa na kumwita kwa jina lake la ubatizo mara tatu akiwa amezungukwa na jopo la makardinali. Iwapo hakutakuwa na jibu lolote kutoka kwa Papa, itatangazwa rasmi kwamba amefariki dunia.

Baada ya kuwa Papa ametangazwa kuwa amefariki dunia, Camarlego huiondoa pete ya papa kidoleni na kuikatakata vipande mbele ya jopo la makardinali.

Camerlengo ni nani?

Huyu ni ofisa wa ngazi ya juu katika ofisi ya Papa, makao makuu ya Kanisa Katoliki ambaye pamoja na mambo mengine, jukumu lake kubwa ni kusimamia mali na mapato ya Kanisa. Kwa ngazi ya cheo katika kanisa, huyo mara yingi anakuwa kardinali.

Ziko sababu kadhaa kwa nini pete hiyo ambayo pia ina muhuri wa Papa hukatwakatwa vipande. Moja ya sababu, na pengine kubwa ni kuzuia kughushi nyaraka. Sababu nyingine ni ishara ya mwisho wa Papa kuwapo madarakani. Pete ya Papa ni ishara ya mamlaka, hivyo hakuna pete hakuna mamlaka.

Kitendo hicho cha kuthibitisha kwamba Papa amefariki dunia, ni wakati wa Vatican kusambaza taarifa kwa waumini na serikali za mataifa duniani kupitia vyombo vya habari vikiongozwa na Vatican News.

Kabla ya kusambazwa kwa taarifa duniani, Camerlengo huwasiliana kwanza na mkuu wa jopo la makardinali na baadaye kuwasiliana na makardinali wengine na mabalozi wa Vatican katika nchi mbalimbali. Ikumbukwe kwamba Vatican ni sehemu ya Rome nchini Italia lakini ina mamlaka kamili. Papa kama Askofu Mkuu wa Vatican ndiye Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani na ana serikali yake yenye mamlaka kamili. Papa huteua wakuu mbalimbali wakiwamo mabalozi wanaoiwakilisha Vatican katika mataifa mbalimbali duniani.

Baada ya kutangazwa kwa kifo chake, ndipo shughuli za mazishi hufuata kutokana na taratibu za Kanisa Katoliki. Mazishi ya Papa hufanyika siku ya nne hadi ya sita baada ya kifo chake licha ya kwamba maombolezo hufanyika kwa siku tisa tangu kifo chake.

Pamoja na kwamba kanisa ndilo husimamia shughuli zote za mazishi, Papa ndiye hupanga mazishi yake yaweje na kuacha maagizo kwa Camerlengo kwa utekelezaji.

Mwisho wa maziko ya Papa hufuatiwa na mchakato wa kumpata Papa mpya kwa jopo la makardinali kukutana kwa ajili ya kutekeleza hilo. Lakini kwa tukio la kifo cha Papa Benedict XVI tukio hilo halipo kwa kuwa yuko Papa aliyeko madarakani, Papa Francis ambaye alichaguliwa baada ya papa Benedict kustaafu.

**•Makala hii imeandaliwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali vya habari.**



# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**NURUH SALOME MSAMI,** AMEPOTEZA PASSPORT YAKE YA KUSAFIRIA YENYE NAMBA **TAE247271** ILIYOTOLEWA TAREHE 26/11/2019. AMEPOTEZA MAENEO YA KINYEREZI, ILALA, DAR ES SALAAM. YEYOTE ATAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. **DAR/STA/RB/94921/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FAUSTA KALOWELA NYONI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya NISSAN yenye namba za usajili **T 498 CZV** chasis namba **RGE24030230,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote polisi. Polisi taarifa **SO/RB/792/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ASHERY MHOLOTO WELYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI-CARRY** yenye namba za usajili **T 712 BD**W chasis namba **SJLOT125264,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **SO/RB/7739/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUHUDINI RAMADHANI SHEMSANGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA-HILUX** yenye namba za usajili **T 657 AVQ** chasis namba **AHTFK22G603029627**,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **SO/RB/7898/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PHILBERT EXUSPER NEMES** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 669 DDZ – TOYOTA SALOON.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DOD/DOD/RB/4330/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EVELYNE NARCIS NGUNGURUTIN** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 872 BGY – TOYOTA HILUX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/5712/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GEORGE NCHIMBI LINGOWE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 888 CLK - TOYOTA MARKX.** Chassis no **GRX1200003127.** Engine NO **4GR0033464.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKB/RB/01/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JENIFA SALVATORY KISHE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 563 EBG - SUBARU FORESTER 2014 NEW MODEL.** Chassis namba **SJG023044.** Engine namba **FA201813551.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: ***DAR/CHU/RB/1161/2023.***

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NICOLAUS ALOIS KIRIA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 989 DMG – TOYOTA RUSH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/56/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**KOSTA MATHIAS KAHISE** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 164 DFS – KING LION.** Chassis namba **L7GPCKLY3N1011470.** Engine namba **KL162FMJN5011470.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MKO/TR/RB/02/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**TEKLEHAIMANOT ASMEROM KIFLE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **RAV 4** yenye namba za usajili **T 801 AFR** chasis namba **sxaii0055607** engine namba **3s6901977,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/5081/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**G S GROUP LIMITED** inatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HAOJUE** yenye namba za usajili **MC747 DGR** chasis namba **LC6PCJK26N0011016,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **SO/RB/766/2022**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# MAMA DANGOTE, ZUCHU MAMBO YAO SAFI

**Na Mwandishi Wetu**

MAMA wa nyota wa muziki wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, Sanura Kassim maarufu kama Mama Dangote, ameonekana kuwa na uhusiano mzuri na anayedaiwa kuwa mkwe wake mtarajiwa, Zuchu.

Katika siku za hivi majuzi, Mama Dangote amekuwa akimzungumzia vema binti huyo na nguli wa taarab, Khadija Kopa na kuonyesha upendo mkubwa kwake kupitia mitandao ya kijamii.

Jumanne, mama Diamond alichapisha picha ya Zuchu akiwa amevalia gauni refu la kijani kibichi na kusema kuwa vazi hilo ni sahihi kwa ajili ya harusi ya Kiislamu.

"Zuchu... Ndio Nguo ya ndoa kwa Waislamu," aliandika chini ya picha hiyo.

Posti hiyo ilikuja kabla ya chapisho lingine ambapo alikuwa akitangaza tamasha la Zuchu nchini Comoro lililopangwa kufanyika Jumamosi wiki hii.

Mama Dangote alitoa wito kwa Wacomoro kujitokeza kwa wingi kwenye shoo hiyo na kudokeza kwamba ataungana nao.

"Habari zenu wapenzi wa Comoro, nimefurahi sana kuwa miongoni mwenu tarehe 7 Januari, 2023 kwa ajili ya "Tamasha la mwaka" pale Uwanja wa Malouzini kwa shoo ya kukumbukwa. Njooni wote tutaburudika."

# Burna Boy awaomba radhi mashabiki

**LAGOS,** Nigeria

NYOTA wa muziki wa Afrobeat kutoka Nigeria, Burna Boy, ameomba msamaha kwa mashabiki baada ya kukosolewa kwa kuchelewa kutumbuiza kwenye tamasha ambalo alipanda jukwaani na kutumbuiza kwa saa chache Jumatatu.

Katika taarifa yake kwenye mtandao wa Instagram, mwanamuziki huyo aliwalaumu waandaji kwa kuchelewa kwake katika tamasha hilo lililopewa jina la Love Damini ambalo lilifanyika Lagos, Nigeria.

"Muundo wa miundombinu haukuwa sawa na ilikuwa ngumu kwa upande wangu na hata vyombo vya sauti havikuwa sawa," aliandika mwanamuziki huyo

Aliongeza: "Ninaomba radhi kwa mashabiki wangu kwa jinsi ilivyokuwa, asante kwa kukaa na kustahimili dhoruba pamoja nami."

Alisema atafanya kazi na wawekezaji kujenga miundombinu ya kiwango cha kimataifa katika tasnia ya burudani ya Nigeria

Mwimbaji huyo ni miongoni mwa wanamuziki wa Kiafrika waliofanikiwa zaidi.



# Nyota Ndogo ataka kuona vitukuu

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII kutoka Mombasa, Nyota Ndogo, kupitia kwenye ukurasa wake wa Instagram amewaacha wanamitandao wakimtumia jumbe za heri njema ya kuzaliwa baada ya kujiandikia ujumbe wa kipekee.

Msanii huyo alindika kuwa anatamani Mungu aweze kumzeesha hadi atakapowaona vitukuu wake.

"Happy birthday to Nyota Ndogo. Leo nimeingia 42, ninafurahia kuongeza mwaka mwingine Mungu azidi kuniongezea miaka ili nami nione vitukuu," alindika Nyota Ndogo.

Mashabiki wake walimtumia jumbe za kumtakia kheri njema.



# MSHINDI CHOMOKA NA NDINGA YA PARIMATCH AKABIDHIWA GARI LAKE

**Na Mwandishi Wetu**

Mkazi wa Lindi, Hamidu Abdallah, amekabidhiwa rasmi gari yake aina ya Toyota Urban Cruiser, yenye thamani ya Sh. milioni 65 baada ya kuibuka mshindi wa promosheni ya Chomoka na Ndinga kutoka Parimatch.

Promosheni hiyo iliyodumu kwa siku 35 kuanzia Novemba 22 hadi Desemba 26, mwaka jana, iliwapa wateja wa kampuni hiyo nafasi ya kujishindia zawadi za simu mbili kila siku, bodaboda mbili kila mwisho wa wiki na droo ya mwisho mshindi kujinyakulia zawadi ya gari mpya kabisa.

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Parimatch Tanzania, Erick Gerald, wakati akikabidhi gari hilo kwa mshindi na kuwashukuru wateja wote ambao wameshiriki na baadhi yao kujishindia zawadi mbalimbali ikiwamo simu na bodaboda ambazo tayari walishazitoa.

"Tunayo furaha kubwa katika kipindi hiki cha mwaka mpya kumkabidhi mshindi wetu wa gari ya aina Toyoya Urban Cruiser, gari hili ni jipya kabisa yaani zero kilometa. Tunawashukuru wateja wetu nchi nzima walioshiriki kwenye promosheni hii ya siku 35 ambayo imemalizika mwishoni mwa mwezi wa Disemba 2022," alisema Gerald. Kwa upande wa mshindi wa gari hilo, Hamidu, aliwashukuru Parimatch Tanzania kwa kuweza kutimiza ndoto yake ya kumiliki gari kutoka katika Kampeni ya Chomoka na Ndinga.

"Wakati napigiwa simu, nilikuwa nyumbani nimelala maana siku hiyo kulikuwa na mvua kubwa, sikuweza kuamini kwa haraka ila baadaye nilipopigiwa tena na kupata ile taarifa kwamba nimeibuka mshindi, nilifurahi sana kwani sikutegemea kabisa kuwa ningeibuka mshindi katika promosheni hii, jambo hili naliona kama ndoto kwangu," Hamidu alisema kwa furaha.

Kampuni ya Parimatch ndio kinara wa michezo ya kubashiri mtandaoni na imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya ukaribisho ya asilimia 100 hadi kufikia Sh. 1,000,000 kwa wateja wapya wanaojiunga nao.

Parimatch imekuwepo nchini Tanzania tangu mwaka 2019, ikitoa huduma nzuri ikijumuisha malipo ya haraka, odds kubwa na promosheni za kusisimua kwenye soka, kasino na michezo ya virtual. Mbali na soka, kampuni ya Parimatch pia hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye tenisi, UFC, mpira wa vikapu, kriketi, baseball na michezo mingine mingi ya Live na pre-match.




Mkurugenzi wa Parimatch Tanzania, Erick Gerald (kulia), akimkabidhi Hamidu Abdallah kutoka Lindi, funguo ya gari aina ya Toyota Urban Cruiser baada ya kuibuka mshindi wa Promosheni ya Chomoka na Ndinga ya Parimatch. Makabidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

# *Medo ataka vifaa vitatu Dodoma Jiji*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji ipo kwenye mazungumzo na wachezaji wawili kwa ajili ya kuwaongeza kwenye kipindi hiki cha dirisha dogo kwa ajili ya kukiimarisha kikosi hicho, imeelezwa.

Afisa Habari wa klabu hiyo, Mosses Mpunga, amesema viongozi wa klabu hiyo wapo kwenye mazungumzo baada ya Kocha Mkuu, Melis Medo, kupendeleza kusajiliwa wachezaji watatu wapya ambao wataingia moja kwa moja kikosini, wakati huu ambao mmoja ameshasajiliwa.

"Kocha Mkuu Medo amewasilisha ripoti yake kwa uongozi ambapo ametaka asajiliwe wachezaji watatu ambao wataingia moja kwa moja kwenye kikosi, lakini tayari tumeshasajili mchezaji mmoja ambaye ni Adeyum Suleiman, hivi sasa uongozi unaendelea na mazungumzo na wachezaji wawili hatutoweza kuwataja kwa sasa, tukishamaliza tutawatangaza," alisema Mpunga.

Pamoja na hayo alisema baadhi ya wachezaji wao ambao walikuwa majeruhi kwa muda mrefu wamepona, hivyo kumpa wigo mpana kocha huyo wa kuchagua wachezaji.

Dodoma Jiji ambayo haikuanza vema kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, imeonekana kuzinduka hasa baada ya ujio wa Medo aliyechukua nafasi ya Mrundi Masoud Djuma.

Hata hivyo, wachambuzi wa masuala ya soka wanasema kurejea tena kuutumia uwanja wa nyumbani, Jamhuri Dodoma uliokuwa umefungiwa, badala ya Uwanja wa Liti, Singida pia kumewasaidia. Timu hiyo inashika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 21 kwa michezo 19 iliyocheza mpaka sasa.

Inatarajiwa kushuka tena dimbani Januari 14, mwaka huu kucheza dhidi ya Geita Gold kwenye Uwanja Jamhuri Dodoma.

# Paralympic kurindima Machi Dar es Salaam

**Na Shufaa Lyimo**

MICHUANO ya Watu wenye Ulemavu Tanzania (Paralympic), yanatarajiwa kutimua vumbi mwanzoni mwa Machi mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam jana, rais wa Kamati ya Paralympic Tanzania (TPBC), Tuma Dandi, alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yanaendelea vizuri na kudai kila mchezaji sasa anatamani siku hiyo ifike mapema.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri, kila mchezaji anajifua kuhakikisha anafanya vizuri katika mashindano hayo ambayo yatashirikisha timu za Tanzania Bara," alisema Dandi.

Rais huyo alisema, itachezwa michezo mbalimbali ambapo alitaja michezo itakayochezwa siku hiyo kuwa ni riadha, kunyanyua vitu vizito na kikapu.

Alisema washindi watakaopatikana kwenye mashindano hayo watapata nafasi ya kuingia timu ya taifa ambayo itakuwa inajiandaa na mashindano ya Afrika yatakayofanyika Mei mwaka huu nchini Ghana.

# Riadha ya vijana kwa Mpaka kesho

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi ya mchezo wa riadha mkoa wa Dar es Salaam, yanatarajiwa kufanyika kesho kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, ambayo yatashirikisha wanariadha wenye umri wa miaka 17.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Kocha Mkuu wa timu ya Riadha Mkoa wa Dar es Salaam, Idd Muhunzi, alisema lengo la mashindano hayo ni kutafuta wachezaji ambao watаunda timu ya taifa ambayo itakwenda kushiriki michuano ya olimpiki mwaka huu nchini Uingereza.

"Lengo la kufanya mashindano hayo, tunataka tuwe na timu ya taifa ambayo itakwenda kutuwakilisha kwenye michuano ya olimpiki inayotarajiwa kufanyika nchini Uingereza ,"alisema Muhunzi.

Kocha huyo alisema mashindano kama hayo watakuwa wanayafanya kila mwezi ili wapate timu imara itakayokwenda kuipeperusha vema bendera ya taifa.

Alisema mtu yeyote ambaye ana kipaji anaruhusiwa kushiriki kwenye mashindano hayo na ambaye atakidhi vigezo moja kwa moja atapewa nafasi ya kujiunga na timu hiyo, hivyo anawaomba Watanzania kujitokeze kwa wingi uwanjani hapo.

## ZISIKUPITE

### WAN-BISSAKA KUUZWA
MANCHESTER United bado inaweza kumuuza beki wa England, Aaron Wan-Bissaka.dirisha la Januari hii, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, kuonyesha kiwango bora hivi karibuni. (***Athletic***)

### CHELSEA KUIPIKU ARSENAL
CHELSEA inajipanga kufanya jaribio la mwisho kuwania kuipiku Arsenal katika mbio za kumsajili winga wa Shakhtar Donetsk na Ukraine, Mykhailo Mudryk, licha ya 'Washikabunduki' hao kuafikiana na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. (***Sun***)

### FERNANDEZ APANDIWA BEI
KLABU ya Chelsea inafikiria kufikia euro 120 katika mkataba wa kiungo wa kati wa Argentina na Benfica, Enzo Fernandez, mwenye umri wa miaka 21. (***Telegraph***)

### DEPAY KUREJESHWA UNITED
KIUNGO wa kati wa Uholanzi, Memphis Depay, amekuwa akihusishwa na kurejea Manchester United, lakini kocha wa Barcelona, Xavi, anataka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 abaki Nou Camp. (***Metro***)

### THURAM SAFI NEWCASTLE
NEWCASTLE United imemaliza harakati zao za kumnunua mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach na Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 25. (Football Insider)

### LEEDS KUMZUIA MESLIER
CHELSEA, Newcastle United na Bayern Munich zinavutiwa na golikipa wa Leeds United, Illan Meslier, lakini klabu hiyo ya Elland Road haitaki kumuuza Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 22. (***RMC Sport***)

### TIELEMANS MKATABA MPYA
KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers bado anatumaini kuwa klabu hiyo inaweza kufikia mkataba mpya na kiungo wa kati wa Ubelgiji, Youri Tielemans mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake unakamilika msimu wa majira ya joto. (***Goal***)


### SCHADE KUTUA BRENTFORD
KLABU ya Brentford inakaribia kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani, Kevin Schade kwa pauni milioni 22 kutoka Freiburg baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kufaulu vipimo vya afya. (Times)

### PRESSLEY KWA MKOPO
MSHAMBULIAJI wa Brentford mwenye umri wa miaka 21, kutoka Scotland, Aaron Pressley, amekubali mkataba wa kujiunga na Accrington Stanley kwa mkopo. (***Football Insider***)

### ARSENAL KUMUUZA CEDRIC
ARSENAL iko tayari kumuuza beki wa kulia wa Ureno, Cedric Soares, lakini uhamisho wa kwenda Fulham unazuiliwa na matakwa ya mshahara ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. (***Evening Standard***)

### ARCHER NA MIDDLESBROUGH
KLABU ya Middlesbrough ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili mshambuliaji wa Aston Villa, Cameron Archer, mwenye umri wa miaka 21. (***TeamTalk***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA ALALAMA ARSENAL KUNYIMWA PENALTI 2 EPL

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amelalamika kwa kile alichokiita kunyimwa penalti mbili ambazo hazikutolewa kwa timu yake, huku wakilazimishwa suluhu na Newcastle United kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumanne usiku.

**Sare hiyo ilikuwa mara ya kwanza kwa Arsenal kudondosha pointi kwenye Uwanja wa Emirates msimu huu, huku wakikosa nafasi ya kuongoza kwa pointi 10 dhidi ya Manchester City wanaoshika nafasi ya pili.**

Arteta alionyesha hasira yake baada ya Arsenal kunyimwa penalti katika dakika za lala salama wakati mpira ulipogonga mkono wa mlinzi wa Newcastle, Jacob Murphy kwenye eneo la hatari.

Pia, Arteta anaamini kwamba, walitakiwa kupewa penalti na mwamuzi, Andy Madley wakati Dan Burn alipovuta jezi ya Gabriel kwenye eneo la hatari.

> ●●● Tulikuwa na nafasi nyingi ndani na nje ya eneo la sanduku kufanya vizuri zaidi na tukanyimwa...

"Ninajivunia jinsi tulivyocheza, jinsi tulivyotawala mchezo, mbinu tuliyokuwa nayo tangu mwanzo," alisema Arteta baada ya mchezo huo.

"Lakini tulikuwa na nafasi nyingi ndani na nje ya eneo la sanduku kufanya vizuri zaidi na tukanyimwa penalti mbili za haki kabisa. Ni penalti au si penalti? Zote ni penalti."

Kocha wa Newcastle, Eddie Howe, yeye alikuwa na maoni tofauti na akaongeza kuwa hakukuwa na suala kati yake na Arteta licha ya wawili hao kukabiliana katika dakika za mwisho.

"Ni wazi katika hatua hiyo ya mchezo kila mmoja alikuwa na shauku, vijana walijitoa," aliiambia Sky Sports.

"Sikufikiri ilikuwa penalti kwa sababu tu ya ukaribu, lakini huwezi kujua. Mimi na Mikel, tunaweza kuwa sawa au si sawa."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,063,6
MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
MANCHESTER CITY
1 | 4.86
X | 3.88
2 | 1.70
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa




# TEN HAG: BAHATI IMEIBEBA UNITED

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United lazima wawe “wanapambana zaidi” baada ya kufaidika na bahati nzuri katika ushindi wa Jumanne wa 3-0 dhidi ya Bournemouth kwenye Ligi Kuu, kwa mujibu wa Kocha, Erik ten Hag.

United walijivuta pointi sawa na Newcastle United walio katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu pamoja na pointi tano mbele ya Tottenham waliopo katika nafasi ya tano - huku Casemiro, Luke Shaw na Marcus Rashford kila mmoja akifunga bao kwenye Uwanja wa Old Trafford katika ushindi huo.

‘Mashetani Wekundu’ hao wanaonekana kujipanga vema kutinga hatua ya nne bora baada ya kushinda mechi nne mfululizo za ligi.

Lakini baada ya kuona David de Gea akiokoa vema na kuwanyima Philip Billing na Jaidon Anthony mabao ya wazi wakati United walikuwa mbele kwa mabao 2-0, Ten Hag alichanganyikiwa na kile alichokiona kuwa ni kukosa udhibiti.

“Nimefurahishwa na matokeo. Leo haukuwa mchezo wetu bora,” alisema akiiambia BBC Sport.

“Lazima tuwe makini na tupambane, hatukucheza kwa akili kama timu.

“Tulitengeneza mabao mazuri, lakini wakati fulani tulikuwa na bahati sana, na tulikuwa na uokoaji mzuri kutoka kwa David. Tungeweza kuwa bora zaidi kama timu.

“Kulikuwa na nafasi kubwa kwa kuongoza 2-0, wakati mwingine inatubidi kushika mpira na kutambua wakati wa kwenda kufunga. Hiyo ni hatua inayofuata.”

# *Conte atoa msimamo kuondoka Spurs*

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, amesisitiza kuwa anafuraha katika klabu hiyo kwa sasa, lakini amedokeza kuwa anaweza kuondoka kama “hatashawishiwa kwa asilimia 100” na maelekezo ya klabu hiyo.

Mkataba wa kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, unamalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa klabu hiyo ina chaguo la kuongeza mwaka mmoja zaidi.

Mustakabali wake unazua mjadala mkubwa huku Spurs wakisuasua katika azma yao ya kuendelea naye.

Conte alitoa ujumbe Jumanne wakati mazungumzo yakiendelea kuhusu mkataba mpya huku kukiwa na kuzorota kwa hali ambayo imeifanya Spurs kushinda mechi tatu pekee kati ya 10 zilizopita katika michuano yote.

“Mwanzoni kwangu haikuwa rahisi,” alisema Conte.

“Huu ni uzoefu muhimu. Nilikubali kufanya hivi kwa sababu nimepata klabu kubwa, klabu ya kisasa na kwa sababu hii nina furaha kufanya kazi hapa. Nilipata watu ambao wanataka kuwa chanya na kujaribu kuunda timu upya.

“Vinginevyo, kama watu hawa wangeniambia ‘lazima tushinde’ ningesema ‘samahani lakini huu si wakati sahihi wa kufikiria kwamba katika mwaka mmoja lazima ushinde taji.

“Sasa, kazi ni hii, changamoto yangu kubwa ni hii: kuendelea kufanya kazi kwa nguvu na wafanyakazi wangu na wachezaji, kuboresha klabu, kujenga msingi imara.

“Nikiridhika kuendelea kufanya kazi hii na siku moja nione matokeo yake nitaendelea kubaki, nisiposhawishika kwa asilimia 100 basi naweza kuacha kazi yangu hapa.

“Ni kazi kubwa tunayofanya pamoja. Naijua vizuri ni nini na ni muhimu. Kazi yangu ni hii.”



605,974/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/01/23 | 18:00 | KAS Eupen vs Royal Charleroi SC | 2.65 | 3.55 | 2.44 |
| 02. 07/01/23 | 18:00 | Millwall FC vs Sheffield United | 2.90 | 3.20 | 2.43 |
| 03. 07/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Burnley FC | 2.32 | 3.40 | 2.90 |
| 04. 07/01/23 | 18:00 | Cambridge United vs Bristol Rovers | 2.85 | 3.30 | 2.41 |
| 05. 07/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Cheltenham Town | 2.50 | 3.25 | 2.75 |
| 06. 07/01/23 | 18:30 | RKC Waalwijk vs SC Heerenveen | 2.43 | 3.50 | 2.70 |
| 07. 07/01/23 | 20:30 | Brentford FC vs West Ham United | 2.65 | 3.25 | 2.65 |
| 08. 07/01/23 | 22:00 | Fortuna Sittard vs Go Ahead Eagles | 2.60 | 3.30 | 2.65 |
| 09. 07/01/23 | 22:45 | Royal Antwerp FC vs KAA Gent | 2.44 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 07/01/23 | 23:00 | Espanyol Barcelona vs Girona FC | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 08/01/23 | 14:30 | US Salernitana vs Torino FC | 3.20 | 3.20 | 2.25 |
| 12. 08/01/23 | 15:30 | Bristol City vs Swansea City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 13. 08/01/23 | 17:00 | Spezia Calcio vs US Lecce | 2.55 | 3.10 | 2.85 |
| 14. 08/01/23 | 18:00 | SV Zulte Waregem vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.70 | 3.70 | 2.32 |
| 15. 08/01/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs GD Chaves | 2.85 | 3.25 | 2.46 |
| 16. 08/01/23 | 18:45 | Excelsior Rotterdam vs FC Groningen | 2.65 | 3.55 | 2.45 |
| 17. 08/01/23 | 19:00 | Fenerbahce Istanbul vs Galatasaray Istanbul | 2.39 | 3.50 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 05/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 11:30 | 2774 | Hangzhou NG vs Jinan Xingzhou | 1.09 | 8.15 | 17.47 |
| 13:30 | 1551 | Teraktor Sazi vs Esteghlal Tehran | 3.46 | 2.78 | 2.22 |
| 13:30 | 3764 | Malavan Bandar Anzali vs Naft Masjed Soleyman FC | 1.93 | 3.11 | 3.84 |
| 14:00 | 2393 | Tiddim Road Athlectic Club vs Sudeva Delhi FC | 1.52 | 3.79 | 5.64 |
| 14:00 | 5511 | SP. Braga U23 vs FC Famalicao U23 | 1.94 | 3.60 | 3.26 |
| 14:30 | 1535 | MES Rafsanjan vs Peykan FC | 2.01 | 2.76 | 4.17 |
| 14:30 | 5310 | Sepahan Esfahan vs Sanat Mes Kerman FC | 1.42 | 3.63 | 8.14 |
| 15:30 | 5462 | Persepolis FC vs Nassaji Mazandaran | 1.45 | 3.55 | 7.78 |
| 15:30 | 5838 | Dhamk vs Al Raed Club | 1.81 | 3.65 | 4.10 |
| 16:15 | 3041 | FC Veria vs Makedonikos FC | 1.65 | 3.45 | 4.86 |
| 16:15 | 4007 | Al Rayyan SC vs Al-Sailiya SC | 1.90 | 3.37 | 3.61 |
| 16:30 | 5153 | Sanat Naft Abadan vs Gol Gohar | 4.36 | 3.00 | 1.86 |
| 17:00 | 3550 | FC Goa vs Hyderabad FC | 2.41 | 3.30 | 2.62 |
| 17:00 | 4842 | Gaziantep BB vs Basaksehir | 3.19 | 3.34 | 2.16 |
| 18:00 | 3083 | Sporting CP U23 vs Estrela Amadora U23 | 3.07 | 3.70 | 1.99 |
| 18:00 | 4491 | Gimnastic Tarragona vs Osasuna | 4.79 | 3.99 | 1.63 |
| 18:00 | 4565 | Al Nasr Riyadh vs AL Tai | 1.24 | 5.80 | 11.00 |
| 18:00 | 4774 | AS Tel Aviv University W vs Maccabi Bnot Emek Hefer W | 3.20 | 4.40 | 1.89 |
| 18:00 | 5509 | Enppi Club vs Al Ahly Cairo | 7.55 | 4.37 | 1.40 |
| 18:00 | 5528 | CD Ibiza Islas Pitiusas vs Betis | 13.91 | 6.36 | 1.18 |
| 18:25 | 5648 | Al Ahli Doha SC vs Al Arabi Doha SC | 4.75 | 4.07 | 1.55 |
| 20:00 | 1026 | Trabzonspor vs Giresunspor | 1.47 | 4.28 | 6.17 |
| 20:00 | 2229 | Karmiotissa vs Aris Limassol | 6.20 | 4.20 | 1.49 |
| 20:00 | 2404 | Adana Demirspor vs Istanbulspor | 1.40 | 4.77 | 6.56 |
| 20:00 | 5083 | Zamalek vs El Daklyeh | 1.34 | 4.69 | 8.78 |
| 20:15 | 4661 | CRS Salmi vs FAR Rabat | 3.98 | 3.15 | 1.88 |
| 20:30 | 4424 | Hapoel Afula vs Hapoel Kfar Saba | 2.27 | 3.16 | 2.91 |
| 20:30 | 4637 | Al Wehda vs Al Shabab Riyadh | 5.00 | 4.20 | 1.58 |
| 20:30 | 4750 | Al Ittihad Jeddah vs Al Hilal Riyadh | 2.66 | 3.41 | 2.50 |
| 21:00 | 1270 | MS Kiryat Gat W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.01 | 13.64 | 48.72 |
| 21:00 | 5675 | Leixoes vs Moreirense | 3.26 | 3.21 | 2.14 |
| 21:30 | 2080 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Hapoel Petach-Tikva W | 2.45 | 3.95 | 2.45 |
| 22:30 | 5733 | Wydad Casablanca vs Sccm Chabab Mohammedia | 1.33 | 4.28 | 8.57 |
| 23:00 | 2218 | Chelsea vs Manchester City | 4.86 | 3.88 | 1.70 |
| 23:00 | 5956 | CD Eldense vs Athletic Bilbao | 8.35 | 5.17 | 1.31 |
| 23:15 | 2135 | Santa Clara vs Sporting Braga | 4.89 | 3.79 | 1.65 |

IJUMAA - 06/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 02:00 | 3527 | Universidad Catolica vs Oriente Petrolero | 1.48 | 3.57 | 7.04 |
| 04:05 | 1054 | CF Atlante vs Alebrijes De Oaxaca | 1.63 | 3.46 | 5.07 |
| 06:05 | 3756 | Dorados vs Correcaminos Uat | 1.97 | 3.41 | 3.36 |
| 09:05 | 3034 | Melbourne Victory W vs Perth Glory W | 1.44 | 4.65 | 5.23 |
| 11:45 | 5077 | Melbourne Victory vs Brisbane Roar | 1.92 | 3.49 | 3.73 |
| 20:00 | 3971 | PAU FC vs Montpellier | 4.17 | 3.58 | 1.80 |
| 20:30 | 2522 | Elche vs Celta Vigo | 3.55 | 3.25 | 2.08 |
| 22:00 | 1066 | Jong AZ Alkmaar vs Heracles Almelo | 3.65 | 3.80 | 1.83 |
| 22:00 | 1452 | NAC Breda vs Jong PSV | 2.17 | 3.41 | 3.01 |
| 22:00 | 1588 | Den Bosch vs Jong Utrecht | 2.03 | 3.50 | 3.25 |
| 22:00 | 2012 | PEC Zwolle vs Almere City | 1.63 | 3.89 | 4.63 |
| 22:00 | 4421 | Twente vs Emmen | 1.47 | 4.26 | 6.14 |
| 22:00 | 4440 | Jong Ajax vs FC Eindhoven | 2.08 | 3.60 | 3.06 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SINGIDA BIG STARS YAFUNGUKA JEZI YA TAMBWE KWA KAZADI

**Na Saada Akida,** Zanzibar

UONGOZI wa Singida Big Stars umefunguka kwa kutoa ufafanuzi kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wao, Hamis Tambwe, ndani ya klabu hiyo baada ya jezi yake namba 17 kuonekana ikivaliwa na straika mpya aliyesajiliwa katika dirisha hili dogo, Kazadi Kasengu.

Tambwe hayuko visiwani Zanzibar na timu hiyo inayoshiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi huku jezi yake namba 17 ikivaliwa na Kazadi na taarifa zikidai kuwa mshambuliaji huyo wa zamani wa Klabu za Simba na Yanga, ametemwa na Singida Big Stars.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa timu hiyo, Ibrahim Mirambo, alisema Tambwe bado yuko katika mipango yao na hayuko kikosini kutokana na ruhusa maalum aliyopewa baada ya kuomba kwenda kwao nchini Burundi kwa ajili ya matatizo ya kifamilia.

Alisema mbali na Tambwe si wachezaji wote walioambatana na timu, akiwamo Pascal Wawa pamoja na Ibrahim Ajib, ambaye ni usajili mpya, na kwamba nyota hao watajiunga na timu hiyo ndani ya wiki hii.

"Kutokuwapo kikosini kwa Tambwe na jezi namba 17 ambayo anaivaa kuvaliwa na nyota mwingine ambaye yuko katika majaribio, haina maana tumeachana na mshambuliaji huyo, bali ameomba ruhusa ya kwenda kwao Burundi kwenye matatizo yake ya kifamilia.

"Uongozi umemruhusu na umempa muda aliomba kwenda kumaliza matatizo hayo na atarejea hivi karibuni na kujiunga na wenzake kikosini," alisema Mirambo.

Alipotafutwa Tambwe alikiri kuwapo kwao Burundi kwa ajili ya mapumziko mafupi na atarejea nchini kujiunga na timu yake kuendelea na majukumu ya kusaidia katika raundi ya 20 ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kazadi ambaye ni raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, alikuwa 'pacha' wa Fiston Mayele wa Yanga wakati wakiwa AS Vita Club.

Mchezaji huyo alicheza mechi yake ya kwanza Jumatatu, wakati SingidaBig Stars ilipoichapa KMKM mabao 2-0 kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi, Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

MILIKI...



Wachezaji wa timu ya mpira wa kikapu ya vijana, Julio Mtaki (kushoto), akipiga hesabu ya kumtoka Isaac Kakoko wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya JK Park jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mgunda ampa faili Robertinho

INATOKA UKURASA 32

ili kuwapa nafasi ya kuonyesha uwezo wao, kwa sababu hatuwezi kuwahukumu wakati hatukuwapa nafasi," alisema Mgunda.

Kikosi cha Simba leo kitakuwa na kibarua kingine katika mchezo wa pili wa mashindano hayo ya Mapinduzi kikivaana na KVZ inayonolewa na aliyewahi kuwa mchezaji na Kocha Msaidizi wa Wekundu wa Msimbazi hao, Amri Saidi.

## *Mudathir ahofia namba Yanga*

INATOKA UKURASA 32

ubingwa," alisema Kamwe.

Yanga imeboresha kikosi chake katika usajili wa dirisha dogo kwa ajili ya kujiandaa na raundi ya 20 ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho Afrika.

Mudathir atakuwa na kibarua kigumu cha kuwania namba sambamba na viungo wawili mahiri wa Yanga, Khalid Aucho na Salum Abubakar Sure Boy, ambao wamekuwa na kiwango kizuri katika timu hiyo.



# Michezo

Alhamisi Januari 5, 2023

Nipashe




Arteta alalama Arsenal kunyimwa penalti UKURASA 29

# Mudathir ahofia namba Yanga

●●● Asema ana kazi kubwa kumshawishi Nabi mazoezini kutokana na ubora wa nyota wengi, hivyo...

**Na Saada Akida,** Zanzibar

KIUNGO mpya wa Yanga, Mudathir Yahya, amekisoma vema kikosi cha timu hiyo nakusema ana kazi kubwa ya kuonyesha kiwango kizuri ili kumshawishi Kocha Nasreddine Nabi kumpa nafasi katika kikosi cha kwanza.

Mudathir amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia Yanga na kuungana na kikosi cha timu hiyo moja kwa moja visiwani Zanzibar, kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi inayoendelea katika Uwanja wa Amaan.

Kiungo huyo mkabaji aliwahi kuichezea Azam FC kabla ya kuachana na miamba hiyo ya Chamazi katika usajili wa dirisha kubwa na kisha kujiunga na KMKM kwa ajili ya kufanya mazoezi kulinda kiwango chake.

Akizungumza na gazeti hili jana katika mazoezi yake ya kwanza na timu yake hiyo mpya kwenye Uwanja wa Mao visiwani hapa, Mudathir alisema amefurahi kuwa sehemu ya kikosi cha Yanga na anapaswa kuongeza juhudi mazoezini ili kuingia katika kikosi cha kwanza.

**Alisema anatambua amesajiliwa katika timu yenye wachezaji wazuri na anakutana na ushindani mkubwa wa namba, hivyo anapaswa kujituma zaidi ili kutowaangusha waliomsajili.**


"Ni kweli kocha Nabi, amependekeza usajili wangu, natakiwa kupambana na nina majukumu makubwa ya kuwashawishi benchi la ufundi kunipa nafasi katika kikosi cha kwanza, lazima nionyeshe kitu tofauti katika mazoezi," alisema Mudathir.

Alisema alipoondoka Azam FC alirejea kwao Zanzibar na kujiunga na timu ya KMKM kwa ajili ya kufanya mazoezi ili kulinda kiwango chake, hivyo kwa sasa yuko fiti na tayari kuitumikia Yanga muda wowote katika mechi.

Naye Ofisa Habari wa Yanga, Ally Kamwe, alisema ujio wa nyota huyo ndani ya Yanga ni usajili wa ubingwa kwa sababu ni miongoni mwa wachezaji ambao kocha wao, Nabi amependekeza.

"Benchi la ufundi limefanya tathmini kubwa ya mechi 19 za ligi tulizocheza na kuona tunahitaji mtu kama Mudathir atakayekuja kuongeza nguvu kikosini na kufanikiwa katika malengo yetu ikiwamo kutetea taji letu la

INAENDELEA UK. 31



Mudathir

# Mgunda ampa faili Robertinho

**Na Saada Akida,** Zanzibar

KOCHA Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, amesema ameshaandaa mafaili ya tathmini ya kikosi cha timu hiyo pamoja na michuano ya Ligi Kuu Tanzania Bara na tayari kwa kumkabidhi bosi wao mpya, Robertinho Oliver.

Simba ilimtambulisha Kocha Mkuu, Robertinho juzi ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili na jioni ya siku hiyo kawasili visiwani Zanzibar, ambapo usiku alishuhudia timu yake hiyo ikishushiwa kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Mlandege FC kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi inayoendelea katika Uwanja wa Amaan.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mgunda alisema amepewa taarifa juu ya ujio wa bosi wao huyo mpya na tayari ameandaa mafaili ya tathmini ya kikosi cha Simba katika michezo 19 iliyopita na ijayo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema benchi lake la ufundi wanamkaribisha kocha huyo na watatoa ushirikiano mkubwa katika kupiga kazi kwa lengo moja tu ambalo ni kufikia yanayotarajiwa na Wanasimba.

"Nifahamu ujio wa Kocha Mkuu ('Robertinho), kwa sasa sina neno juu ya uwezo wake ila natambua ni kocha mwenye uwezo mkubwa na tayari nimeshaandaa faili kwa ajili ya kumkabidhi bosi wangu ili kuanza kufanyia kazi rasmi," alisema Mgunda.

Kuhusu kupoteza mechi ya kwanza ya Kombe la Mapinduzi, Mgunda alisema yote hayo ni sehemu ya mchezo wa mpira wa miguu ambapo ukifanya makosa unaadhibiwa.

Alisema walitengeneza nafasi wakashindwa kuzitumia na wapinzani wao (Mlandege), walipata nafasi moja na kuitumia kwa kufunga bao la ushindi na kusonga mbele katika hatua ya nusu fainali.

"Kila kitu kimeonekana wazi, viwango vilivyoonyeshwa na mapungufu ya wachezaji wangu tumeyaona na jopo letu la makocha tunaenda kufanyia kazi ili kujipanga kwa mechi ijayo.

Hii mechi nimewatumia wachezaji ambao hawapati nafasi ya kucheza mara kwa mara ndani ya timu yetu

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042